**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. Masoud Ali Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |
| 9. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. | Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge. |
| 11. | Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. | Mhe. Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. Mhe. | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake |
| 19. Mhe. | Abdalla Abasi Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 20. Mhe. | Ali Abdulgulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 21. Mhe. | Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 22. Mhe. | Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |
| 29. Mhe. | Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 30. Mhe. | Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 31. Mhe. | Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 32. Mhe. | Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 33. Mhe. | Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 34. Mhe. | Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 35. Mhe. | Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 36. Mhe. | Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 37. Mhe. | Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. | Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 39. Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 40. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 41. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 42. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 43. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 44. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 45. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 46. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 47. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 48. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 49. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |
| 50. Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 51. Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 57. Mhe. | Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. Mhe. | Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. Mhe. | Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 63. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 64. 5Mhe. | Sabiha Filfil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 65. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **66. Mhe.** | **Salma Mussa Bilal** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **67. Mhe.** | **Suleiman Makame Ali** | **-** | **Jimbo la Ziwani** |
| **68. Mhe.** | **Suleiman Haroub Suleiman** | **-** | **Jimbo la Kiembe Samaki** |
| **69. Mhe.** | **Sulubu Kidongo Amour** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |
| **70. Mhe.** | **Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **71. Mhe.** | **Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Jimbo la Micheweni** |
| **72. Mhe.** | **Shaib Hassan Kaduara** | **-** | **Jimbo la Chake Chake** |
| **73. Mhe.** | **Yahya Rashid Abdulla** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **74. Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **75. Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **76. Mhe.** | **Zawadi Amour Nassor** | **-** | **Jimbo la Konde** |

**Ndg. Raya Issa Msellem** - **Katibu**

**Kikao cha Pili – Tarehe 11 Febuari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 33**

**Daftari la Wapiga Kura**

**Mhe. Hassan Hamad Omar**– Aliuliza**:-**

Afisi yako iliweka Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na kufanya uboreshaji wa daftari kwa wale ambao walikuwa hawajafikia umri wa kupiga kura na sasa tayari wamefikia umri wa kupiga kura.

(a) Je, uboreshaji wa Daftari la Kudumu hutakiwa kutolewa kwa yule ambaye tayari alikwisha kuwemo ndani ya daftari.

(b) Je, kigezo gani kilichotumika kuwatoa wapiga kura waliotangulia kuwemo ndani ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

(c) Je, utalitatua vipi suala hilo ili kuepusha ukiukwaji wa haki za wapiga kura katika uboreshaji wa Daftari katika chaguzi zinazokuja ndani ya nchi yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Utaribu na Baraza la Wawakilishi –** Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c), kwanza naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliweka Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kufanya uendelezaji na uhakiki wa Daftari hilo kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ili kuwa na Daftari sahihi la Wapiga Kura kwa Uchaguzi huo. Kufanya hivyo ni moja ya hatua za kutekeleza wa matakwa ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 4 ya 2018 vifungu vya 5, 11, 31 na 32 vya Sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa vifungu hivyo vya Sheria, Tume ya Uchaguzi inapaswa kupanga tarehe na maeneo ya uandikishaji wa wapiga kura na kufanya uendelezaji wa Daftari hilo ili kuwa na Daftari linaloendana na wakati na lenye wapiga kura wenye sifa tu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa ruhusa yako sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, uboreshaji au uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura hauna lengo la kumtoa au kumfuta mpiga kura ambaye ana sifa za kuwemo katika daftari, na badala yake una lengo la kuwaingiza wapiga kura waliotimiza sifa na kuwatoa wapiga kura waliopoteza sifa. Lakini pia kuhamisha wapiga kura walioomba kwa ridhaa yao kuhamishwa au kufanya masahihisho ya taarifa za wapiga kura kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Uchaguzi wa mwaka 2020 wapiga kura waliofutwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wanajumuisha makundi yafuatayo:-

i. Wapiga kura waliofariki dunia;
ii. Wapiga kura ambao hawakufanya uhakiki wa taarifa zao katika Daftari; na
iii. Wapiga kura waliopoteza uraia au kutumikia kifungo katika vyuo vya mafunzo kwa kosa la jinai.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kigezo kilichotumika kuwafuta wapiga kura waliopoteza sifa katika Daftari ni maelekezo ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 4 ya 2018 ambayo katika kifungu cha 31 na 32 yamuelekeza Afisa Uandikishaji kufanya uchunguzi juu ya wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo katika daftari na baadae kuweka wazi orodha ya wapiga kura hao kwa muda wa siku saba katika eneo la wazi la Ofisi ya Uchaguzi ya Wilaya na hatimae kuwafuta waliopoteza sifa kwa mujibu wa sheria.

(c) Mhe. Mwenyekiti, hakuna tatizo la kulitatua juu ya suala hilo kwa vile lilifanywa na litaendelea kufanywa kwa mujibu wa sheria na naomba kumhakikishia Mhe. Mjumbe na wananchi kwa jumla kuwa hakuna haki iliyokiukwa katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Tume ya Uchaguzi wakati wa uandikishaji na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura itamuandikisha kila Mzanzibari atakaeomba kuandikishwa baada ya kutimiza sifa za kuwa Mpiga kura kwa mujibu wa sheria.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Ahsante nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.
Mhe. Waziri pamoja na majibu yako mazuri na ufanisi mkubwa uliofanywa tuna daftari la kudumu kama ilivyofanywa na sheria lakini tumeshuhudia wananchi wengi wakikosa kupiga kura na wakiwa wapiga kura ambao wametolewa katika daftari na hili daftari tunasema linaboreshwa wale waliokuwa hawajatimiza umri wanapofika kutimiza umri ndio wanaingia. Lakini tunashangaa kama wamo katika daftari la kudumu lakini wametolewa.

Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha watu hao kutolewa.

**Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Utaribu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuavayo:-

Kama nilivyosema katika jibu mama waliotolewa ni wale waliopoteza sifa au waliofariki ama hawakwenda kuhakiki wakati wa zoezi la kuhakiki. Sasa kama hukuwenda kwenye zoezi la kuhakiki *automatically* unatoka.

Lakini kifungu cha Sheria cha 32 pia kimetoa fursa kwa sababu lile daftari linawekwa kwa wazi kwa siku saba katika Afisi za Wilaya au katika eneo lolote ambalo tume itaamua. Ndani ya siku saba kama bado mtu analikwenda na hakuona jina lake wakati ana haki na sifa ilikuwa arudi tume ili jina lake liingizwe. Tunajua kabisa wako watu wengine maarufu ambao walitolewa kwa sababu walikosa kuhakiki lakini walivyokwenda walihakikiwa na baadae kurudishwa katika daftari.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kumuuliza Mhe. Waziri maswali moja lenye vifungu viwili kama ifuatavyo:-

Kama alivyonukuu Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 ibara ya 7, ibara (iid) Ibara ya pili ambayo inaeleza masharti yanayoweza kumfanya mtu asipige kura yameelezwa hapa yakiwa ni manne. Lakini la (d) linasema kukosa au kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, urai au uandikishwaji kama mpiga kura.

(a) Katika vitambulisho vilitajwa hapa cha umri, urai au uandikishwaji kama mpiga kura. Kitambulisho cha Mzanzibari ni kipi.

(b) Katiba hii hii inasema mbali na sababu zilizoelezwa ibara (iv) mbali na sababu zilizoelezwa na kifungu hichi hakuna sababu nyengine yoyote inayoweza kumzuia Mzanzibari asitumie haki yake ya kupiga kura. Katika zoezi lililofanyika katika Tume ya Uchaguzi wamesema wanahakiki na wanataka vitambulisho vilivyohakikiwa na Mamlaka ya Usajili wa Mzanzibari.

Wakati tume wanatangaza hivyo serikali haijatangaza vitambulisho vya zamani kwamba ni tabili na havitumiki tena. Lakini tume walikuwa wanawakatilia watu kuandikishwa kwa kutumia vitambulisho vya zamani huku bado vitambulisho hivyo vikiwa halali na vinatumika katika matumizi mengi.

Je, kwa nini tume walikuwa wanazuia watu wasitumie vitambulisho ambavyo havijatangazwa kwamba havitumiki tena na kuwanyima watu kukosa kujiandikisha kupiga kura.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Utaribu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba alirudie lile suala la kwanza la pili nimelipata.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Omar Said Shaaban rudia suala lako la mwanzo.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 hasa ibara ya 7 ibara (ii) ilikuwa inaelezwa Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria na kuweka masharti na kuzuia Mzanzibari asitumie haki ya kupiga kura kutokana na yoyote kwa sababu zifuatazo.

Kukosa kushindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, urai au uandikishwaji kama mpiga kura na hivi vimetumika neno (au) haijatumika neno (na) kwa sababu maana lazima viwe vyote. Kwanza kitambulisho cha Mzanzibari hapa ni kipi na kwa nini tume ilishindwa

kuandikisha wau waliotimia umri wa miaka 18 ikiwa wameonesha vyeti vya kuzaliwa. Kwa sababu katiba inasema ukionesha kitambulisho chao kinachothibitisha umri una haki ya kusajiliwa kuwa mpiga kura.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili, Sera, Utaribu na Baraza la Wawakilishi:**

(a) Mhe. Mwenyekiti, kukitizama sheria ya Tume ya Uchaguzi namba 4 ya mwaka 2018 imeeleza kwa uwazi kabisa ni vitu gani ambavyo vinatakiwa kwa Afisa Uandikishaji katika zoezi zima la kuchunguza mpiga kura halali, na kitambulisho cha Mzanzibari ni moja wa vitambulisho ambavyo vinatakiwa kwa ajili ya kuhakikiwa na Afisa wa Uchaguzi.

Kwa hivyo, kitambulisho cha Mzanzibari ni moja ya masharti ya kuweza kuingizwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

(b) *Process* ya vitambulisho ilianza mwaka 2018 ya uandikishaji na ikaendelea mpaka mwaka 2020. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika zoezi la Uboreshaji wa Daftari lilianza mwaka 2019 na liliendelea mpaka Disemba mwaka 2019 na hiyo ilikuwa kwa upande wa Pemba.

Lakini zoezi hilo lilifanyika tena kwa Unguja Januari 2020 na liliendelea mpaka Aprili. Lakini pia kulikuwepo na *room* iliyotolewa ambayo ilifanyika mwezi wa Mei 2020 hadi Juni 2020. Katika *process* yote hiyo ilikuwa inataka kuwachukuwa wale wote wenye sifa za kupiga kura wawemo katika Daftari la Kudumu.

Lakini isitoshe kama nilivyosema mwanzo daftari hili liliwekwa wazi kwa siku saba kwa mujibu wa kifungu cha 32 na liliwekwa wazi kuanzia tarehe 24 hadi tarehe 30 Juni, 2020. Sasa kama mtu hakwenda na *process* zote hizo hakika daftari litamtoa kuwemo kama ni mpiga kura mwenye sifa na hicho ndicho kilichofanyika kwa mujibu wa sheria.

Naomba sana Waheshimiwa watizame na Mhe. Omar Said Shaaban utizame sana kifungu cha 31 na 32 cha Sheria ya Tume ya Uchaguzi namba 4 ya mwaka 2018. (*Makofi*)

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** "*Bismillah Rahman Rahim*" Mhe. Spika, mimi nitaomba kumuuliza swali moja la ziada Mhe. Waziri.

Kwa kuwa Wajumbe wawili wameshatoa *query* yao ya kumlalamikia lini atakaa nao labda kuwasaidia kwenye masuala haya.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa Wajumbe hawajatoa *query* wameuliza swali.

**Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa haya mambo yaliyozungumzwa yamesapita na sasa hivi...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa naomba ukae. Tuendelee Mhe. Waziri.

**Nam. 27**

**Utunzaji wa Taarifa za Wafanyakazi**

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Kny. Mhe. Salma Mussa Bilal) –** Aliuliza:-

Moja kati ya mambo muhimu katika dhana ya utawala bora ni kuhakikisha masuala ya watumishi wa umma yanawekwa vizuri sambamba na kutunziwa mafaili na kuwekewa kumbukumbu zao ipasavyo, ili kuondoa usumbufu wakati wa kustaafu.

(a) Je, ni mara ngapi wizara imepita katika Afisi za Serikali kuhakikisha kwamba kumbukumbu zote za watumishi zinatunzwa ipasavyo.

(b) Je, ni afisi ngapi mmeshazipitia ili kujiridhisha na utunzaji wa kumbukumbu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 27 lenye Kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kupitia Maofisa wa Ukaguzi kumbukumbu kutoka Taasisi za Nyaraka na kumbukumbu Zanzibar katika kipindi cha Februari 2020 hadi Januari 2021 imefanya ukaguzi mara 16 katika ofisi mbali mbali za serikali, ili kuhakikisha kwamba kumbukumbu za aina zote zinatunzwa ipasavyo na masuala ya watumishi wa umma yanawekwa vizuri pamoja na kutoa ushauri kwa uimarishaji wa utunzaji wa kumbukumbu na uwekaji wa mafaili ya watumishi.

Taasisi ya Nyaraka na kumbukumbu tayari imezipitia taasisi na Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar 15 Unguja na Pemba kwa ajili ya kujiridhisha na utunzaji wa kumbukumbu zikiwemo Wizara tisa (9) na taasisi sita (6) za serikali kama ifuatavyo:-

- Wizara ya Fedha na Mipango (iliokuwa wakati huo);
- Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale (iliokuwa wakati huo);
- Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ;
- Ofisi ya Kamamu wa Pili wa Rais;
- Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
- Wizara ya Afya (iliokuwa wakati huo);
- OR – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora;
- Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale;
- Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

Taasisi zilizokaguliwa ni:-

- Benki ya Watu wa Zanzibar Ltd (PBZ);

- Wakala wa Serikali wa Uchapaji;
- Shirika la Bandari;
- Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii;
- Mahkama ya Ardhi – Vuga;
- Baraza la Mitihani Zanzibar.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri Sheria namba 2 ya mwaka 2011 na Kanuni yake ya Sheria namba 2 ya mwaka 2014, Mhe. Waziri ni wazi imetamka kwamba watumishi ambao wamepewa uhamisho aidha kutoka Pemba-Unguja au Unguja-Pemba ikawa wenza wao yaani waume zao wako sehemu moja uhamisho huo. Kwa kweli, sheria iko wazi kwamba watu hawa watapata kibali cha uhamisho kufuata familia yao.

Je, hadi sasa wale watu ambao wanahangaika na kusumbuka kwa ajili ya kupewa uhamisho kufuata familia zao wizara yako imejipangaje. Kama ni shida kwa nini wafanyakazi wale aidha wakaajiriwa Unguja au Pemba alimradi ikijulikana kwamba wanafamilia ambazo zinawategemea. Mhe. Waziri naomba majibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, inaelekea umelikubali swali maana yake suala hapa ni ukaguzi wa kumbukumbu za mawizara na taasisi mbali mbali sasa kama umelikubali nitalijibu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri kama unao uwezo wa kulijibu lijibu nimekupa nafasi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora:** Naweza sana kujibu, Mhe. Shaibu Hassan Kaduara swali lako linahusiana na mambo ya uhamisho wa wafanyakazi, wakati hapa tunazungumzia katika suala zima la ukaguzi wa kumbukumbu katika mawazira na taasisi za serikali.

Kimsingi ni kwamba uhamisho ni haki ya mtu wakati inapotokea dharura kama hio lakini kuna taratibu zetu vile vile za uhamisho. Kwa mfano, kumejitokeza tatizo sasa hivi tunapotangaza ajira na husema kuna ajira kwa mfano Mkoa wa Kusini Unguja, Mkoa wa Kusini Pemba Mkoa Kaskazini Pemba kwa hivyo, anayeomba nafasi hii ajaze kwa ajili ya kwenda katika eneo hilo, kinachojitokeza watu wanaomba wakishafika kule utasikia kashaolewa kama mwanamke matokeo yake sasa kinachotokea hapo ni kwamba basi anaomba uhamisho, ili amfate mume wake Unguja sasa hilo linakuwa ni tatizo kinyume na utaratibu utumishi wa mkataba tuliokuwa tumekubalina.

Kwa kweli, kwanza akafanye kazi pale angalau miaka miwili au mitatu lakini kumbe ile inakuwa ni njia ya kupatia ajira tu, halafu baadae arudi hapa hapa. Kinyume chake vile vile wengine wanaomba kwa ajili ya kufanya Unguja wanatokea Pemba baada ya kushapata anaomba kwenda Pemba. Kwa hivyo, ni utaratibu ambao kusema kweli hauko vizuri inabidi wafanyakazi waliangalie hilo lakini, hawezi kunywima mtu uhamisho kwa dharura kwa mfano, kashafanya

kazi zaidi ya miaka mitano kapata uhamisho mume wake au mke wake basi atafatana nae huko anakokwenda hakuna mapatizo yoyote na hilo linafanyika mara zote ahasante.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwakumbushe na ndio maana Mhe. Waziri akaniambia nimelikubali swali. Kwa kweli, maswali yetu ya nyongeza yatokane na swali la msingi. Kwa hivyo, ukianza swali jipya ndio maana Mhe. Waziri akaniambia ila kwa busura tu najua na upya wetu ndio maana nikaona nimuachie nafasi ili akujibu. Lakini, tujitahidi waheshimiwa maswali yetu na kama kanuni zinavyotutaka tuendane kwenye swali la msingi litoe swali la nyongeza, tunaendelea Mhe. Bihindi Hamad Khamis.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeza Mhe. Waziri kwa ufafanuzi mzuri ambao ameutoa lakini pia niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri tunajua kumbukumbu ni kitu muhimu sana je, wafanyakazi wako umewachukulia hatua wangapi waliokuwa wamepoteza kumbukumbu za wafanyakazi.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora:** Tunazo taarifa kwamba kumbukumbu kweli zinapotea hasa katika Taasisi ya Nyaraka, na serikali tayari imechukua hatua kuna wafanyakazi walihusika na upotezaji wa nyaraka zile na tuliwasimamisha kazi na wengine wamefukuzwa kazi. Hayo ni kweli yanafanyika lakini pia kuna utaratibu mwengine unatumika sasa hivi kwa watumishi wasiokuwa waaminifu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna haki ya kuuliza maswali na kupata baadhi ya taarifa, lakini kuitoa nyaraka ndani taasisi serikali ambayo iko ndani ya serikali yenyewe katika masjala unakwenda kuichukua na kuileta hadharani ni makosa na itabidi tukuulize umeipata wapi nyaraka ile.

Hayo wakati mwengine yanafanyika lakini, wafanyakazi walikuwa si waaminifu huzitoa nyaraka zile za siri wakati mwengine wanazitoa kwa watu wasiohusika kwa wale wanaohusika inakuwa hakuna matatizo kwa sababu kwa ruhusa maaalum ama ya Katibu Mkuu au Waziri inaweza ikatoka hivyo lakini yanafanyika wafanyakazi hawa ambao si waaminifu hutoa nyaraka zile za siri kwa watu wasiohusika hilo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

**Nam. 20**

**Ujenzi wa Barabara za Ndani katika Jimbo la Nungwi**

**Mhe. Abdalla Abasi Wadi** – Aliuliza:-

Wakati wa Kampeni Mhe. Mgombea Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi aliwaahidi wananchi (wapiga kura) juu ya ujenzi wa barabara za ndani. Kwa kuwa jimbo langu lina njia nyingi zilizoingia ndani ya mahoteli ya kitalii.

Je, wizara ina mpango gani wa ujenzi wa barabara hizi hasa ukizingatia utalii ndio nguzo muhimu kwa wananchi wetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wa Kampeni, Dkt. Hussein Ali Mwinyi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Chama cha Mapinduzi aliwaahidi wananchi juu ya ujenzi wa barabara za ndani. Aidha, ahadi hiyo hakuitoa tu wakati wa kampeni bali pia ameitoa wakati akilizindua Baraza lako hili tukufu mwezi Novemba, 2020.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwajuilisha Waheshimiwa Wawakilishi wote pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imejipanga kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuzijenga barabara za ndani zinazoenda sehemu za utalii na maeneo mengine muhimu ya kiuchumi na kijamii kwa kiwango cha lami kadiri hali ya uchumi itakavyoruhusu. Kwa sasa tayari tumeshazifanyia upembuzi yakinifu jumla ya kilomita 242 Unguja na Pemba.

Aidha, serikali katika hatua za awali imezidisha bajeti ya ujenzi wa barabara za ndani kutoka asilimia 15 hadi asilimia 40 ya fedha za Mfuko wa Barabara na mipango mengine ya kutafuta fedha katika vyanzo vyengine ikiwemo mikopo na ufadhili kutoka washirika wa maendeleo inaendelea.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Nakushkuru sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuidhatiti serikali ya awamu ya nane katika kuzijenga barabara za ndani. Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kama utakubaliana na mimi Mkoa wa Magharibi ni Mkoa wanaoishi watu wengi *statistically* kwa Zanzibar sasa ni mkoa pia ambao kuna barabara zote mbovu za ndani. Sasa Mhe. Rais alipokuwa katika kampeni pale Dole aliahidi kuijenga barabara ya ndani ya Makufuli Munduli je, barabara hiyo ya jimbo langu la Welezo unahisi Mhe. Waziri itaanza lini.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la kwamba lini barabara hiyo aliyoitaja itaanza ujenzi huo. Mhe. Mwenyekiti naomba nuimjibu swali hilo kama nilivyotoa katika jibu langu la msingi kwamba ujenzi wa barabara hiyo utaanza katika katika kipindi ambacho cha mwaka wa fedha wa bajeti mwaka wa fedha unaofata 2021-2022.

**Mhe. Asha Abdalla Mussa:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nilitaka kujua kwamba wamesema kwa sasa tayari wamezifanyia upembuzi yakinifu jumla ya kilomota 242 Unguja na Pemba, kwa ajili ya

kufanyia matengenezo barabara hizo tulitaka kujua tu kwamba ni barabara zipi ambazo wamefanyia upembuzi lakini pia je, zimezingatiwa maeneo hayo maalum ya ukanda wa utalii.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**Ahsate Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Barabara ambazo tumezifanyia upembuzi yakinifu ambazo ni kilomita 242 Unguja na Pemba ni barabara mbali mbali na kwa kuzianisha naomba Mhe. Mwakilishi nimletee hizi barabara kwa njia ya maandishi kujua ni ipi na ipi ambayo tumeshazifanyia upembuzi yakinifu.

**Mhe. Habibu Ali Mohamed:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ napenda nimuulize swali la nyongeza. Katika jimbo langu la Mtambwe kuna barabara ambazo zimetengenezwa kwa kiwango cha fusi barabara ya Kivumoni na Mitambuuni Kinazini na barabra hizi tayari zimeshakuwa katika hali siyo nzuri. Je, ana mpango gani katika bajeti yake kuweza kuzishughulikia barabara hizi mbili ambazo ni kero kwa wananchi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**Ahsante Mhe. Mwenyekiti,kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ningependa kumueleza Mhe. Mwakalishi kama nilivyoeleza awali katika jibu langu la msingi, kwamba serikali ina mpango wa kuzifanyia matengenezo barabara zote za ndani kwa kiwango cha lami. Barabara ambazo anazitaja ni sehemu ya barabara za ndani. Kwa hivyo, ahadi yetu kama serikali ni kwamba kadiri hali ya uchumi itakavyoruhusu barabara hizo alizozitaja na barabara nyengine zote zitafanyiwa ukarabati kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**Nam. 26**

**Utoaji wa Mikopo ya Kuwakwamua Wananchi Kiuchumi**

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman (Kny. Mhe. Salma Mussa Bilal)** – Aliuliza:-

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umekuwa ukitoa mikopo kwa vikundi na wananchi mmoja mmoja ili kuwakwamua kiuchumi.

a) Je, baada ya kutoa mikopo hiyo, mmeweza kuwarudia wakopeshwaji na kufanya tathmini ni kwa kiasi gani wananchi hao wamefaidika na mikopo hiyo.

b) Na kama mmefanya hivyo, mikopo hiyo inakwenda kwa faida au kwa hasara.

c) Ni asilimia ngapi ya mikopo imekwenda kwa faida na asilimia ngapi imekwenda kwa hasara.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 26 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida Mfuko wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi baada ya kutoa Mikopo huwa inawapitia wateja wake wote kila mwezi kupitia maafisa wake wa mikopo waliomo katika kila Wilaya. Madhumuni ya kuwapitia huko ni:-

i) Kuhakikisha fedha zilizotolewa zimetumika kwa mujibu wa mpango biashara aliouandaa mjasiriamali.

ii) Kutoa ushauri wa kibiashara na kusaidia kutatua matatizo ya mjasiriamali, na

iii) Kukusanya marejesho ya mkopo.

b) Mhe. Mwenyekiti, biashara za wajasiriamali ambao wamepatiwa mikopo huwa haziendeshwi kwa hasara kwa sababu maafisa mikopo wa mfuko wako karibu sana na wajasiriamali kuona kuwa biashara zao zinaendeshwa vizuri na bei zinazotozwa kwa bidhaa zinawiana na gharama halisi za bidhaa zinazouzwa.

c) Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 90 ya mikopo yote inaendeshwa kwa faida kwa mujibu wa sababu zilizoelezwa hapo juu.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kumuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake ya ufasaha lakini pia Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuipongeza serikali ya awamu ya saba kwa kuanzisha Mfuko huo wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na lengo kuu la mfuko huu Mhe. Mwenyekiti, ni kuweza kuwasaidia wananchi wetu ili waweze kujikwamua katika harakati za maisha.

Mhe. Waziri, hivi karibuni sote ni mashuhuda tuliona nchi yetu ilifikwa na janga la Corona na kusababisha uchumi wa nchi yetu kushuka lakini hivi sasa *Alhamudulila* tumamshukuru Mwenyezi Mungu nchi iko salama na mapato yameendelea kupanda. Je, wizara yako imejipangaje kuwasaidia wajasiriamali wale ambao waliomba mikopo kwa muda mrefu na mpaka sasa haijawafikia.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Kimsingi kwanza naomba tufahamu kwamba idadi ya mikopo inayoombwa ni mingi kuliko uwezo wa mfuko wenyewe. Kwa hivyo, serikali kwa upande wetu tumejipanga kuhakikisha kwamba tunaoungezea uwezo mfuko na tumedhamiria kuweka mambo mawili kwanza ni kuanzisha kamati maalum ambayo itakuwa inahusika na masuala ya utanuzi wa mfuko kwa kuendesha harambee mbali mbali ambazo ziztakuja kuengezea mfuko uwezo wake.

Vile vile, kwa mwaka 2019/2020 tumeweza kukusanya zaidi ya shilingi milioni 350 ambazo zimetokana na mikopo iliyotolewa katika shughuli za kilimo za mboga mboga na matunda. Kwa hivyo, tumeona kabisa kwamba sekta hiyo inao uwezo mkubwa wa kupata marejesho mengi ambayo yataweza kuongezea mfuko wetu, na tunatarajia kwamba kwa kupitia huko, basi tunaweza kuuongezea uwezo mfuko na hatimae kuwafikia wananchi wengi zaidi na kuwawezesha. (*Makofi*)

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini nimpongeze waziri kwa majibu mazuri maana anatupeleka kwamba serikali inataka kuendeshwa kwa harambeee. Lakini, nataka kumuuliza tu kwamba katika ahadi ya serikali kwenye bajeti iliyopita kulikuwa kuna Dola Milioni 20. Milioni 10 kutoka *Khalifa Fund* na 10 SMZ katika kusaidia hawa wajasiriamali, utekelezaji wake umefikia wapi na kama haupo nini kauli ya serikali kwa wajasiriamali wetu hawa.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Mhe. Mwenyekiti, suala la *Khalifa Fund* halipo katika Wizara ya Uwekezaji suala la *Khalifa Fund* liko katika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashkuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kwanza Mhe. Waziri nikupe taaifa kwamba *Khalifa Fund* inakusudiwa kwenda kwenye Mfuko wa Uwezashaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ilo ulitambue. Lakini Mhe. Waziri, amesema kwamba mfuko huu ni mdogo kutokana na mahitaji ya wanaohitaji kuomba huo mkopo wenye kwanza nikita kujua.

a) Una kiasi gani ya fedha kwa muda miaka saba sasa mfuko huu kama ni mtaji.

b) Mhe. Waziri, kuna gari aina ya *carry* kuna siku nililikuta ilikuwa imeandikwa kwamba nikiwa mkubwa nitakuwa *fuso*. Je, hawa wafanyabiashara wadogo wadogo munaowapa mkopo wa shilingi milioni mbili na nusu mpaka milioni tano katika miaka mingapi munakwenda kuwatembelea, ili kuona kwamba wameendelea vipi kimaisha na zile pesa wanazirejesha.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la kiasi gani ambacho kipo katika serikali huu ni mfuko ambao tunasema ni *revolving fund* kwa hivyo, pesa kimsingi zipo kwa wananchi wenyewe ambao

wamekopesha na kiasi ambacho kipo sasa hivi kwenye *circulation* ni zaidi bilioni 1.5. Lakini kwenye upande wa kuwapitia hawa wananchi, hawa wanachi wanapitiwa kila mwezi katika zoezi zima la kuwahakiki na kuhakikisha kwamba ile biashara yao inastawi inaendelea na vile vile kuhakiki kwamba pesa zile ambazo wamezikopa basi zinareje serikalini.

**Mhe. Salha Mohamed Mwimjuma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi na kunipa nafasi hii ya mwisho ya upendeleo kwanza kabisa na mimi niungane na wenzangu kwa kuipongeza serikali yetu kwa adhma hii ya kuweza kuanzisha mfuko huu ikiwa ni sababu au kianzilishi cha kuweza kuwasaidia wananchi wetu hasa wale wajasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tuna *experience* kuona kwamba fedha ambazo zinatolewa kwenye mfuko huu ni kiwango kidogo sana na ukizingatia wananchi wanakuwa wamejikusanya na miradi yao inakuwa ni mikubwa. Je, ni lini serikali itaona ipo haja *at list* mfuko huu kuongeza kiwango kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**Ahsante Mwenyekiti, viwango vya utowaji kwanza vinaanzia kima cha chini ni shilingi laki mbili mpaka milioni tano na hii inategemea na zaidi na *business plan* yako ambayo umekuja nayo. Kwa hivyo, maafisa wetu kabla ya kutoa hizo fedha wanahakiki kwanza uwezo wa biashara yako, malengo yako ya baadae na nini hasa ambacho umedhamiria kukifanya. Kwa hivyo, utoaji wa hizi fedha unategemea hasa na *business plan* yako ambayo unayokuja nayo. Lakini tunao mpango wa kuongeza kima kutoka wastani wa hiyo milioni tano mpaka kufikia angalau milioni 10 pale ambapo hali ya mfuko itakuwa imekaa sawa.

**Nam. 54**

**Matumizi ya Eka Kinyume na Utaratibu wa Sheria**

**Mhe. Haji Shaaban Waziri** – Aliuliza:-

Pamoja na dhamira nzuri ya serikali yetu ya kuwapatia wananchi wake maeneo ya eka kwa ajili ya matumizi ya kilimo, bado imeonekana kuna changamoto nyingi hujitokeza kwa wananchi na hatimaye eka hizo kuingizwa katika suala zima la kurithishana familia kinyume na utaratibu wa sheria.

Je, serikali haiona ipo haja ya kutoa elimu juu suala hilo ili kusaidia kupunguza migogoro ya ardhi katika maeneo ya eka.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 54 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, suala la eka tatu ni moja kati ya tunu muhimu sana za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Moja ya changamoto kubwa katika matumizi ya eka tatu ni wananchi kurithishana bila ya kufuata utaratibu uliowekwa kisheria.

Wizara kwa kuliona hili imeona kwamba ipo haja ya kutoa elimu kwa wananchi wake kuhusiana na masuala mazima ya eka kwa kupitia mikutano mbali mbali, pamoja na wadau wa sekta ya ardhi katika Wilaya na Mikoa. Pia kwa kutoa elimu kupitia vyombo vya habari ili kupunguza migogoro ya ardhi Unguja na Pemba.

Kwa hivyo, tunawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tutakapokuwa tunapita tutashirikiana na nyinyi vizuri, ili mtusaidie sana katika kutoa elimu kwa wananchi wetu. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa mujibu wa sheria za heka ambazo zipo zinaonekana kwamba ukiwacha kutoa elimu, lakini kuna sheria ambayo inabana.

Kwa mfano, mimi nimeowa mke wa mwanzo ambapo ndio nimepata eka hiyo. Mke huyo nimeza naye watoto wawili lakini kwa bahati amefariki. Nikaowa mke mwengine ambaye nimezaa naye mtoto mmoja nimemuacha. Nikamuowa mke wa tatu ambaye sikuzanaye, kwa mujibu wa sheria ya eka inasema kwamba mridhi ni mke, mke huyo atakuwa ni yule ambaye sikuzaa naye. Sasa hawa watoto wangu wa mwanzo ambao nilianza kutumikia eka hiyo, maana yake ni kwamba inawafanya eka hiyo isiwapate.

Je, kuna mpango gani wa kubadilisha sheria hiyo?

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimpongeze sana Mhe. Mjumbe kwa kuowaowa, kwa kutimiza sunna ya Mtume.

**Mhe. Mwenyekiti:** Katoa mfano tu Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Ndio ni mfano, na ni mfano mzuri na zuri huigwa. Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la sheria. Kwanza serikali ina mpango huo kwamba sheria zote ambazo tunaziona kwamba zina mapungufu tuna mpango wa kuzirekebisha. Kwa hivyo, hata na hii kama tunaona bado ina mapungufu hayo basi ni miongoni mwa sheria ambazo zitapita katika kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la uridhi wa eka. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hizo za eka niseme kwamba ataridhi mke ama watoto wa marehemu ndio ambao wataendeleza hilo shamba. Kwa hivyo, miongoni mwao na watoto pia wametajwa, kwa hivyo maana yake ni kama mke atakuwa hajazaa naye, lakini bado haimnyimi haki kwamba sio mkewe, atabaki kuwa ni mkewe, kuzaa na kutokuzaa hayo ni majaaliwa ya Mwenyezi Mungu. Lakini kama hivyo yeye ni mke, ni kizuka, ulikaa naye basi na yeye ana haki yake, lakini vile vile na watoto wanayo haki yao.

Kwa hivyo, katika msingi huo, kwa sababu watoto wa baba na mke ni mke wa marehemu ambaye amekufa. Kwa hivyo, basi wanaweza wote kwa pamoja wakawa wanatumia sehemu hiyo ya shamba, kwa sababu miongoni mwa familia ndio ambayo itakwenda kuomba katika kuendelea kulitumia. Kwa hivyo, miongoni mwao ni mwamba katika hao wote wamo. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mihayo Juma N'hunga:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza na mimi nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia nitumie fursa hii kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huko nje bado kuna kadhia kubwa sana ya migogoro ya ardhi hasa kwenye maeneo ya maeka na mashamba. Ukisoma vizuri sheria ya ardhi ile *Land Tanure Act* namba 12 ya mwaka 1992 katika kifungu cha 55, imempa mamlaka Mhe. Waziri kuamua vyenginevyo pale ambapo migogoro hii imekuwa ikikithiri.

a) Je, ni lini sasa Mhe. Waziri ataacha ule ukakasi wa kuogopa kutumia kifungu hiki namba 55 katika kufanya maamuzi, jambo ambalo litaweza kupunguza mgogoro huo.
b) Je, Mhe. Waziri anaweza kutuambia mpaka sasa, kwa sababu sheria ya eka ipo ni vyema akatuambia mpaka sasa serikali imeweka akiba ya eka ngapi kwa niaba, ili wananchi wakaweza kufahamu na ambao wanahitaji eka hizo wajitokeze kuja kuomba. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mhe. Mwakilishi wa Wananachi wa Jimbo la Mwera na hasa ukizingatia kwamba katika jimbo lake ni sehemu moja ambayo inaongoza kuwa na maeka mengi ambayo wananchi wengi wameyavamia na kubadilisha matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza serikali haina ukakasi katika matumizi ya sheria yake na vifungu vyake. Hilo namuomba radhi sana kwamba atuombe radhi kwa hilo hatuna ukakasi huo. Tunatatua migogoro kwa mujibu wa sheria zetu zilivyo  na kwa mujibu wa tatizo lilivyo vile vile, hatuwezi kwenda kukurupuka katika kusema kwamba kwa sababu hapa kuna Mhe. Mihayo na hapa kuna mwengine, basi tena tukurupuke katika kutoa hayo maamuzi. Tunatumia vifungu vya sheria kama ambavyo vinapaswa kutumiwa.

Katika swali lake la pili, ni kwamba mpaka sasa tuna akiba ngapi ya eka. Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kwamba ardhi yetu ya Zanzibar haikuwi ilivyo ndivyo ilivyo. Bahati nzuri sana baada ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar, Mhe. Rais wa Awamu ya Kwanza Marehemu Sheikh Abeid Karume aligawa eka kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, tuseme kwamba eka ziligaiwa kwa wananchi wakati huo na eka hizi zimeendelea kutumiwa na watu tofauti tofauti, kwa maana kwamba alianza kutumia warithi wamekwenda mpaka tunavyozungumza kuna baadhi ya eka zimetoka katika uwasili kwa wale watu ambao walikuwa wamerithi na kuingia katika mikono mingine kutokana na serikali kuzichukua baadhi ya eka hizo.

Kwa hivyo, kwa sasa tunavyozungumza eka ngapi ambazo zipo za akiba natamani mniletee kwa maandishi, lakini sio nyingi ambazo zipo kwa sababu eka nyingi zina watu na kuna watu wananyang'anywa eka kutokana na kukiuka yale masharti ya matumizi ya eka. Kwa hivyo, katika sehemu hiyo Mhe. Mwenyekiti, nitaomba nimjibu kwa maandishi, ahsante sana.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza naomba nimwambie Mhe. Waziri tu kwamba, atujibu asitusute, maana inakwenda kama anatusuta suta kidogo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, migogoro ya ardhi katika maeneo yote ya Zanzibar baadhi yao husababishwa na Masheha, tukitaka tusitake huo ndio ukweli, kwa sababu kuna Masheha wengine hujifanya madalali katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri migogoro hii ya ardhi huoni kwamba ipo haja sasa kuanzisha Mabaraza ya Shehia ya Ardhi ambayo yatatatua migogoro hiyo ya ardhi kule katika shehia, ili kuondokana na migogoro hiyo ya ardhi ya kila siku.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda sana kumshukuru Mhe. Suleiman Makame Ali wa Jimbo la Ziwani. Mhe. Mwenyekiti, sijamshushua mtu, inawezekana umeona labda nimesema kwa *speed*, basi kama nimesema kwa *speed* sana naomba radhi kwa hilo, nilikuwa nimekolea katika kuzungumza.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kuna migogoro mingi ya ardhi, siwezi kusema moja kwa moja kwamba yote inasababishwa na masheha, lakini masheha nao ni binadamu na binadamu tuna tabia tofauti tofauti. Kwa hivyo, inawezekana wapo miongoni mwetu kwamba tuna kiuka taratibu, inawezekana nasema. Kwa hivyo, sitaki kusema kwamba Masheha wanafanya hivyo, lakini inawezekana kwa sababu na wao ni binadamu kama binadamu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala ambalo amelizungumza kwamba la kuanzisha Mabaraza ya Shehia katika kutatua migogoro. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunapokwenda kutatua migogoro tunashirikiana sana na Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Kwa hivyo, katika hili maana yake ni kwamba tunawashirikisha sana na Masheha.

Kwa hivyo, suala la kuanzishwa Mabaraza ya kutatua migogoro, ni kwamba mwelekeo ni kuwa tutatuwe migogoro hata katika ngazi za sheha, na ndio maana Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya wakati wanaapishwa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa kila mmoja tunaambiwa kwamba tutatuwe changamoto za migogoro ya ardhi katika maeneo yetu. Kwa hivyo, kupitia hayo Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwamba yote yatakuwa yanafanyika katika msingi kama huo. Lakini wazo lako ni jema sana na tunalipokea. Tunakushukuru sana Mhe. Mwakilishi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri. Katibu kwa wizara inayofuata.

**Nam. 4**

**Upungufu wa Walimu Katika Skuli ya Dodo**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha (Kny. Mhe. Bahati Khamis Kombo)** – Aliuliza:-

Kumekuwa na upungufu mkubwa wa walimu katika skuli ya Dodo Shehia ya Dodo Jimbo la Chambani, ambapo kuna walimu kumi na moja (11) tu na skuli ikiwa na wanafunzi 1,170 ambao hulazimika darasa kuwa na wanafunzi kati ya 86 mpaka 88 na maandalizi 139.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna utaratibu gani wa kuwasaidia walimu hawa angalau waweze kusomesha kwa ufanisi zaidi.

(b) Je, Darasa kuwa na wingi huu wa wanafunzi inakubalika.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi** (**Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) -** Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, Skuli ya Msingi ya Dodo ipo chini ya usimamizi wa Baraza la Mji Mkoani. Hii ni baada ya sheria ya ugatuzi kuanza kazi ambapo elimu ya Msingi inasimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ, badala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama ilivyokuwa huko nyuma. Hata hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kuwa msimamizi mkuu wa upatikanaji wa elimu iliyobora kwa watoto wetu katika ngazi zote, ili kuhakikisha wanajengewa misingi imara ya kuwafanya waendelee na ngazi mbali mbali za masomo baada ya elimu ya msingi, na hivyo nchi yetu kuwa na wataalamu wa kuiletea maendeleo nchi yetu.

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Skuli ya Dodo ina upungufu mkubwa wa walimu kama zilivyo baadhi ya skuli nyingine katika Wilaya ya Mkoani na wilaya nyinginezo. Hata hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ tayari imepanga kupeleka walimu wawili kwa mwaka huu wa 2021, kama ambavyo imefanya katika Skuli za Msingi za Pujini na Chambani, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu katika skuli hiyo. Walimu hawa wa muda watakaopelekwa ni kutoka skuli za Sekondari za jirani ambao wanasomesha chini ya vipindi 27 kutoka katika skuli zao na hivyo watapelekwa hapo kwa muda kusomesha na kufikisha vipindi 27 vinavyopaswa mwalimu kusomesha kwa wiki.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hali ya wingi wa watoto darasani, kwa mfano wa skuli katika jimbo la Chambani ni mkubwa kulinganisha na viwango vya wizara vya wanafunzi 25 kwa darasa kwa ngazi ya elimu ya Maandalizi, wanafunzi 45 kwa darasa kwa ngazi ya elimu ya Msingi na wanafunzi 40 kwa darasa kwa ngazi ya elimu ya Sekondari. Wingi wa wanafunzi darasani ni miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili Sekta ya Elimu katika nchi yetu.

Serikali yetu tukufu ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na jitihada mbali mbali kwa kushirikiana na jamii, pamoja na wadau wengine mbali mbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi katika kuimarisha miundombinu ya elimu, hasa ujenzi wa skuli, madarasa na

skuli za kisasa kabisa, ili kupunguza wingi wa watoto madarasani. Hata hivyo, kasi ya ongezeko la watu ni kubwa kulinganisha na kasi ya kuimarisha miundombinu ya elimu. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya njema. Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba kuna baadhi ya skuli zina idadi kubwa ya wingi wa walimu hadi kufikia kiwango mwalimu ana vipindi 20 mpaka 30, kinyume chake baadhi ya skuli zina upungufu mkubwa wa walimu hadi mwalimu kufikia vipindi 40 mpaka 50 na baadhi ya masomo yakawa hayafundishwi kabisa.

a) Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwamba Je, wizara yake ina mpango gani wa kuweka uwiano mzuri ili kulinganisha idadi ya wanafunzi na idadi ya walimu kulinganisha na skuli nyengine.

b) Je, wizara imejipanga vipi ili kuondosha upungufu wa walimu ambapo ni tatizo sugu katika jamii zetu hadi sasa na kwa vile Mhe. Rais ana kazi kubwa ya kuboresha elimu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi** (**Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Napenda kumshukuru sana mwalimu Mhe. Zawadi Amour kwa swali lake. Najua ni mwalimu na mwalimu ni mwalimu tu ataendelea kusomesha, hongera sana Mhe. Zawadi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alichokizungumza Mhe. Mwakilishi ni kwamba kuna baadhi ya skuli zina walimu wengi ukilinganisha na skuli nyengine. Katika kuliona hili ni kwamba tayari serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tunafanya mpango wa kufanya *reallocation* ya walimu katika kuona kwamba kwenye wilaya kwa mfano, kupanga walimu wake katika kila skuli ili kupata idadi yake vizuri, kwa sababu kuna walimu wengine unakuta wamo masomoni, lakini inapokuja ile orodha ya walimu anakuwa anaoneshwa kwamba na yeye ni miongoni mwa walimu ambaye yupo katika kuendelea na kazi, lakini kiuhalisia anakuwa hayupo yupo kwenye masomo na baadhi ya wengine wako katika likizo mbali mbali, hasa zile zinazotolewa za akina mama.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika hali kama hiyo unaweza kukuta idadi ya skuli ukaambiwa kwamba ina walimu wengi, lakini ukienda katika hali halisi hawapo wapo katika masomo. Kwa hivyo, wizara ina mpango wa kufanya *reallocation* ya walimu wake, ili kuona kwamba kama kuna skuli katika wilaya ambazo zimezidi walimu ni kuwapunguza na kuwapeleka katika skuli nyengine, lakini vile vile katika ngazi ya mkoa na taifa kwa ujumla wake.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la kuondosha upungufu wa walimu ni kwamba serikali yetu inakuwa inaajiri walimu katika kila awamu. Katika bajeti ya mwaka 2021 basi pia mpango wa kuajiri walimu nao ulikuwa upo, lakini yote inategemea na hali ya fedha, kwa sababu huwezi kumuajiri mwalimu bila ya kuwa na fedha ya kumlipa mshahara. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hili nalo linaendelea kuzingatiwa vizuri katika kuajiri walimu, ili kupunguza uhaba wa walimu na inapotokezea katika wilaya maalumu kuna upungufu mkubwa wa walimu, basi serikali inakuwa inaweka umakini mkubwa na kipaumbele katika kuajiri ajira maalum kwa skuli hizo tu,

ili kuondokana na upungufu huo wa walimu ambao amezungumza Mhe. Mwakilishi. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri tatizo la wanafunzi kuwa wengi katika madarasa linapelekea hali ya kuwafanya wanafunzi kusoma mpaka chini ya miti na tatizo hilo lipo katika Skuli ya Mbuzini.

Je, serikali ina mpango gani wa kuweza kujenga mabanda ambayo tayari wazazi wameshatia nguvu zao. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi** (**Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Napenda sana kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa swali lake zuri.

Mhe. Mwenyekiti, alichokizungumza Mhe. Mjumbe ni kweli kwamba kuna baadhi ya skuli zina uhaba wa madarasa sio zote, na skuli aliyoitaja hapa ni Skuli ya Mbuzini ambayo iko chini ya Halmashauri, kwa maana kwamba imo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mhe. Waziri tayari amelisikia na amenitikisia kichwa kwamba hilo amelipokea na atalizingatia. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Sulubu Kidongo Amour:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakupongeza Mhe. Waziri amejibu maswali yote vizuri na kwa sauti nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya Jimbo langu la Mkwajuni kila siku asubuhi napata tatizo, kuna walimu wengi ambao bado hawajaajiriwa na wanajitolea.

Je, walimu hawa wataajiriwa lini. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi** (**Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Napenda sana kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, suala la walimu wa kujitolea ni kwamba serikali ilikuwa tayari imeshapanga mpango wa kuweza kuwaajiri walimu hawa, tokea serikali ya awamu iliyopita na katika awamu ya sasa ambayo inaendelea najua kwamba mpango huo bado unaendelea. Lakini kwa walimu ambao walikuwa wanajitolea, walimu wengi walikuwa katika ngazi zaidi ya msingi na maandalizi, walimu wa sekondari hawakuwa wengi sana, kwa sababu baadhi ya walimu wengi waliokuwa wanajitolea wameajiriwa na katika Jimbo lake la Mkwajuni nimwambie tu kwamba wako walimu ambao tuliwaajiri, kama Jimbo la Chaani vile vile walikuwepo walimu ambao tumewaajiri na majimbo mengine tumewaajiri wale walimu ambao walikuwa wakijitolea.

Kwa hivyo, ni kwamba ule mpango wa kuwamalizia wale ambao tayari walikuwa wapo orodha yao tayari ipo kwenye serikali, wizara ya utumishi wanayo hiyo orodha na mambo yakishakuwa

mazuri basi na mpango huo nao utakamilika na wale walimu nao wataweza kuajiriwa. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini na mimi nina swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alizungumza kwamba kweli kuna matatizo ya walimu kwa baadhi ya skuli, skuli nyengine kuna wengi na skuli nyengine wapo kidogo. Nalizungumzia kwamba wanaangalia uwiano ukizingatia kwamba kwenye wilaya wana walimu wengi wapunguzwe na kupelekwa baadhi ya skuli.

Mhe. Mwenyekiti, katika Skuli ya Makoba ina walimu wawili tu wa hesabati na katika walimu hao mwalimu mmoja ana vipindi karibu 40 au kupindukia 40. Mwalimu wa pili ana nusu siku, kwa sababu yupo pale siku mbili na siku mbili yupo Kiongwe. Lakini kwa kuzingatia kwamba tunahitaji wanafunzi wetu wapate kusoma, baada ya kuongeza walimu kwamba pana upungufu baadala yake kaondoshwa mwalimu mmoja yule wa hesabati ambaye mwenye vipindi zaidi ya 40 kaplekwa uhamisho skuli nyengine ambapo skuli aliyopelekwa haina mahitaji ya mwalimu wa hesabati.

Kwa hivyo, naomba kuuliza je ni lini tutaletewa mwali mwengine wa hesabati ndani ya Skuli ya Makoba, ili kukidhi haja hiyo, ukizingatia wanaliopasi Kiongwe sasa hivi wote tayari wameelekea Makoba madarasa yataongezeka. Kwa hiyo, ni lini tutarudishiwa yule mwalimu wa hesabati pale Skuli ya Makoba. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana na naendelea kumshukuru sana Mhe. Mwakilishi mwalimu na yeye Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba nimelipokea swali lake na nitaenda kulifuatilia ili kuona kama huyu mwalimu aliyehamishwa na huko alikokwenda kama hakuna uhitaji huo basi tutamrudisha katika skuli ambayo ametoka.

Lakini naomba nikiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba tuna uhaba mkubwa sana wa walimu wa hesabati. Kutokana na hali hiyo naomba nitoe wito kwa jamii kupitia kwetu sisi basi tuendelee kuwashawishi vijana wetu wasome sana masomo haya ya sayansi hasa hasa hesabati na fizikia, kwa sababu hilo ndio tatizo kubwa ambalo limetukabili ndani ya nchi yetu. Kwa kweli, naamini tukiwashajihisha vijana wetu wakasoma masomo hayo, basi tatizo hilo ambalo tunalizungumza litapata ufumbuzi.

Vile vile, kama wapo vijana ambao wamesomea masomo ya hesabati ambao hawajaajiriwa, basi naomba sana tuwasiliane na Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, ili tuweze kuwapatia ajira vijana hawa walimu wa hesabati na fizikia, kwa ajili ya kuweza kupunguza tatizo hilo la uhaba wa walimu wa hesabati. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

**Nam. 12**

**Kuimarishwa kwa Huduma za Dakhalia**

**Mhe. Mussa Foum Mussa** – Aliuliza:-

Miongoni mwa malengo ya Bajeti ya mwaka 2020/2021 ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kuimarisha huduma za Dakhalia kwa kuzipatia usafiri na chakula kwa wanafunzi.

(a) Je, lengo hilo limefanikiwa kiasi gani hadi sasa.

(b) Je, Dakhalia ngapi zimepatiwa usafiri.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilisi swali lake Nam. 12 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba miongoni mwa malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni kuimarisha huduma za dakhalia kwa kuzipatia huduma za usafiri na chakula. Katika kulifikia lengo hilo Wizara kwa sasa inapeleka huduma za chakula kila mwezi katika dakhalia zote saba zinazotumika. Dakhalia hizo ni CCK Mazizini ya Unguja, Mohd Juma Pindua, CCK Kiuyu ya Pemba, Fidel Castro, Kengeja Ufundi, Utaani na Chasasa.

(b) Kwa mwaka huu wizara haijanunua usafiri wowote kwa huduma za dakhalia kutokana na upungufu wa fedha. Hata hivyo, wizara ilinunua basi moja katika bajeti ya mwaka uliopita kwa dakhalia ya Mazizini ambalo linasaidia sana watoto wote wanaokaa dakhalia hiyo. Watoto wanaokaa dakhalia ya Mazizini ambao wananufaika na usafiri huo ni wale wanaotoka sehemu za mbali mbali zikiwemo wale ambao wanatoka Skuli za Pemba ambao wanakuja kusoma Unguja na wanaishi katika dakhalia ya Mazizini. Lakini vile vile wale ambao wanaosoma katika skuli za michipuo za Lumumba, Kiponda, Ufundi Mikunguni pamoja na Skuli ya Biashara Mombasa ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mussa Foum Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa amekiri katika malengo ya mwaka huu bado hawajanunua usafiri na kwa kuwa katika baadhi ya dakhalia kwa mfano kama dakhalia ya Skuli ya Mohd Juma Pindua haina usafiri wa aina yoyote. Je, Mhe. Waziri kuna mpango gani wa dharura juu suala hili kupeleka usafiri wa dharura pale katika Skuli ya Mohd Juma Pindua, ili ikitokea dharura yoyote wakati wa usiku watu waone kwamba inatatuliwa kwa haraka. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushuru kwa kuendelea kunipa nafasi na napenda nimshukuru sana Mhe. Mussa Foum Mussa kwa swali lake nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza katika swali letu mama ni kwamba hatujanunua basi sio kama tulitaka ni mpango wa matumizi tulipanga tununue lakini mpaka sasa hali ya fedha haiku vizuri na sisi mashahidi tunaelewa kwamba ambacho kilitokezea ni kwamba kutokana na janga ambalo lilitokea katika dunia limeathiri hata hali ya uchumi wetu wa Zanzibar. Kwa hiyo, kutokana na hilo ambalo limepelekea kwamba kutokununua kwa basi hilo lakini pale ambapo tutatokezewa na dharura Mhe. Mwenyekiti ni kwamba bahati nzuri hiyo skuli ilipo kuna viongozi tuna Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya vile vile tunashirikiana nao vizuri katika kuona kwamba tunapotokewa na tatizo basi tunalitatua kwa haraka haraka.

Pia lolote litakalotokezea Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba basi tutashirikiana na viongozi wenzetu hawa kuona kwamba tunapatia ufumbuzi wanafunzi wetu. Lakini kwa sasa sitaki kuja kumwambia kwamba kesho tunakwenda kupeleka basi hali ambayo itakuwa sikusema sahihi.

Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi naomba tufanye stahamala kwamba hali yetu itakapo ruhusu tutanunua kama ambavyo tuliahidi, lakini kutokana na hali ya fedha kwa sasa hali haijaweza kuturuhusu nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa yeye anakutambua sana Micheweni na jiografia ya Micheweni hali halisi ilivyo na kumekuwa kilio cha muda mrefu kuhusiana na masuala mazima ya usafiri, sisi kule Chuoni hatuhitaji lazima tupate basi lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri ni lini hasa katika mpango huo pindipo tukifanikiwa ataweza kuweka kipau mbele kwa Micheweni kuweza kulitekeleza hilo kama ambavyo mahitajio ya muda mrefu yameshalalamikiwa na uongozi wa chuoni.

Lakini vile vile, jengine Mhe. nilitaka kujua ni vigezo gani ambavyo vimetumika badala ya kupeleka usafiri kwanza Kiuyu na badala yake akaanza kupeleka hapa Mjini wakati tunaona kwamba kuna huduma nyingi za usafiri.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni Jimbo la Dhahabu naona linafanana na Jimbo la Chumbuni,

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tatizo la usafiri kama ambavyo tulizungumza lipo katika dakhalia zote si Micheweni peke yake na mpaka ukifanikiwa tutaweka kipaumbele pale ambapo tunaona kwa sababu zote ni muhimu. Kwa hiyo, kusema kwamba tutampa kipaumbele Micheweni bila ya kumuacha Pindua au nitapeleka Utaani ama Chasasa. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tuombe tupate hizo fedha tununue usafiri tuwapelekea wananfunzi wetu, wote ni muhimu sana kwetu sisi viongozi na serikali kwa ujumla wake.

Kuhusu kigezo kilichotumika. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wanafunzi wa dakhalia Mazizini wanasema kwamba watu wanaokaa pale labda wanasema nui Mjini, lakini wanaokaa pale wahasomi Mazizini wanasoma katika skuli mbali mbali na bahati mbaya sana, ambao wanakuwepo pale ni wanafunzi kutoka maeneo tofauti na skuli tofauti. Watoto hawa ambao wanakaa pale wanatoka mashamba lakini hata ambao wanatoka Pemba wapo na hali za uchumi

kama tunavyozielewa kwamba hata ule usafiri mtoto kwenda skuli na kurudi basi pia inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, baada ya kupatikana basi ikaonekena ipelekwe pale, ili kuwasaidia wanafunzi walio wengi na hasa hasa wengi wao wakiwa ni wanawake. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya upendeleo naomba nimuulize Mhe. Waziri swali ndogo la nyongeza.

Mhe. Waziri najua Chuo cha Kiislamu Micheweni kimeasisiwa mwaka 2001 na mwaka huo ilikuwepo gari kubwa sana ambayo ilikuwa inatumika kwa wanafunzi kwa shughuli zao za kuendea maeneo mbali mbali. Je, Mhe. Waziri ile gari iliyokuwepo pale imeuzwa na kama imeuzwa fedha hizo zimepelekwa wapi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi (Kny. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naendelea kukushukuru na napenda sana nimshukuru Mhe. Mwakilishi kwa swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba hakuna wizara yoyote ambayo ina mamlaka ya kuuza mali ya serikali isipokuwa Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo ambayo ina mamlaka ya kufanya mauzaji ya mali za serikali. Kwa kweli, kama ambavyo alizungumza tokea mwaka 2001 maana gari hii ilikuwa tayari imeharibika halikuuzwa na pesa yake haikupelekwa pahala pengine, gari ilitumika na baada ya muda ulipofika maana yake gari hiyo kwamba imeshindwa kutengenea.

Kwa hiyo kilichofanyika kama kuna *spare* nyengine zilionekana kama zinafaa, basi zilikuwa zikiingizwa kwenye gari nyengine kwa kuendelea kunusuru gari hiyo nyengine, lakini gari kama gari yenyewe maana yake ni kwamba iliharibika kutokana na kwamba ilitumika kwa muda mrefu na ilifanya kazi nyingi. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Nam. 50**

**Kuharibika kwa Njia "*Eazypesa*" kwa Ajili ya Manunuzi ya Umeme**

**Mhe. Sabiha Filfil Thani** - Aliuliza:-

Hivi karibuni kulikuwa na matatizo ya mtandao wa simu "*EazyPesa*" iliyopelekea huduma za umeme zinazolipwa kwa njia ya mtandao kukosekana na vituo vya kulipia kwa kawaida ni kidogo sana.

Je, Shirika la Umeme (*ZECO*) halioni ipo haja ya kuweka vituo vyengine hata vya dharura iwapo tatizo litajirudia.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nikiri kwamba kumewahi kutokea matatizo mbali mbali kwenye mitandao ya simu ya *EazyPesa* ambayo ilikuwa ikipelekea huduma za umeme zinazolipwa kwa njia ya mtandao kukosekana na hivyo kupelekea usumbufu kwa baadhi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa, Shirika la Umeme linaendelea na mpango wa kutanua wigo wa kuongeza mitandao mingine ya simu (*HaloPesa, Tigopesa* na *AirtelMoney*) pamoja na Mawakala wa *CRDB Bank* ambao watatoa huduma hizo hadi mitaani, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba huo, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme haioni sababu ya kuongeza vituo vya kuuzia umeme zaidi ya vilivyokuwepo, kwa vile huduma hiyo ya kuuza umeme inaweza kupatikana kwa kutumia mitandao amabayo nimeieleza.

**Mhe. Sabiha Filfil Thani:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuru aliyoyajibu naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Je, hii huduma utekelezaji wake utaanza lini ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, hatua za mazungumzo na mitandao ambayo nimeitaja zinaendelea na mapema mwaka wa fedha 2021/2022 tutaanza utaekelezaji wa shughuli hii.

**Nam. 14**

**Usumbufu wa Mashimo Makubwa katika Barabara ya Mfenesini hadi Mwera**

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara (Kny.Mhe. Machano Othman Said): –** Aliuliza:-

Napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika juhudi zake za ujenzi wa miundombinu hasa ya barabara. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi, wananchi wa maeneo ya Kitundu hadi Mkanyageni wamekuwa wakipata usumbufu na ajali kutokana na mashimo makubwa katika barabara ya Mfenesini hadi Mwera katika eneo la Kitundu/Mkanyageni.

Ni lini serikali itaifanyia matengenezo makubwa barabara hiyo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara imekuwa ikizifanyia matengenezo ya kuziba mashimo barabara mbali mbali zilizojengwa kwa lami Unguja na Pemba ikiwemo barabara ya Mfenesini hadi Mwera, kazi ya uzibaji wa mashimo kwenye barabara hizo ni kazi endelevu. Aidha, serikali inaendelea kutafuta fedha za kuzifanyia matengenezo barabara kubwa ikiwemo barabara ya Mwera hadi Mfenesini ahsante Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana  Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Waziri barabara ya Chake – Tundaua ni miongoni mwa barabara hizo hizo ambazo zinatatizo kama hili je kupitia Misooni Jimbo la Chake Chake. Je, Mhe. Wizara yako ina mpango gani kwenye barabara kama hiyo ambayo ina tatizo kama hilo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Mwenyekiti, naona hii barabara imekwenda *specific* na kanuni ya Nam. 41 inasema uende kwenye swali mama naona kaenda kwenye barabara ya Chake na tunazungumzia barabara ya Mfenesini –Mwera.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri kuhusiana na swali la barabara na linafanana na swali mama kwa hiyo nahisi tunaweza tukamjibu.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, niseme tu katika swali lake linajirudia katika jawabu langu la mwanzo kwa sababu tumesema serikali inaendelea kuzifanyia matengenezo barabara zote Unguja na Pemba. Kwa hivyo, jibu litakuwa ni lile lile.

**Mhe. Anna Athanas Paul:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kuniona na mimi napenda kumuuliza swali la nyongeza Mhe.Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa kweli, arabara hizi zimekuwa kila mara zinafanyiwa matengenezo haya mashimo yapo katika barabara, lakini mvua zikinyesha mashimo yanarudi vile vile tena sehemu zile zile. Sasa nataka kujua huu uzibaji wao wa mashimo unakuwa hauzingatii viwango ama vipi. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Anna Athanas Paul swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli hata sisi tumebaini kwamba barabara zikizibwa mara kwa mara zinakuwa zinakuwa zinarudia vile vile. Lakini kwa sasa tumewasiliana na wenzetu wa *TANROAD*  tayari tumepata utaalamu wa kutumia lami kavu ambayo tuna imani kwamba  barabara zikitumiwa kwa lami kavu zinaendelea kuwa imara. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti wewe mwenyewe ni shahidi katika daraja la Pondeani kuna siku ulikwama ulikuwa unarudi kwenye kamati unataka kwenda Wesha. Mhe. Waziri daraja la Pondeani tunasubiri ile kusema Mungu amepanga ikinyesha mvua daraja lile pale Pondeani halipitiki. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha daraja lile analiboresha, ili kuondosha usumbufu ule kwa wananchi wanaokwenda maeneo ya Wesha na maeneo ya Chake Chake hata Mwenyekiti mwenyewe wa Baraza kuna siku alikunja nguo mpaka kwenye mafutini. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tumebaini madaraja mengi yana matatizo na hivi sasa tumetuma timu za wataalamu ambazo zitakuwa zinapitia madaraja yote na kuifanyia upembuzi zaidi, ili tuyafanyie marekebisho likiwemo daraja la hilo ambalo amelitaja. Ahsante Mhe. Mweneyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa taratibu maswali yameisha sasa na maswali ya nyongeza ni mawili na tayari tumemaliza na bado mnaendelea kusimama ili mupate muulize. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe sana tuzingatie hilo, tuzingatie kufuata taratibu zetu kwa sababu mnanipa mtihani na mnakuwa mnajua kama tayari sasa hivi wakati umeshakwisha Mhe. Waziri naomba uendelee.

**Nam. 3**

**Ahadi ya Uchimbaji wa Kisima cha Kumwagilia Shamba la Kimbuni**

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha (Kny. Mhe. Bahati Khamis Kombo) –** Aliuliza:-

Wananchi wa Kimbuni walitembelewa na Mhe. Rais katika mashamba ya Kimbuni na kupewa ahadi ya kuchimbiwa kisima cha umwagiliaji, lakini mpaka leo bado ahadi hii haijatekelezwa na muda umekuwa mrefu sana.

(a) Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa.

(b) Je, ni lini utakwenda kuwatembelea wananchi hawa wa kilimo cha umwagiliaji na kujua changamoto zao.

**Mhe. Waziri Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla sijajibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia nikiwa katika hali ya uzima mbele ya Baraza lako tukufu. Vile vile, nimpongeze Dkt. Hussein Ali Mwinyi kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kura nyingi. Pia, nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kunichagua kuwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. Kwa namna ya pekee niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Paje kwa kunichagua mimi kuwa Mwakilishi wao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 3 lenye (a) na (b) naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Bahati Khamis Kombo kwa jitihada zake anazozichukua katika kufuatilia na kuendeleza kilimo hususan katika umwagiliaji maji. Aidha, nakubaliana nae kwamba Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein alivyotembea maeneo ya kilimo ikiwemo bonde la Kimbuni, liliopo katika Wilaya ya Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa ziara hiyo ambayo aliifanya katika kipindi chake cha mwanzo cha uongozi alitoa ahadi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji ikiwemo na pamoja na uchimbaji wa kisima.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inakiri kwamba kazi hii imechukua muda mrefu bila ya kutekelezwa. Hata hivyo, wizara yangu bado inatambua deni na kutekeleza ahadi hiyo muhimu sambamba na dhamira pana ya kuendeleza mabonde yote yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji, ikiwemo bonde la Kimbuni, kama nilivyoelekezwa kwenye Mpango Mkubwa wa Umwagiliaji Maji wa Mwaka 2003.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza dhamira pana ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji, wizara yangu imefanikiwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde tisa ya kilimo na hivi sasa inaendelea na ujenzi wa mabonde saba mengine.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba kazi ya ujenzi wa miundombinu wa umwagiliaji maji kuwa na gharama kubwa serikali inaendelea kujenga miundombinu bora ya kilimo hicho hatua kwa hatua, kadri inavyopata uwezo wa kufanya hivyo kwa kutengeneza Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na wakulima wa bonde la Kimbuni waendelee kuwa na subira huku wizara yetu ikiwa inafanya juhudi ya kutafuta fedha, kwa ajili ya kuendeleza mabonde mengine ya kilimo ikiwemo Kimbuni.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kuwatembelea wakulima wa bonde la Kimbuni, tayari nimeshafanya ziara maalum kwa bonde hilo na mabonde mengine ya kilimo ya Unguja na Pemba kuzungumza na wakulima. Aidha, wakati wa ziara yangu katika bonde la Kimbuni nilipata fursa ya kuzungumza na wakulima wa bonde hilo na kujua changamoto zao na mafanikio yao katika uendelezaji wa kilimo hicho cha umwagiliaji. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

**Mhe. Mohamed Mgaza Jecha**: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na sahihi. Kwa kweli, napenda kumuuliza swali moja tu, wakati amekiri kwamba ni muda mrefu, sisi wengine sio waimbaji wa nyimbo za taarab, lakini nataka nimuulize tu, tusubiri mpaka lini. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mhe. Mohamed Mgaza Jecha, alilouliza kuwa mpaka lini atafanikiwa. Kama nilivyosema katika maelezo yangu, tunafahamu kuwa umwagiliaji una gharama kubwa na nimesema kwamba muwe na subra huku wizara ikiwa inafanya juhudi ya kutafuta fedha, kwa ajili ya kuendeleza mabonde hayo mengine ya kilimo ambayo ikiwemo hilo Kimbuni. Kwa hivyo, naomba tuwe na subra tutakeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Aza Januar Joseph:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwamba suala la umwagiliaji ni muhimu sana kwa wananchi hawa wa Kimbuni na muda mrefu wamechukua kwa kusubiri, kwa miaka kumi kwa kweli wamefanya subra ya hali ya juu.

Naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo atachukua kipaumbele gani kuwasaidia wananchi hawa ambao ndani ya miaka hii kumi wamekuwa na tamaa ya kuona kwamba kesho tutamwagilia na mpaka leo kutokupata matunda yoyote. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru sana Mhe. Aza Januar Joseph. Kwa hivyo, naomba niseme kwamba nilipotembelea Kimbuni, tuliweka mikakati ya wakulima hao kuona kwamba wanaanza na umwagiliaji maji, kwa sababu tayari wameshaanza kuwa na mifumo midogo midogo ya umwagiliaji na tumekubaliana kwamba hali itakaporuhusu tu tutaanza na ujenzi wa bwawa kwa ajili kumwagilia maji katika maeneo hayo. Ahsante. Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa nafasi ya kumuliza Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa majibu yake fasaha kwa kina na yenye kufahamika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Waziri alisema wizara yake imefanikiwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde tisa ya kilimo na mengine saba. Mimi nataka kuyafahamu tu haya mabonde tisa ambayo walifanikiwa pamoja na hayo saba ambayo ameyaeleza mwenyewe kwamba tayari na hayo amefanikiwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo majibu.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:** Ahsante sana Mhe. mwenyekiti, naomba kumjibu swali lake Mhe. Shadya Mohamed Suleiman kama ifuatavyo. Katika mabonde saba ambayo tayari tumeanzia kwa upande wa Unguja ni Cheju, Kibokwa, Kinyasini, Kilombero, na kwa upande wa Pemba ni Makwararani na Mlemele hayo ndio katika mabonde saba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mabonde kumi ambayo tumeanzia katika umwagiliaji kwa Unguja na Pemba, mabonde yenyewe ni haya yafuatayo; Mtwango, Kibondemzungu, Koani, Mchangani, Dobi, Machimbini- Ole na Kwalemporona. Hayo ndio mabonde kumi ambayo tumeshayaanzisha katika umwagiliaji maji. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali na majibu umemalizika lakini kabla ya kuendelea na suala jengine naomba niwatangazie wajumbe wote waliojaza fomu za maombi wa Baraza Kuu Taifa UWT wanatakiwa warejeshe fomu hizo leo kabla ya saa nane na akabidhiwe Mnadhimu wa Wawakilishi wa CCM.

Tangazo jengine. Kuna Waheshimiwa ambao wameteuliwa waende kumpa pole mwenzetu Mhe. Salma Mussa Bilali ambae amefiwa jana na mama yake mzazi nao ni Mhe. Harusi Said Suleiman, Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe.

Mohamed Mgaza Jecha. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa hao watuwakilishe kwa kwenda kumpa pole mwenzetu aliyefiwa na mama yake jana.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi wa Wawakilishi Iliyotolewa Tarehe 11 Novemba, 2020 na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema ya uzima, lakini pia kutuwezesha kukutana leo hii katika Baraza hili tukufu. Lakini namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuiweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wetu Dkt. Hussein Ali Mwinyi, nampongeza kwa dhati kabisa kwa jitihada zake, weledi na umakini mkubwa katika kuiongoza nchi yetu. Sote ni mashahidi kwamba katika kipindi kifupi sana Mhe. Rais, amedhihirisha kwa dhati kabisa nia yake ya kuleta Mapinduzi ya Kiuchumi katika nchi yetu. (*Makofi*)

Katika kipindi kifupi na kama ilivyodhihirishwa katika Hotuba yake ya siku 100 ya uongozi wake, ameonesha kwa vitendo, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Lakini pia, ameonesha kwa vitendo utekelezaji wa ahadi zake alizozitoa wakati wa kampeni lakini na zile alizokuwa akizitoa katika hotuba zake sehemu mbali mbali. Ameweza kuongeza mapato katika vyanzo vikuu vya mapato hasa pale bandarini.

Lakini pia, juhudi kubwa sana za kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hayo. Vile vile, Mhe. Rais katika kipindi kifupi kabisa ameweza kurudisha nidhamu katika utumishi wa umma na ameonesha ushupavu mkubwa sana wa kupambambana na vitendo viovu vya rushwa, ubadhirifu na wizi wa mali za umma.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais katika kipindi kifupi sana amevutia wawekezaji wengi walioweza kufika katika nchi yetu wenye nia ya kuwekekeza na kushirikiana na serikali katika kuiendeleza nchi yetu. *Signing* zilizofanyika hivi karibuni za hati za makubaliano *MOU* kwa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri na Mangapwani ni sehemu ya jitihada hizo.

Sambamba na hilo, Mhe. Rais wetu kama sote tunavyojua jinsi alivyojidhatiti kupambana na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na udhalilishaji wa watoto na hata kufikia hatua ya kuundwa kwa Mahakama ya Udhalilishaji ambayo hivi sasa tayari inaanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Nampongeza sana Mhe. Makamu wa kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, lakini pia nampongeza Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia sana Mhe. Rais katika jitihada hizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyokumbuka tarehe 11 mwezi wa Novemba, 2020 Mhe. Rais alizindua Baraza la Kumi la Wawakilishi na alifanya hivyo kwa mujibu wa Katiba yetu kifungu

cha 84.  Katika uzinduzi wa Baraza alitoa hotuba na kwa kweli iligusa maeneo yote ikiwemo maeneo ya kimaendeleo, aligusa sekta za uchumi, huduma za kijamii, alizungumzia sana masuala ya amani na utulivu, mshikamano na umoja wa wananchi wote, aligusa masuala ya utawala bora (utawala wa sheria), kupambana na rushwa na ufisadi. Alizungumza pia utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi na mengine mengi ambayo yamo katika hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hotuba hii kuwa imesheni mambo muhimu sana kwa maendeleo ya nachi yetu. Mjumbe mwenzetu Dkt. Saada Mkuya Salum aliita hotuba hii ni *Golden Speech* na kweli ni hotuba ya dhahabu kwa sababu ilikua na uchambuzi wa kina wa hali halisi katika maeneo yote lakini pia ilitoa muelekeo na dhamira ya dhati kabisa ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi na ya kasi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Saada Mkuya Salum, alitoa hoja ya kwamba hotuba hii ijadiliwe katika kikao hichi na hoja hiyo tuliunga mkono wajumbe wote tuliokuwepo katika kikao kile. Sasa hii leo wakati umefika wa kuijadili hotiba hii na kwa sababu hoja imeshatolewa sitotoa hoja nyengine.

Lakini Mhe. Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe niwaombe tu kwamba tuchukue fursa hii kuijadili hotuba ya Mhe. Rais na kwa kweli iwe ndio dira ya kutuongoza sisi tunaomsaidia, pamoja na sisi wawakilishi katika kuhamasisha wananchi katika maeneo yetu, ili kumuunga mkono katika jitihada za safari yetu ya kuleta maendeleo katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo maneno ya utangulizi, sasa naomba kuruhusu mjadala uendelee, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Lakini kabla sijawapisha wachangiaji ambao nimepata orodha hapa naomba niwakumbushe kanuni ya 59(6) naomba kunukuu.

Kanuni ya 59(6) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar inaeleza hivi:-

> "Kila mjumbe anaejadili hoja ataruhusiwa kuzungumza kwa muda usiozidi dakika 10 kwa mikutano ya kawaida na dakika 15 wakati wa mikutano ya bajeti, lakini Mhe. Spika akiona inafaa anaweza kumuongeza mzungumzaji muda usiozidi dakika 10."

Kwa hiyo, nimeona niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe ili kila anaesimama na kuchangia akumbuke kwamba kanuni zetu zinaturuhusu hivyo.

Kwa maana hiyo nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, kila ambae anachangia aende katika taratibu hizo na sio vyenginevyo.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba nimuite mchangiaji wetu wa kwanza Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, atafuatiwa na Mhe. Shamata Shaame Khamis na  Mhe. Juma Makungu Juma ajiandae.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** *Bismillah Rahmani Rahim,* Mhe. Mwenyekiti naomba kuchangia Hotuba ya Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ambayo umesomwa Novemba 2020. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya, uzima kwa sote lakini vile vile niwashukuru viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi walioniweka mimi madarakani pamoja na jimbo la Chaani wananchi wangu wote nawashukuru sana kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwaambie wananchi wote au niwaambie viongozi wenzangu kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi aliyemaliza kutoa maelezo pamoja na Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum sio peke yake ni *golden speech* tu bali Mhe. Rais mwenyewe ni dhahabu ukiacha *speech* yake. Maana yake ni maneno yake ni dhahabu na yeye mwenyewe ni dhahabu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Rais wetu kwa ukweli wake, kwa kuleta amani, kwa kuleta upendo na kuleta maendeleo ya kasi na ufanyaji wa kazi wa kasi ndani ya muda mfupi. Vile vile nampongeza sana kwa kukubaliana na kufanya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ili kushirkiana na wenzetu na leo humu ndani tunao tunaishi nao vizuri na hatuhisi kabisa kama humu ndani tumo vyama tofauti bali tunahisi sote ni wanzanzibar tunafanya kazi kwa pamoja, hongera sana Mhe. Rais. *(Makofi)*

Nimpongeze sana kwa uteuzi wa makamu wake wa Pili wa Rais. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais namfahamu tokea tupo kwenye kamati za Mkuu wa Mkoa mpaka leo amefika cheo hicho. Mtendaji mzuri na yuko *fit* na kijana, hapo hata ukimdanganya ukimwambia jambo lipo kwenye mtende au kwenye mnazi anapanda mnazi mpaka juu mwenyewe. Pia, nampongeza Mhe. Makamu wa Kwanza Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad lakini yeye ni mtu mzima hatoweza kupanda mnazi, atoweza kupanda mnazi ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naamini sana mwanzo alioanza nao Dkt. Hussein Ali Mwinyi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwneyekiti wa Baraza la Mapinduzi peke yake ni faida tosha kwa Zanzibar na nataka nikwambie kama ni *shares* basi *shares* zimepanda ndani ya Zanzibar kama ingelikuwa kuna watu wameweka *stock marketing* biashara zao basi *shares* zimepanda na zimepanda kwa nini. Kwa kweli, zimepanda kutokana na amani iliokuwepo, upendo uliokuwepo na kasi ya maendeleo na nguvu alioanza nayo ndani ya siku mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tukipigania sana na tulikua tukilalamika sana sio sisi wana CCM wala sio wapinzani, kwamba tunahitaji Mhe. Rais kijana, ambae atatumbuwa watu, atakemea, atazuia fedha na atafanya mambo mengi yaliokuwa ya muhimu. Hivi sasa wakati wake umefika na tunayaona jengine lipi ambalo tunalitaka zaidi ya hili. Kwa mfano, ikiwa tunaona kuanzia viongozi wote walioteuliwa, kwa wale waliopata rizki ya kuteuliwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakukubali sana kwa utendaji wako wa kazi. Waheshimiwa Mawaziri nakupongezeni sana kwa uteuzi mlioupata na hususan Katibu Mkuu Kiongozi mwanamama nampongeza sana na niwape taarifa tu kwamba Katibu Mkuu Kiongozi yupo *fit* na inasemekana anapigana karati. Sasa mujitayarishe mbali ya kazi ambayo anaweza kuifanya pia yupo *fit* kwenye mazoezi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwamba mambo yaliyoongelewa humu kwenye hotuba ni mambo mengi masuala ya uchumi wa buluu, masula ya barabara, masuala ya maji na nishati, masuala ya kilimo, masuala ya mifugo, masuala ya viwanda na biashara na mambo mengineyo muhimu ndani ya nchi yetu. Kwa kweli, ndani ya muda mfupi vitu ambavyo vimetiliwa sahihi ya *MOU* hivi karibuni masuala ya bandari, masuala ya gesi na masuala ya uvuvi wa buluu mambo ya meli ya uvuvi, masuala ya viwanda vya mwani na masuala mengineyo yote ndani ya siku mia moja. Hesabu yake kwenye *investment* ile ni zaidi ya bilioni mia tano kwenye *project* ile lakini *project* ile tusiangalie kwamba *investment* inakuja kufanyika bali ajira zitakuwepo pale nyingi nchi itapanda thamani lakini vile vile heshima ya Zanzibar kwenye uchumi itakuja juu.

Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama kuna mtu ana sababu kwa muda huu na tunaokwenda nao mbele kwa serikali ambayo tunayo sasa hivi, ambae ataweza kusimama na labda kubishana na kusema kuna vitu havioni vinavyofanyika. Mhe. Rais kaanza na *speed* kubwa pamoja na viongozi wake wote wanafanya kazi kwa *speed* kubwa na hata mimi nimkosoaji mzuri sana lakini mpaka hadi sasa sina kimoja cha kukikosoa kwa sababu sijakiona tuzungumze ukweli.

Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote sisi ndio tunatakiwa tuoneshe mfano kumsaidia Mhe. Rais ukiacha viongozi wengine ndani ya nchi hii. Sisi ndio tunaofaa kuwa Makamu wa Pili wa Rais, tunaofaa kuwa Mawaziri, tunaofaa kuwa Manaibu Waziri hawezi kuwa mtu mwengine yeyote ndani ya nchi kuwa na vyeo hivi kama hajapitia kuwa mwakilishi.

Sasa mfano wetu tukamsaidie Mhe. Rais hata kwenye majimbo yetu kwenye kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini kwente kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu, tuoneshe mfano sisi na sisi tunamuahidi hata kama hatulipwi tutamsaidia kwa sababu ya moyo wake na nafsi yake anayotuonesha na imani yake na upendo wake kwa wananchi wa Zanzibar tutamsaidia bila ya kujali mishahara, bila ya kujali maposho na masuala mengineyo kuhakikisha kwamba serikali yetu inafanikiwa na huko mbele hatuji kupata tabu. Naamini hata ndugu zangu wa upinzani tulionao humu ndani kwa upendo tulionao basi ipo siku na wao wataingi CCM. *(Makofi)*

Hii nasema dhahiri kwa sababu tunaonesha kwamba sasa hivi Zanzibar ni kitu kimoja na walichokuwa wanakitaka wao wapinzani kwamba ni maendeleo na tunachokipigania sisi na wao kila siku ni maendeleo. Tuone maendeleo, tuone ajira, nchi inakuwa kiuchumi na masuala ya unyanyasaji na mengineyo yanaondoka. Sasa ikiwa Mhe. Rais wetu haya mambo yote yanapatikana tena kwenye siasa tunataka nini huko mbele. Ningeomba sana sote tujitathmini tulichokitaka tushakipata serikali tuliokuwa tunaitaka ambayo tunasema iende na mfumo huu ndio serikali hii tulonayo sasa hivi. Nafahamu kwamba Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na viongozi wote maadui mtakuwa mnao wengi, mimi nimeota hivi karibuni nasema mimi nimeota wanarogwa kweli kweli.

Wapo wanaowaroga kutaka vyeo, wapo wanaowaroga kutaka kupendwa lakini Mwenyezi Mungu amewapa *protection* anawalinda. Ninachowaomba viongozi hawa waendelee kufanya kazi wasiogope mtu kwa yeyote yule aliyefanya makosa atumbuliwe, aliyechukuwa fedha ya umma airejeshe tunaomba sana na sisi tupo tayari kumsaidia na nikiwa mjumbe wa Kamati ya Uchumi ningewaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wafuatao Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Waziri wa Uchumi na Kazi, Mhe. Waziri wa Utalii, Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda atakaekuja, Mhe. Waziri wa Mawasiliano, Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu ni lazima

mushirikiane ikiwezekana make vikoao kila wiki kuangalia munaenda na ajenda gani ya kumsaidia Mhe. Rais kwenye kuinuwa uchumi kwenye *department* zenu na wizara yenu kwa ujumla. Mawaziri hawa niliowataja mawaziri sita au watano ndio mnaopaswa kuinuwa uchumi huu wa Zanzibar mkiangalia mambo yote alioyaahidi Mhe. Rais mnayo nyinyi kwenye mawizara yenu mawaziri watano kwa sita na kama tutakuja kumuangusha Mhe. Rais kwa awamu hii maana yake kwamba tutaanza kumlaumu mmoja mmoja.

Tunachotaka kuona kwamba kila waziri anakuwa *creative* kwenye kuandaa, kuleta wafanya biashara na kufanya watu wenye *investment* waliokuwa wana uhakika na wenye maana. Naomba sana watu wote wanaohusika wasimpelekee Mhe. Rais watu wenye kufanya *investment* ambao hawana uwezo na kazi zao za utapeli bali Mhe. Rais atakapofanyiwa *appointment* ya kuonana na wafanyabiashara wawe wamechunguzwa, wana uwezo na wana uhakika wa kufanya jambo na sio kwenda ikulu kutembea.

Nazungumza haya kwa sababu tushaona kila mmoja atakwenda ikulu kila mmoja anataka kwenda kwa Mhe. Rais na ifike wakati tuende na viwango ikiwa mtu anataka kufanya uwekezaji wa bilioni moja mpaka bilioni kumi basi akaonane na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais au Mhe. Waziri lakini mwenye uwekezaji mkubwa ndio anapaswa kwenda kumuona Mhe. Rais. Mimi binafsi na uwakilishi wangu sijui hata mlango ikulu ukoje sijawahi kuingia na wala simuonei mtu choyo kwamba nazuia mtu asiende lakini waende watu wenye uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, uchumi wa buluu tunaokuja nao tushaanza kuona mafanikio yake na uchumi huu utakapoendelea ndani ya mwaka mmoja mpaka miaka miwili tutakuja kuona Zanzibar sasa inakuja juu haraka iwezekanavyo. Vitu vinavyo taka kuja sasa hivi vinavyoletwa na Mhe. Rais kwa ujumla. Mhe. Mweneyekiti, niendelee kusema kumshauri Mhe. Rais kwamba likimpendezea kwamba hata kuanzia sasa magari ya bei kubwa yasinunuliwe ndani ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Unakuta gari anatembea nalo mkurugenzi au Katibu lina thamani zaidi ya milioni mia moja nidhamu ya matumizi haipo, leo gari anayotembelea Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na gari anayotembea nayo Mkurugenzi kiwango ndio hicho hicho hafahamiki Makamu wa Pili nani Mkurugenzi nani.

Kwa kweli, inavyotakiwa nchi zote viongozi hawa wa juu wawe wanatumia gari kulingana na hadhi zao na sio zinazofana na watu wa chini. Leo Zanzibar nidhamu ya manunuzi ya gari haipo. Mkurugenzi, Katibu hafamiki huyu Waziri Naibu Waziri wala ana cheo gani na wenye kutumia gari za thamani katika nchi ni watu wafuatao. Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Rais, Spika, Jaji Mkuu na Waheshimiwa Mawaziri. Waliobakia watumie gari za milioni ishirini na thelathini hakuna haja tena ya kutumia pesa kwenye gari za bei kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la uwekezaji. Tunafahamu na tunaona kwamba kuna watu wamehodhi viwanja vikubwa *square meter* elfu ishirini kwenda juu maeneo ya baharini zaidi ya maeneo mia mbili. Tunataka kusema kama Kamati ya Uchumi tutafuatilia kiwanja kimoja kimoja kuhakikisha watu waliochukuwa maeneo makubwa sasa wanajenga hoteli, wanajenga nyumba na kama hawawezi kwa usalama wao warudishe waseme hawawezi bali wasituletee utapeli kwenye nchi yetu na hususan wageni. Kuna wageni wanachukuwa ardhi hapa wameenda kuomba mikopo kwao wanafanyia uwekezaji sehemu nyengine na sio Zanzibar.

Sasa tunachoomba kwenye serikali hii muhali umekwisha na ikiwa mtu wenzetu huko nje wapo waliofungwa kwa kuiba ndizi na baskeli na wanafungwa miezi sita wananyang'anywa vitu wanarejesha vitu kama kuna mtu ameiba fedha na amejulikana na kuna mambo yamefanyika yaliokuwa siyo ni vyema na yeye akarejesha tukaendelea na kazi tukamsaidia Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru sana naonga mkono hoja hii asilimia mia moja ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Shamata Shaame Khamis atafuatiwa na Mhe. Juma Makungu na Mhe. Habib Ali ajiandae.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nitumie fursa hii kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Rais ambayo alitoa siku ambayo alizinduwa Baraza letu hapo Novemba 11, 2020. Kwanza kabisa naomba nianze na utangulizi wa kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu na ile *slogan* ya kwamba "Yajao ni Neema Tupu" tumeshaanza kuiona kwa vitendo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wasaidizi wake Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini vile vile nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi kubwa nzito ambayo anaendelea kuifanya pia nae katika nchi yetu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri pamoja na wasaidizi wengine kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika kubadilisha taswira za muonekano katika hali ya kiuchumi ambayo tunakwenda nayo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nitumie fursa hii kuipongeza sana serikali ya awamu ya saba nayo kwa kazi kubwa ambayo iliifanya ambayo na Mhe. Rais ameahidi kuendeleza pale ambapo pamefikiwa. Kwa haraka haraka nitumie fursa hii kuwapongeza sana wapiga kura wananchi wa jimbo la Micheweni kwa kuniamini ama kwa kuendelea kuniamini baada ya Chama cha Mapinduzi kuridhia jina langu liingie katika kinyang'anyiro na mwisho nikaweza kuwepo hapa kwa kuwaakilisha naomba niwaahidi kwamba bado nitaendelea kuwatumikia kwa unyenyekevu mkubwa na kwa huruma kubwa. Baada ya maelezo hayo pia nitumie fursa hii kuipongeza pia na familia pamoja na wazazi na jamaa na ndugu kwa kuwa karibu na mimi na kunishauri nakunisaidia mambo mengi ili niweze kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba hotuba ya Mhe. Rais ambayo aliitoa hapa mbele yetu ambacho nathubutu kusema kwamba imezingatia vigezo vyote na imekamilika na ni imani yangu kwamba kwa kasi hii na tutakapofanikisha kazi hii nadhani huko majimboni kwetu hakutakuwa na manung'uniko na masikitiko ya namna gani ya kuzipata huduma ambazo wanazitarajia. Vile vile Mhe. Rais wakati alipokuja hapa alisema kwamba wananchi wa Zanzibar wanachokihitaji sasa hivi, hawahitaji simulizi za Mapinduzi wala simulizi za Muungano wanachokihitaji zaidi ni maendeleo kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, kazi hii imefanya tokea Rais wa awamu ya kwanza Mhe. hayati Abied Amani Karume na marais wengine wote ambao wametangulia walifanya kazi hii kwa moyo mkubwa na kutokana na zama hizo na mpaka sasa hivi kazi inaendelea. Kwa hiyo, niwaombe sana kwamba hotuba hii na maneno haya mazito tunapaswa kila mmoja na sisi tuwajibike katika kuona kwamba tunamsaidia Mhe. Rais katika kutimiza hili.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Rais alisema wawakilishi wa wananchi hapa Barazani alikuja kwa sababu sisi tuna kazi miongoni mwa kazi mbili pia tunatakiwa tuzifanye kama wawakilishi. Kazi ya kwanza kwake yeye alituomba ni kwamba kufahamiana lakini vile vile kumsaidia kazi kwa kumshauri na pia kuisimamia serikali kwa kuyatekeleza yale ambayo imeyapanga. Naomba niahidi kwamba kazi hii tutaendelea kuifanya kwa moyo thabiti kutokana na uwono wa hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kilimo. Mhe. Rais alisema katika serikali hii baada ya mwendelezo wa serikali ya awamu ya saba alisema kwamba ataendeleza nma ule mpango mkuu wa umwagiliaji maji Zanzibar yaani Zanzibar *irrigation master plan* ambapo amebainisha kuwa zito hekta elfu nane mia tano ishirini na moja (85021) zinazofaa kujengwa miundombinu ya umwagiliaji maji na kwa kweli alisema kwamba serikali ya awamu ya saba iliweza kutekeleza elfu mbili mia tano ishirini na saba (2527) na zinaendelea kujenga na miundombinu ya umwagilia maji kutoka mia saba za mwaka 2010 na ujenzi huo utaendelezwa katika mabwawa mbali mbali ambayo Mhe. Rais ameyataja.

Maana yangu ni kwamba kuainisha haya ni dhamira njema na nidhahiri kwamba Mhe. Rais kwa namna gani ambavyo amekusudia kufanya kazi kubwa katika sekta ya kilimo ambacho ndio tegeemeo letu katika nchi yetu ndio hitajio letu kubwa. Kwa hiyo, hata asubuhi tuliweza kuona mijadala kila Mheshimiwa Mjumbe alikuwa na shauku ya kuweza kujua kwa namna gani anaweza kupata mahitajio haya katika sekta nzima ya kilimo. Vile vile Mhe. Rais, katika sekta hii pia alisema kwamba anakusudia pia kuhakikisha pia serikali itahakikisha itaendeleza huduma kwa kuajiri wataalamu wa kutosha pia kutoa vifaa vinavyohitajika kwa sekta ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo la faraja sana na kumpongeza sana Mhe. Rais wetu na haya uwezekano huo upo. Kwa kweli, bahati nzuri sana tunacho Chuo cha Kilimo Kizimbani nadhani tokea mwaka 2017 wakati hakijaunganishwa kuwa tawi la *SUZA* kulikuwa na vijana wengi na dhamira ya serikali kwa wakati ule ilisema kwamba inafundisha vijana kutoka vijana katika chuo kile ili baadae warejee makwao vijijini wakaweze kutoa huduma, leo asubuhi tumshuhudia pia kwamba baadhi ya wafanyakazi wanaajiriwa wanakwenda mazingira ya vijijini hatimae wanataka kurudi. Kwa hivyo, hii itasaidia sana na kwa bahati nzuri vijana hawa wapo nadhani kama 150 kama sikosei, 25 wa fani ya mifugo na kilimo 150 nadhani itakuwa ni sehemu nzuri tukizingatia kuangalia rasilimali hii kuweza kuitumia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la barabara Mhe. Rais amezungumza vya kutosha na kwa bahati nzuri yale ambayo yakilalamikiwa sana na wananchi ni suala la barabara, hatuwezi kuwa na uchumi ambao utaendana na uchumi wa *bluu economic* zikiwa barabara zetu bado ziko katika hali mbaya. Lakini Mhe. Rais akaliona hili na akaona, ili tuende sambamba na uchumi wa buluu maana yake lazima tuwe na barabara safi, ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami na iweze kuonekana kwamba zitasaidia kuweza kuharakisha azma hii njema ya serikali pamoja na Mhe. Rais, ambayo pia inatokana na msingi mzima wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, hili sote kwa pamoja tumeshaanza kuliona kwa vitendo kwamba Mheshimiwa sasa kazi imeshaanza na kwa bahati nzuri cha kufurahisha sana, ambacho wananchi wa jimbo la Micheweni pia wamenituma nimuombee dua kwa niaba yao Mhe. Rais kwa kazi kubwa

anayofanya kwa mara nyingi tumeanza kuona mikakati wa kuona kwamba wananchi wa jimbo la Micheweni watashuhudia kuona barabara ya kiwango cha lami ambayo itatoka *round about* Micheweni itaelekea katika maeneo ya uwekezaji, hii ni dhamira njema sana ni kwamba Mhe. Rais wetu anaposema na hii ndio kawaida ya viongozi wa CCM, kwa hivyo moja kwa moja anakwenda kutekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikupe habari njema kwamba sasa hivi kazi ya ujenzi wa barabara katika jimbo la Micheweni inaendelea na hii imetokana na hotuba ya Mhe. Rais tumeiona namna aliyoyasema baada ya kusema utekelezaji unaendelea.

**Mhe. Mwenyekiti:** una dakika mbili Mheshimiwa.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Zinanitosha Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja mimi niende katika suala zima la afya Mheshimiwa amesema atahakikisha kwamba hospitali na vituo vya afya vipya vitajengwa, lakini vile vile tutakarabati skuli na mambo mengine. Kwa kweli, naomba niseme tu kwamba ni jambo la furaha sana kila mmoja wetu anahitaji kupata huduma za kiafya na hakuna mmoja ambae anaweza kukwepa hili, Mhe. Rais, hili kaliona na naomba pia tumpongeze sana kwamba jitihada hizi nazo zinaendelea tumeona mipango mbali mbali katika nchi yetu imeanza kuonekana katika kuhakikisha kwamba jambo hili litafanikiwa.

Kwa hiyo, naomba niende haraka haraka kabla sijamalizia dakika zangu mbili kwenye sekta ya uchumi wa bluu kama ambavyo tumesema, tunakwenda kwenye uchumi wa bluu Mhe. Rais kasema mengi. Kutokana na hali hiyo, naomba tu kwamba tuongezee tu kwa wizara zenye dhamana tunao wataalam wa kutosha kwa wananchi wetu wengi hususan wavuvi wamekuwa wakilalamika sana, sheria zetu ambazo tumekuwa tunazitunga wakati mwengine kumekuwa na malalamiko na manung'uniko kwa mfano sisi tuliosoma kilimo. Katika ufaulu wa mwanafunzi aliyesoma chuo anatakiwa asilimia 40 awe ni *theory* kwamba anaweza kufahamu na ku-*perform* kinadharia, lakini asilimia 60 aende kwa *practice*, lakini inavyoonekana wataalam wetu wa uvuvi bado hawajajikita kwenye *practice* zaidi na badala yake unakuta ni utaalam zaidi wa kinadharia.

Kwa hiyo, ni vyema tuongeze angalau kidogo hivi sasa tuwafanyie mafunzo angalau ya kufanya *diving system* wale wataalam wetu angalau waweze kujua hali halisi ya huko baharini ilivyo, maana yake vile tutakavyomsaidia Mhe. Rais tutamsaidia vizuri zaidi, kwa sababu inawezekana mtu anaweza kujua kwamba baharini kuko hivi na hivi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme tu baharini hali ya mazingira yake inabadilika katika upatikanaji wa samaki tunakwenda na uchumi wa bluu na nashukuru Mhe. Rais kaahidi vyombo vingi vitanunuliwa kwa kuwaletea wavuvi wetu.

Sambamba na hilo naomba sana Mhe. Waziri basi na hili tuangalie wale wavuvi wetu wanapofanya utafiti na kutoa taarifa basi angalau kuwe na wataalam ambao wanaweza kufanya *diving system* ya hali halisi ya upatikanaji wa samaki, tusiwe kwamba sisi wataalam tushindwe maarifa na wavuvi ambao hawajasomea taaluma hii kwa kuwa ni mvuvi nilikuwa na nataka kuona hali halisi kuweza kuisaidia zaidi.

Kwa hivyo, baada ya maelezo hayo naomba sana niipongeze kwa asilimia mia moja hotuba ya Mhe. Rais kwamba hichi kimekuwa ni kitabu ambacho kitatupa dira na mwelekeo mzuri katika kupata uchumi mzuri, na mafanikio makubwa na kujenga majimbo yetu ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Shamata Shaame nakushukuru sasa naomba nimuite Mhe. Juma Makungu, atafuatiwa na Mhe. Habibu Ali na Mhe. Aza Januari ajiandae.

**Mhe. Juma Makungu Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Husein Ali Hassan Mwinyi aliyoitoa siku ya ufunguzi wa Baraza lako tukufu tarehe 11 Novemba, 2020.

Awali ya yote nianze kumshukutu Mwenyezi Mungu *(Subuhana Wataala)* kwa kunijaalia uhai na uzima wa kuweza kuja katika Baraza lako tukufu hapa kwa kuweza kuchangia hotuba hii. Lakini pili niwashukuru kwa dhati wananchi wa jimbo la Kijini kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi kuwa muwakilishi wao na leo hii nasimama kwa niaba yao. *(Makofi)*

Lakini tatu niwashukuru kwa kuanza na Mhe. Rais, Makamu wote wawili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri na wateule wote wa Mhe. Rais kwa namna ambavyo wanafanya kazi kwa kujituma kwa uzalendo, kama alivyosema Mhe. Rais vigezo vitatu vile vinatuonyesha namna ambavyo binaadamu anatakiwa awe katika kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki kimeeleza mengi na wengi bila ya shaka watasema mengi, lakini naomba niseme machache tu. Kwanza nianza na upande wa barabara, ukiangalia ukurasa wa 19 Mhe. Rais ameeleza barabara ambazo vitajengwa kwa kiwango cha lami naomba ninukuu kidogo; "Miongoni mwa barabara zitakazojengwa kwa Unguja na Tunguu, Jozani, Charawe/Ukongoroni, Bwejuu, Fumba/Kisauni, Kizimbani/Kiboje, Kichwele/Pangeni, Umbuji/Uroa na Mkwajuni/Kijini". Hapa ndio penyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nimeshukuru sana kuiona hii barabara kwanza iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na Mhe. Rais akaja akaisisitiza hapa utengenezaji wa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Kijini na ni njia moja katika njia kubwa na ya zamani lakini kwa bahati mbaya ilikuwa muda wake bado wa kuwekwa lami.

Mhe. Mwenyekiti, naombe sana viongozi wetu kwa maana ya Mawaziri hasa wanaouhusiana na Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi hapa katika upangaji kutajwa haijatajwa mwanzo lakini ikiwezekana sijui hizi nyengine umuhimu wake kwa maana ya ubovu wake na harakati zake zilivyo, lakini ingependeza sana kama hii ingeanzwa mwanzo.

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hivi sasa wananchi wa Jimbo la Kijini wanapata tabu sana wanalazimika kama wanatoka safari zao kwa wale ambao wanaijua *geography* ya kule wapitie Kigomani, Mbuyutende ndipo wafike Kijini na huko kwenyewe gari hazifiki kule kwa sababu njia sio nzuri kwa hivyo wanalazimika kutembea masafa marefu kwa miguu kwa sababu hamna usafiri. Sasa kutengenezwa kwa njia hii maana yake ni ukombozi mkubwa kwao kwa vile watakwenda na kurudi katika shughuli zao za kiuchumi.

Lakini sio hilo tu bali pia wawekezaji kwa sasa tunafahamu kwamba kuna hotali moja kubwa kule ya Mnemba, kuna hoteli nyengine zinajengwa zenye hadhi ya nyota tano lakini pia wanapta usumbufu wa kwenda na kurudi na wageni, wanalazimika kupita hiyo njia ambayo nimeitaja mwanzo lakini pia ikiwa wanataka kwenda Nungwi kwa sasa wanalazimika kuzunguruka sana na wakati *short cut* ingewasaidia kama ingekuwa inapitika vizuri. Sasa niombe sana njia hii iangaliwe ikiwezekana iwe njia za mwanzo ambazo zitajengwa kwa hapa Unguja.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa 27 na 28 kwenye suala zima la maji kama tunavyofahamu kwamba maji ni uhai na kitabu hichi kimeonesha dhamira halisi ambayo inaelekea kulitatua tatizo hili la maji, lakini mimi naomba nishauri hapa kwa sababu hapa inasema pamoja na kujenga matangi mapya ya kuhifadhia maji, uchimbaji wa visima vipya vya maji na kuendelea kuvifanyia matengenezo miundombinu ya zamani, sina tatizo hili.

Lakini ningeshauri kwamba awamu ya saba iliweka mikakati ya kuvimaliza vile visima vilivyochimbwa na Ras-Al-hemah sasa sijui kwa sasa imefikia hatua gani, lakini ningeshauri kwanza tungeweka nguvu hapa ya kwenda kuvitengeneza na kuvikamilisha kuliko kuchimba vipya, kwa sababu vile visima ni vingi lakini vimechimbwa katika maeneo ambayo wataalam wamethibitisha kuna maji mengi na ya uhakika.

Kwa hivyo, ukamilifu wa visima hivi kungesaidia sana upatikanaji wa maji kwa sababu vile visima vipo mijini na vijijini na hasa ukizingatia Mhe. Waziri wa Maji bila ya shaka ameshazunguruka sana kule Kibuyuni pale Kiashange kuna visima ambavyo vinahitaji kukamilishwa na kuingizwa kwenye *tank* kubwa la Kibuuni kusudi lipeleke maji sehemu ya Pwani Mchangani na Matemwe.

Mhe. Mwenyekiti, imani yangu ukamilifu wa visima vile kuingia kwenye tank pale Kiashange tatizo kubwa la maji kwa Matemwe litapungua. Sambamba na hilo kwa hapa naomba niunganishe pia pamoja na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Waziri wa Maji, Nisharti jana nilitoa *brief* kwenu kwamba kuna siku nitakuombeni tufanye ziara ya pamoja kwa ajili ya kwenda kuangalia namna gani tunaweza kuyachukua maji kutoka pale Matemwe kutoka bomba kubwa la *ADB* kupeleka Kigomani kwenye njia mpya ya lami, kusudi tatizo la maji Kigomani limalizike na miaka mitano hii ndio linakwenda kumalizika kabisa hili tatizo la maji Kigomani.

Lakini niende kwenye ukurasa wa 33 Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na mambo ya mikopo ya uwezeshaji kwa maana ya mkopo wa wananchi vijana wa kike, wavuvi nimeelezwa sehemu nyingi kwenye ukurasa wa 11, 29 na 33. Kwa kweli, naomba sana hapa Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hasa Waheshimiwa Mawaziri wawe makini sana si tu kupata idadi ya kwamba tumetoa vikundi vingapi au kwa watu wangapi mikopo hii, isipokuwa ni muhimu sana kujua kwamba mikopo hii imetolewa kwa watu wepi katika maeneo yetu kama tuna wilaya 11 ni vyema basi tungekuwa na mipango asilimia ngapi zisipungue katika kila Wilaya, vyenginevyo utakuja kukuta bin Kinanat, bin Hudhaimat, bin Mudirikat, bin Iliyasa ndio waliopata wale waliokuwa hawana majina watakuwa hawapati, itakuwa sio jambo jema na sio azma ya serikali kufanya vitu hivyo kwa ubaguzi.

Kwa kweli, hayo Mhe. Rais mwenyewe pia alisisitiza katika ukurasa wa 29 naomba kunukuu kidogo pale aliposema "katika kuhakikisha kwamba mkakati huu unaleta ufanisi tunaotarajia tutakuwa tumefuatilia kwa karibu na kufanya tathmini ya mikopo tunayoitoa kwa vikundi hivyo, ili kujiridhisha endapo inawafikia walengwa na kwamba hakuna matumizi mabaya ya fedha hizo yanayowafanywa na watumizi wa serikali wasio waaminifu".

Suala hili ni muhimu sana katika kumsaidia Mhe. Rais kuhakikisha kwamba mikopo inayotolewa haitolewi tu sehemu moja bali inatolewa sehemu zote za Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba mijini na vijijini, kwa sababu ukizingatia mjini kufika kwenye ofisi ni rahisi kuliko kumtoa shamba lakini pia uelewa wa namna gani hiyo mikopo inapatikanwa basi ingekuwa vyema ikatolewa kwa uwazi kusudi ili wananchi hasa wale wa vijijini wakapata kujua na wao wakatumia fursa hii ya kupata mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa afya imeelezwa hapa kwamba serikali itajitahidi kujenga nyumba za madaktari lakini pia ununuzi wa vifaa tiba na madawa. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Mawaziri wafanye ziara za mara kwa mara hasa kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi watakuonesheni changamoto nyingi katika maeneo yao hasa vijijini, kwa sababu wakati mwengine si vyema mpaka aje Mhe. Rais aje aambiwe changamoto zile ambao tungeweza kuzitatua kabla ya kuja kwake itakuwa haipendei sana.

Kwa mfano, pale Kigomani kwenye jimbo la Kijini kuna nyumba imejengwa kwa ajili ya madaktari lakini bado haijakamilika, hali kadhalika kuna kituo ambacho dawa zake hazijapatikana vizuri sana. Kutokana na hali hiyo, ingekuwa vyema sana Mhe. Waziri ndhani wa TAMISEMI akipata muda wa kuja kutembelea basi naomba nimuoneshe kile kituo pamoja na ile nyumba kusudi serikali ione nguvu gani inaweza kuweka pala na kuunga mkono juhudi za wananchi na serikali yao kwa jumla.

Mwisho Mhe. Mwenykiti, naona unawasha taa naomba niende kwenye uvuvi kiduchu kwa sababu ni mtu wa pwani. Katika uvuvi hali kadhalika kama mlivyosema kwenye mikopo ya vijana na wale akinamama nilizungumza na Mhe. Waziri wa Uchumi wa Bluu na tulikubaliana kwamba tutakwenda siku moja kufanya ziara kule ya wavuvi, na ni imani yangu kwamba tutaifanya hiyo ziada kabla ya kikao cha Baraza kijacho kusudi wakapate changamoto za wavuvi, kuna changamoto nyingi ziko chini na pa kusemea maana yake pale anapokuja Waziri au mtendaji wa serikali kusudi wazione na nyengine inawezekana zinasababisha na watendaji wetu wa serikali.

Imani yangu ni kwamba tutakwenda tukazione, kwa sababu kuna tatizo ambalo linahusiana na Mnemba na pale kuna marine amamimka kuna tatizo kubwa sana wavuvi wana hamu sana ya kumpata kiongozi wakamlalamikia au kumueleza, imani yangu kwamba Waziri akifika akiyapata yale atayashughulikia na ukizingatia kule kuna ahadi ya Mhe. Rais Mbuyutende kwamba atakwenda kipindi kile wakati anagombea aliwahi kufika na akazungumza na wavuvi lakini pia aliweka ahadi kwamba atafika na muungwana akiweka ahadi hutekeleza. Kwa hivyo, kabla hajatekeleza ingekuwa vyema Mhe. Waziri wa Uvuvi tukafika pale kusudi yale ambayo yako kwenye mamlaka yake akayatengeneza kabla ya yeye kuja.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi namna ambavyo alianza mwanzo wengi walimbeza, lakini sasa wengi wanampongeza miongoni mwao ni wale ambao walimbeza kwamba asingeweza kufanya jambo. Lakini kweli uungwana ni vitendo na atunashuhudia tunamuombea Mwenyezi Mungu amjaalie umri mrefu, ili aweze kuyatekeleza yale aliyokusudia ikiwa siku mia tu tumeona haya tuliyoyaona, miezi sitini tunategemea mengi zaidi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia nashukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru Mhe. Juma Makungu kwa mchango wako. Sasa naomba nimuite Mhe. Habibu Ali Muhamed atafuatiwa na Mhe. Aza Januar Joseph na Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum ajiandae.

**Mhe. Habibu Ali Muhamed:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii kwa mara ya mwanzo kuingia katika ukumbi huu kwa ajili ya kuwakilisha wananchi wangu wa jimbo la Mtambwe ambao walinipa ridhaa kubwa kwa kura nyingi walizonichagua, kwa bahati katika jimbo la Mtambwe ni jimbo pekee niliweza kupata fomu za matokeo nilipata kura zaidi ya elfu tatu. Kwa hivyo nawapongeza sana wananchi wangu wa jimbo la Mtambwe wa vyama vyote vya siasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kipindi kifupi cha siku mia kwa kuweza kufanya mambo makubwa, leo hii tumeona ameweza kuanzisha wizara ambayo katika awamu zote hatukuweza kuisikia kwa hivyo tunamuona ni mtu ambae ni *creative* Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu wengi walikuwa hawajui uchumi wa bluu ni nini.

Kwa hivyo, hata ukifika katika mabaraza utasikia watu wanasema uchumi wa bluu, kwa hivyo kuna haja kubwa kabisa waziri anayehusika awaelimishe wananchi walioko chini kwa sababu kuna wananchi wanasema uchumi wa bluu wengine wanasema kwa nini usiwe uchumi wa zambarau. Nawambia uchumi wa zambarau bado ushanifahamu ukifika wakati utaambiwa tunaweza tukabadisha uchumi wa bluu kwenda zambarau. Uchumi wa kijani baadaye huo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hichi kifupi tumeona kwenye sekta ya utalii juzi nilipita pale katika kiwanja cha ndege nimeona kuna ndege karibu tano kubwa. Kwa hiyo, kuna ongezeko sana la watalii ambayo inaweze fursa kubwa ya kuongeza mapato kwa serikali na amini katika kipindi kinachokuja kifupi inawezekana hata *parking* ikakosekana pale.

Kwa hiyo, naishauri serikali ifungue ofisi *agencies* kwa zile nchi ambazo zina watalii wengi kuhamasisha watalii waingie katika kisiwa hichi cha Zanzibar na jengine tuboreshe hoteli zetu ukiangalia katika kisiwa cha Pemba sasa hivi hoteli ziliopo ni za daraja la chini. Kutokana na hali hiyo, tunaiomba serikali iangalie mkakati wa kujenga hoteli kubwa kama zilivyo katika kisiwa cha Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine kuwe na matangazo tufanye matangazo ambayo yatahamasisha watalii tutumie *social media*, *advertisement* kama vipeperushi ili watalii waweze kuja wa kwa wingi katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine nitakalochangia ni sekta ya maji safi na salama humu katika kitabu hichi maelezo yako karibu asimila 83 nimeshafika katika visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba, naipongeza serikali kwa hilo tumebakisha kama asilimia 17 naamini katika kipindi kifupi kinachoja na hizo asilimia 17 zinamalizika na wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba wote watafaidika na kupata maji salama.

Kwa kweli, isipokuwa natoa tahadhari tu kwamba kuna baadhi ya maeneo mfano katika jimbo langu la Mtambwe kuna sehemu tangi la maji liko karibu lakini watu waliopo pale hawapati maji wanapata watu wa mbali maji. Kwa hivyo, Wizara ya Maji na Nishati iweze kuwasimamia watendaji kwamba *once* likitokea *problem* basi wawe rahisi kufika pale mapema, na wenzetu wanavyofanya likitokea tatizo sehemu fulani Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba wanawahi ku-*solve* lile tatizo haiwezekani kama binadamu anakaa wiki nzima hajapata maji.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye suala la umeme naamini nalo limepiga hatua kubwa kwa hotuba ambazo tumezisikia katika vipindi vya nyuma liko katibu asilimia 78, lakini kuna maeneo bado umeme haujafika katika jimbo langu la Mtambwe naishukuru serikali kwamba sasa hivi imeshalipa wananchi fidia na baada ya kufuatilia suala hili kwa Meneja wa *ZECO* nimeambiwa jana kwamba tayari wanaanza kuchimba mashimo kwa ajili ya kupeleka umeme. Kwa hivyo, naamini katika kipindi kifupi majimbo mengi ya Unguja na Pemba yatakuwa yamepata umeme na hayo ndiyo ambayo maendeleo tunayotataka, tumefahamiana waheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la miundombinu barabara ya Mji Mkongwe/Chake/Wete barabara hii ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kisiwa cha Pemba na niliona kama barabara ilitengenezwa barabara ambayo kutoka meli 5 kwenda Konde na kwenda Wete, barabara ile ilikuwa katika hali nzuri, kwa hivyo mara nyengine serikali iangalie kama barabara hii iko kwenye hali nzuri iangalie ile barabara ambayo iko katika hali mbaya, tusijikite kutengeneza barabara ambayo bado iko vizuri. Kwa hiyo, waelekee kwenye barabara ambazo ziko katika hali mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nitakalozungumza ni suala la amani imeelezwa katika kitabu hichi. Suala la amani kwanza nampongeza Mhe. Rais pamoja na wasaidizi wake wote wawili kwa kutoa taaluma ya hali ya juu kuwaelekeza wananchi kwamba sasa hivi tumo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa hivyo tunatakiwa tujikite zaidi kwenye maendeleo, hata Mhe. Rais tunamuona anapita katika misikiti mbali mbali sasa hivi leo namsikia amesali Malindi, kesho amesali msikiti wa Kikwajuni, kesho Wawi, kesho Wete.

Kwa hivyo, nikuonesha kwamba Mhe. Rais wetu amejitoa kwenye maeneo tofauti na watu, kwa hivyo tofauti na zamani unamkuta Mhe. Rais anachagua msikiti mmoja tu huo huo, lakini Mhe. Rais anajiamini anatembea popote kifua mbele. Kwa hivyo ni faraja kubwa kwetu sisi na hiyo ndiyo Serikali ya Umoja wa Kitaifa unayotaka na hayo ndiyo ni maridhiano ambayo tunayataka. Jana tu ilikuwa ni mfano mmoja hapa palipigwa kura na vyama tofauti lakini baada ya kuangalia Mhe. Mwenyekiti kura zile zote zilikuwa *hundred percent* unakuta sabini na mbili, sabini na

mbili hii ni kuonesha kwamba tumeshikamana tunayasahau yale ya nyuma yaliokwisha pita tunakwenda mbele ili nchi hii iweze kunufaika na watu waweze kupata kazi na ajira kwa sababu watu wataanza kukaa vijiweni sasa hivi leo mtu ana *degree* anakaa kijiweni anacheza *draft*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi sina zaidi na naipongeza hotuba hii naikubali kwa asilimia mia moja Mwenyezi Mungu atasadie atufikishe ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti,** ahsante Mhe. Habibu Ali Mohamed kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Aza January Joseph atafuatiwa na Dkt. Saada Mkuya Salum na Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) ajiandae.

**Mhe. Aza January Joseph:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wetu lakini naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikaamka nikiwa mzima na kuweza kufika katika majukumu haya.

Mhe. Mwenyekiti, na pia naomba baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake alioufanya wa kutupatia mawaziri wetu pamoja na viongozi wake wote ambao amewateua naamini kwamba watakuwa wanashirikiana naye kwa hali na mali katika uongozi huu. Sambamba na hilo Mhe. Rais wetu ameanza kwa kasi kubwa ya awamu ya nane ambayo inaonekana kwamba inaleta mapinduzi ya kimaendeleo zaidi nimpongeze sana Mhe. Rais wetu na niombe tumuombee Mwenyezi Mungu ili aweze kumpa kuweza kufikia lengo lile ambalo sote tumekusudia tukiwa tunashirikiana na yeye.

Baada ya hayo, naomba nichangie katika hotuba hii ambayo imejotosheleza katika fani zote na naikubali kabisa kwamba inatupa muongozo mzuri katika kazi zetu hizi za kufanya kwani sote tumekuja hapa kwa lengo ambalo limetuleta la kuendeleza nchi yetu na kushirikiana na Mhe. Rais katika kuleta maendeleo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu naomba nizungumzie kuhusu Sekta ya Utalii ambayo naona kwamba katika kisiwa chetu sekta hii ya utalii ni muhimili moja wapo ambao uko katika uchumi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sekta hii ipo katika uchumi wetu tuwaombe wawekezaji katika utalii wawe na *hospitality* ya wageni wetu wanaokuja katika kisiwa, hii itatusaidia kutuletea wageni zaidi na tutaweza kuzalisha zaidi katika hii Sekta yetu ya Utalii. Lakini pia nikuwa naomba tuangalie hawa wageni wanaokuja wanakuja kivipi, wageni wanatoka katika nchi zao wanakuja kwetu kwa ajili ya kuja kuona vivutio vyetu vya Kizanzibari na wakishafikia katika kisiwa nakumbuka katika miaka ya nyuma kulikuwa na utamaduni kwamba wageni wanapokuja wakifika Zanzibar wakiangalia ile mandhari ya Wazanzibari walivyokaa basi, mtu alikuwa anaweza kujua kabisa kwamba nimefika eneo jengine.

Wageni walikuwa wakiingia Zanzibar basi kama mtu amekuja kichwa wazi akifika bila kuambia alikuwa anastuka kutoka na ile mandhani yetu wenyewe tulivyokuwa tumejiweka. Sasa niombe tu katika sekta hii pamoja na ukarimu wetu ambao tutaonesha kwa wale wageni wanaokuja

tunategemea kwamba wanatuletea uchumi na tunaboresha uchumi wetu, lakini tuwe waangalifu sana wasije wakawa kwamba wanatuvuta sisi kuwafuata zaidi tamaduni zao wao, sisi tuweze kufanya tamaduni zetu za kiafrika na wao wakifika huku kwetu waweze kufutiwa na zile tamaduni zetu ili tuweze kufuata yale ya nyuma ambayo wageni walikuwa wakifika basi unamkuta hata kama ametoka nchi nyengine za ulaya akifika anatamani na yeye kujifunika kama tunavyojifunika sisi ile inaonesha kwamba ni kiasi gani Wazanzibari tulivyokuwa kwamba tuko tunadumisha sana uafrika wetu.

Lakini pia ile inawachangia zaidi wale wasiathiri jamii zetu kwa sababu watalii wanakuja na mila zao wanafika huku ikiwa hatujawaa-*tend* vizuri, basi tunaweza tukajikuta kwamba tunaharibikiwa na kuiga yale ya kwao tukaacha ya kwetu. Kwa hivyo, hapa niombe jamani tuweze kuielimishe jamii kwamba wageni tuwapokee kama wageni na sisi tuendelee kudumisha zaidi mila na desturi zetu za kiafrika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo naomba niingie kwenye Sekta ya Kilimo ambayo pia tunaona kwenye tamaduni zetu za Kizanzibari kilimo kinamgusa kila mwananchi, inaigusa jamii yote ya Kizanzibari hata kama mtu ni muajiriwa kama mfanyakazi lakini bado atakuwa anashughulika kwenye kilimo. Sasa Sekta hii nimuombe tu Waziri wa Kilimo aweze kuitolea elimu zaidi kwa wale watu wa chini jamii ambayo wao wako kwenye kilimo ambacho wanalima bila mitaji na pia bila elimu ya kujua kwamba watumie vipi kilimo kile ili waweze kunufaika.

Kwa kweli, wananchi tulionao ni kwamba tunajikita kwenye ulimaji wa mboga mboga lakini pia tuna kilimo chengine kama cha mpungu pamoja na mihogo, ikiwa watapata elimu nahisi kwamba elimu hii itazidi kuwaelimisha na kilimo kitakuwa kinaleta tija zaidi, kwani wananchi wengi wa chini wanatumia zaidi kilimo katika kujipatia mahitaji yao ya kila siku. Niombe basi Wizara ya Kilimo pia iweze kuhakikisha kwamba ile miradi ya umwagiliaji ambayo ipo katika sekta ile iweze kutimizwa kwa wakati ili wananchi waweze kunufaika zaidi.

Baada ya hayo machache kwenye hotuba hii, naomba tu niuunge mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ambayo imejitosheleza kwa pande zote, ahsante naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana nakushukuru sana Mhe. Aza Januar Joseph kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum atafuatiwa na Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) na Mhe. Hassan Hamad Omar wa Jimbo la Kojani na yeye ajiandae.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati akizindua Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata faraja kubwa kuona kwamba hoja ambayo niliitoa tarehe 11 Novemba, 2020 kwamba tujadili hotuba hii *Golden Speech* ilipata *support* ya wajumbe wote tulikuwemo humu ndani, na faraja kubwa inakuja wakati tunajadili sasa hoja hii ni kwamba uongozi wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi unatimiza siku mia moja *so we had golden speech* lakini vile vile *we are having a golden hundred days* ambazo kusema ukweli *framework* ambayo aliitoa ya serikali yake katika kipindi cha miaka mitano tumeanza kuiona katika siku zake mia moja ambazo ameongoza Zanzibar. Tunampongeza sana kwa muono wake lakini muono wake huo

umekwenda sambamba na kuteuwa viongozi ambao watamsaidia katika harakati za mapinduzi ya kiuchumi kwa Zanzibar. *(Makofi)*

Nampongeza sana kwa kumteuwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, nampongeza kwa kumteuwa Mhe. Hemed Suleiman Abdalla kwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais, nampongeza vile vile kumteuwa *Engineer* Zenna Ahmed Said kuwa Katibu Mkuu Kiongozi pamoja na viongozi wengine na hii inakwenda saambamba vile vile na ahadi aliyoitoa kwamba wanawake aatawaka kipaumbele katika uongozi wake kwa sababu anajua wanawake ni waaminifu, wanawake ni wachapa kazi, lakini vile vile wanaweza kuleta matumaini makubwa kwa jamii tunayoiongoza tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa maeneo sijui machache lakini tutakwenda yakuchangia pamoja na jitihada kubwa ambayo imeonekana pamoja na *framework* hii nzuri ambayo Mhe. Rais ameitoa. Mhe. Rais ana *dream* kubwa kwa Zanzibar sasa *dream* hii amewapa kazi watendaji wai-*realise* pamoja na yeye na sisi tukiwepo katika lile jopo la viongozi tuko pamoja naye katika kutengeneza Zanzibar ambayo tulikuwa tukiiota siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, naanzia na suala la elimu ni suala la msingi sana na nasema kwamba ukitaka kuharibu taifa basi haribu elimu. Kwa kweli, jitihada zimeendelea kuonekana kwa upande *infrastructure* tunaona majengo mazuri ile ni *hard infrastructure*, sasa tunataka *soft infrastructure*, ili kuona kwamba tunafika kule ambapo Zanzibar tuataka kufika. Katika hatua hii nampongeza sana Mhe. Rais kwa mkutano wake ambao wamefanya na wadau wa elimu na amewapa fursa kabisa ya kutoa kile ambacho wanakiona malalamiko, changamoto lakini wamepata fursa vile vile ya kutoa maoni yao jinsi tunakavyokuwa tunakwenda huko mbele.

Tunaomba sasa katika mukhtaza huu Mhe. Rais awe anaendelea mufanya mikutano ile kila mara kwa sababu mabadiliko yanatokea kila siku hatuko *static*. Kwa hivyo, awe anafanya mikutano na wadau hii inakwenda sambamba na mkutano aliofanya na wadau wa afya, awe kila mara anaifanya ile mikutano ili wapate fursa wadau kutoa maoni yao jinsi gani tunaweza ku-*archive objective* zetu na hii inadhihirisha wazi kwamba sasa Mhe. Rais ameichukuwa serikali inaongozwa na wananchi wenyewe, kwa maana yale ambayo wananchi wanayatoa ndiyo yale ambayo yeye anayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili tunaomba sasa sera pamoja na sheria zinazoongoza elimu ziangaliwe upya ili ziendane na uhitaji wetu wa sasa hivi na uhitaji wetu wa baadaye, hakuna mtu anayependezewa siku matokeo yakiwa yanatoka tukiangalia skuli za Zanzibar hususan skuli za *public* skuli za serikali kuanzia wanafunzi mia moja ndio wanapata *division zero* au *division four*. Lakini skuli za *private* utaona sasa kwa sababu kwanza wako kidogo, lakini vile vile utaiona jinsi gani wao wenyewe wanavyo ji-*access performance* zao wana-*performance* vizuri.

Kwa hivyo, lazima tukubadi kwamba skuli zetu za serikali vyovyote zilivyo ziangaliwe upya ili kuona kwamba tunakwenda tunakuwa na *graduates* ama tunakuwa na wanafunzi ambao wanaingia katika vyuo vikuu, wanaingia katika soko la ajira lakini wakiwa na *competence*. Skuli za serikali bado hazifanyi vizuri katika mitihani ya kidato cha nne, katika mitihani ya kidato cha sita hilo lisemwe na tuone sera pamoja na sheria ambazo zinaangalia elimu ziwe zinaangaliwa upya.

Lakini hili liende sambamba na kuweza kuwatizama walimu wenyewe ambao ndio wanaosomesha *in terms of* mazingira yao wanayosomesha, *in terms of* maslahi yao mengine yaangaliwe kwa sababu elimu ndio msingi wa uchumi wowote katika dunia hii, hilo lilikuwa kwenye suala la elimu.

Sasa tuangalie *social* sekta nyengine ya afya. Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la afya ni suala pana sana, lakini kwetu ukizungumzia afya unaangalia mlolongo mzima wa utoaji wa huduma za afya. Tukirudi chini zaidi tuangalie hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, nampongeza sana, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ziara zake, kwa mabadiliko yake ambayo ameyafanya tume-*realize* kwamba ile Mnazi Mmoja ambayo leo waheshimiwa mkipita Mnazi Mmoja, sio Mnazi Mmoja ile iliyokuwa ikisemwa siku za nyuma. Imebadilika madaktari wako pale, wako katika *places* zao kila mtu na beji yake ukienda unamjua huyu daktari nani. Sasa hivi ukienda huna haja sijui ya kubeba buku lako kila kitu kiko in *place*, changamoto zipo *in terms* upatikanaji wa madawa yote kwa wakati mmoja. Vile vile *infrastructure* kwa sababu wengine wanakaa katika sehemu ambazo zina joto kali na watoa huduma kwa wananchi na wengine bado utakuta kwamba kuna vifaa havijaongezeka pale.

Kwa hiyo, katika hili serikali iangalie namna gani tunaweza kuongeza uwezo wa hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ambayo ndio inahudumia wananchi wengi zaidi. Mhe. Mwenyekiti, kimbilio la wananchi wa Zanzibar kwenye masuala ya matibabu ni hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kwa upande wa Unguja. Tunapongeza sana Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika kipindi hiki tu cha miezi mitatu basi alivyokuwa anakwenda *sociological approach* ameleta mabadiliko makubwa katika huduma za afya pale hospitali ya Mnazi Mmoja. Kilichobakia ni kuangalia jinsi gani tunaweza sasa tukaboresha haya mambo mengine, ili madaktari na wafanyakazi wanaotoa huduma pale Mnazi Mmoja na wao waweze kutoa huduma vizuri. Pia na wao waangaliwe maslahi yao, vile vile waangaliwe mazingira yao ambayo wana-*operate* kwa ajili ya kutoa huduma hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Rais katika ndoto yake ya kuifanya Zanzibar ameangalia kwa upana zaidi fursa ama *roll* ya mashirika yetu ya umma katika *contribution* ya uchumi wetu wa Zanzibar. Lakini hili pamoja na mambo mengine yaliyofanyika, pamoja na maboresho yaliyofanyika katika taasisi zetu hususan haya mashirika ni kwamba bado kuna changamoto. Nichukue taasisi moja kwa mfano *PBZ*, katika eneo ambalo tuna *competition* kubwa ni kwenye masuala ya kutoa huduma za fedha.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda *PBZ* leo V/S nenda katika benki nyengine za *private* utatamani kulia. Ukienda *PBZ* leo nenda tu kipindi tu cha mshahara au nenda kipindi ambacho pensheni inatolewa utatamani kulia. Wazee wetu wako pale jasho linawatoka, wako kwenye foleni wamejaa mpaka nje, utaambiwa aah hawataki kutumia *ATM*, wengine hawataki kutumia *ATM* nyinyi benki mpo, lakini kuhudumia wale wateja wanaokwenda pale ni mtihani mkubwa sana *PBZ*. Utakuta watu wamepanga *line* hivi lakini zile *stalls* zinakuwa saba *PBZ* unaweza ukakuta moja, na hiyo moja *I'm real sorry to say about this* lakini inaumiza hata kumuona tu dada hivi yupo kashughulika hivi kidogo kidogo, yaani hebu twende tuingie katika *cooperate culture* kama wenzetu wa *private* wanavyofanya, kwa sababu hizi ni taasisi za serikali na ni taasisi ambazo tunatarajia zitengeneze faida, lakini taasisi ambazo tunataka ziwe ndio mstari wa mbele katika huduma bora.

Mhe. Mwenyekiti, lakini taasisi ambazo tunataka ziwe ndio mstari wa mbele katika kutoa huduma bora. Lakini *PBZ* sijui hawaoni hizi *opportunities* miaka mitano tu nyuma kulikuwa kuna benki labda nne au tano *to day as you speak* kuna *banks* lukuki, kwa sababu wanaona *opportunity* ya kutengeneza faida hapa Zanzibar kwa kutoa huduma bora. Sasa linakuwa ni kimbilio. *PBZ* wame-*relax* kwa sababu kuna *transaction* za serikali zinapita hawatoki, huwaoni wakifanya *aggressive marketing* kwa watu kwenda *PBZ*. Asubuhi tu unasikia yule atakukopa mpaka nywele yaani *we just here that* hatuwaoni wakifanya *aggressive marketing* kama *banks* nyengine wanazifanya.

Kwa hiyo, tunaona kwamba mashirika kama yale ya serikali yame-*relax* sasa unashangaa haya mashirika kwani yameundwa nini si tungeweka tu idara ikawa inatoa huduma, yaani wanafanya kazi kama idara. Kwa hiyo, kuna maboresho makubwa sana yanahitajika kwa ajili ya ku-*realize dream* ya Mhe. Rais anayotaka tufikie katika kipindi cha miaka mitano.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine suala la *private sector*, Mhe. Rais anajua kabisa *private sector* ndio *engine of growth*, *private sector* ndio kitivo ambacho kitatoa ajira nyingi kwa sasa uchumi wetu ulivyo *public sector* ndio imebeba wafanyakazi wengi kuliko *private sector*. Mhe. Mwenyekiti, kwenye hili *private sector* ambayo ipo ambapo vijana wamejikita katika kwenda kutafuta ajira, na wanafanyakazi Mhe. Mwenyekiti bado serikali haijaangalia mazingira ya vijana wanaofanya kazi katika *private sector* nyengine.

Kwa kweli, katika hatua hii naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Waziri wa Kazi, kuna changamoto ilitokea katika Kampuni ya *ZAT* pale *Airport* kwa wafanyakazi. Wamekwenda na kutuliza ile hali lakini hususan Mhe. Waziri wa Kazi changamoto yao ya maslahi ambayo aliahidi ataitatua tunamuomba itatue haraka kabla mambo hayajaharibika zaidi. Hili linakwenda sambamba kuhakikisha kwamba sekta zote ambapo kuna wawekezaji binafsi, serikali iangalie mazingira ya watu wetu ya vijana wetu wanaofanya kazi katika maeneo yale kuona wanakwenda katika mazingira bora. Inawezekana ikawa sio mshahara lakini hata *treatment* ya vijana wetu iwe bora. Tunaomba lichukuliwe hili lifanyiwe kazi kuna maeneo mengine unyanyasaji umezidi...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa malizia dakika mbili.

**Mhe. Saada Mkuya Salum:** Namalizia dakika mbili mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye eneo jengine ni suala zima la uwezeshaji, Mhe. Waziri leo umejibu maswali vizuri. Suala la uwezeshaji si tu linachukuliwa na serikali lakini sasa hivi naiomba serikali, sasa hivi uchumi wetu umekuwa *pa capital DGP* ni *thousand one hundred and fourteen dollars per year per capital*. Lakini *opportunity* kama hii sio tu inachukuliwa na serikali kuona inafanya *investment* zaidi, wenzetu wasio waaminifu wanachukua *opportunity* hii ya kwamba Wazanzibari wanazo fedha na hawana vya kuzifanya na wanatengeneza makampuni ambayo yana-*operate* Zanzibar bila ya kuwa na leseni. Kampuni za ukopeshaji hatuelewi wanakopesha nini wananchi na hili ni bomu, wananchi wanakwenda kuekeza katika kampuni ambazo kwanza zinafanya kazi Zanzibar bila ya kufuata sheria. Kampuni hizi zinafanya biashara za fedha ambazo hawana kibali cha Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa hiyo, wananchi wanaamini kwamba fedha zao ziko salama lakini hazipo salama, nitaomba kama hili halijachukuliwa hatua basi kipindi kijacho tutakuja tutazisema hizi kampuni hapa hadharani, ili labda serikali inaweza ikaenda katika hatua zaidi ya kunusuru mitaji hii ya wananchi midogo ambayo wanaekeza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda na ahsante sana na naunga mkono hoja yetu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Issa Haji Ussi atafuatiwa na Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza hili la Wawakilishi, Baraza la Kumi tarehe 11 Novemba, 2020.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, siha pamoja na mitihani yake midogo midogo imani yangu kwamba sote tutarudi kwake na yeye ataturuzuku yale yenye kheri kwetu.

Kipekee naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana kwa dhati Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi wake mkubwa alioupata katika uchaguzi uliopita. Imani ya Wazanzibari, imani ya Watanzania ni kutuvusha hapa tulipo ili tufike ng'ambu ya pili, ng'ambu ya maendeleo ingawa *destination* ya maendeleo inawezekana ikawa haina tafsiri moja, lakini imani yangu kwamba kile ambacho na yeye atakichanga itakuwa sehemu ya kufanikiwa katika kufika safari kubwa ya maendeleo tuliyoianza rasmi miaka 57 iliyopita baada ya kufanya Mapinduzi matukufu ya 1964. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukiitaza hotuba yenyewe, ukimtizama taswira, matendo na miongozo ambayo amekuwa akiitoa Mhe. Rais bila ya shaka yoyote hotuba hii inakupa kama ni dira, mwongozo na maelekezo tosha kwa upande wa serikali kwenda kufanya maandalizi, mikakati, mipango, miongozo, ili sasa katika kutafsiri hotuba hii tunaamini kwamba mipango ya dhati itakayoletwa na serikali tutaweza kufika kule ambako tunakwenda kwenye kupunguza changamoto za maisha ya Mzanzibari na Mtanzania kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, na katika taswira za uongozi wapo viongozi ambao wana sifa, haiba na uwezo kama ambavyo Mwenyezi Mungu ametujaalia kwa Rais wetu. Wapo viongozi wenye mtazamo na upeo katika kutazama kile ambacho anakiongoza kuweza kufika katika kuisaidia jamii na sehemu anayoiongoza kupunguza changamoto na kuleta shufaa.

Mhe. Mwenyekiti, ukitazama kwenye hotuba namna ambavyo Mhe. Rais ameeleza katika kupunguza changamoto za maisha hasa kwa Wazanzibari, imani yangu kwamba sekta husika, wizara husika wakati ukifika wakija wakitafsiri haya kwa vitendo bila ya shaka changamoto nyingi sana zitapungua. Lakini yeye mwenyewe Mhe. Rais amesema haya yote ambayo

anayafanya, anayatenda anayafanya hayo na kuyatenda hayo ikiwa ni sehemu ya kutafsiri kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa mfano, ukisoma kwenye ukurasa wa 7 ndipo ambapo yeye mwenyewe Mhe. Rais ameeleza hayo bayana kwamba atakayoyatenda yote haya mazuri itakuwa ni sehemu ya kutafsiri kwa vitendo mkataba wa Chama cha Mapinduzi na wananchi waliomchagua. Imani yetu, wito wangu, maombi yangu kwa viongozi na wawakilishi wenzangu pamoja na Wazanzibari wote kwa jumla tuendelee kumpa shime kushirikiana nae, kushirikiana na serikali ili tuweze kutimiza na kumpa nafasi ili uchaguzi ujao chama chetu kiweze kushinda vizuri zaidi na kiendelee kushika hatamu ya kuongoza dola. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Rais amesema maneno mengi sana, lakini kwenye ukurasa wa 8 na wa 9 amesema mambo mahsusi ambayo yanatuhusu sisi *generation* yetu kwa maana ya kwamba amejitolea mfano yeye mwenyewe akiwa ni Rais ambaye amekuja *post revolution* pamoja na jamii kubwa ya viongozi naamini hata tuliomo humu wengi tumezaliwa *post revolution.* Yeye ameomba amesihi na kutaka kwamba sasa ni wakati rasmi wa kunufaika na matunda ya Mapinduzi na Muungano kiuchumi na kubadilisha hali zetu isiwe tu simulizi. Mhe. Mwenyekiti, ili sasa tufikie hapo kuona kwamba matunda ya Mapinduzi na Muungano tunanufaika nayo ndio maelekezo na dira ambayo ameitoa Mhe. Rais ili sasa serikali iende ikatafsiri na jamii tushirikiane nayo tuweze kufikia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukitazama kwenye jambo jipya ambalo Mhe. Rais anakuja kulikazia, ili liweze kutekeleza na kuleta tija, jambo la uchumi wa buluu. Hivyo, imani yangu kwamba serikali itajipanga na jamii na wananchi kwa ujumla tutawaelimisha, ili jambo hili walifahamu vizuri. Jambo hili ni kubwa na jambo hili linahitaji maandalizi marefu na pengine inaweza ikachukua kitambo yapo ambayo yatatupa faida kwa wakati mfupi, yapo ambayo yatatupa faida kwa wakati wa kati na yapo ambayo yatatoa faida kwa wakati mrefu.

Mategemeo yangu kwenye sekta za gesi na mafuta inawezekana ikawa jambo la muda mrefu, lakini kwa upande wa uvuvi nina hakika kwamba ni jambo la muda mfupi linalohitaji *strategies* za kawaida za haraka tukipata *capital* ya kutosha tunaweza tukawanufaisha wananchi wetu kuweza kuvua kwa kuwapa nyenzo utaalamu na vifaa, ili waweze kupata tija kama ambavyo imekusudiwa katika suala zima la uchumi huu wa buluu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika hili la uchumi wa buluu jambo moja niombe tu kuishauri serikali tuna haja ya kutazama kwa jicho la kipekee katika kukuza na kuzipa uwezo taasisi zetu, ili ziweze kuja kuhimili ushindani mkubwa utakaokuja katika makampuni ambayo yatakuja kushiriki kwenye shughuli hizi za uchumi wa buluu na hasa hasa makampuni makubwa yatakayokuja kwenye harakati za uchimbaji wa gesi na mafuta. Wenzetu hawa ni wataalamu wana uwezo mkubwa, wana uzoefu mkubwa lazima taasisi zetu za *ZPDC, ZPRA* lazima tuzijengee uwezo mkubwa ili kuweza kuhimili ushindani, mijadala, miongozo, utaalamu ili tusije tukafika pahali tukawa tumepata neema ya gesi, neema ya mafuta taasisi zetu zikashindwa uwezo wa kusimamia vizuri katika kutafuta tija yenye maslahi mapana kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili Mhe. Rais ambalo amelisema kwenye hotuba yake ni suala la utalii kwa wote. Imani yangu kwamba tayari jambo hili limeanzishwa, limesemwa, limeonekana

kwamba linawezekana likafanyika. Lakini kuna jambo moja nadhani serikali niiombe kuishauri kuna *expert* moja ya *media* nadhani haijatumika vizuri. Suala la utalii kwa wote sijaiona ile *role* ambayo tunaichukua kuipa taasisi au tasnia ya media katika kulifanikisha na kulitangaza jambo hili. Kwa kweli kama hatukulipa msukumo maalum na mtazamo maalum sekta ya *media* nina hakika kwamba jambo hili linaweza lisilete tija ambayo inakusudiwa.

Lakini maoni yangu kama serikali itajipanga vizuri kwa kutumia vyombo vya habari jambo hili litakuwa lenye manufaa na upeo mkubwa. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, imani yangu kwamba matendo ambayo anayafanya ni sehemu ya kutafsiri hili akishirikiana na taasisi nyengine akijipa na *assignment* ya kuvihusisha vyombo vya habari na kuwatengea nguvu maalum katika kufanikisha hili linaweza likaleta tija kubwa ya kufikia malengo ambayo yamekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo nataka kuishauri serikali katika kutimiza azma ambayo Mhe. Rais ameeleza katika hotuba yake nzuri ni suala zima la viwanda. Mhe. Mwenyekiti, ili tuwe na viwanda vingi na vyenye tija nadhani umefika wakati sasa wa kutafuta fursa nzuri ya kuzungumza na wenzetu wa upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sote tunajua kwamba suala la viwanda ni suala la Muungano na kiwanda kinapoanzishwa Zanzibar kionekane sawa sawa na kiwanda ambacho kimeanzishwa upande wa Tanzania Bara, bidhaa ambazo zinazalishwa Zanzibar zionekane sawa sawa na bidhaa ambazo zimezalishwa upande wa Tanzania Bara. Sasa ili hili liende vizuri tunahitaji kuwa na mjadala wa wazi wa kuzungumza kwa upana, kuaminiana, kushauriana na kukubaliana na bila ya kufanya hivyo tutakuwa tunaimba nyimbo ambayo haiwezi kuwa na kiitikio, kwa sababu hatuwezi kuanzisha viwanda kama hatuna masoko na tukitaka tusitake soko la bidhaa liko zaidi upande wa Bara.

Kwa hiyo, ni lazima pafike pahali tutengeneze mjadala mpana wenye maslahi mapana wa kuisaidia jamii yetu, biashara kwa hivi ilivyo itakuwa biashara ya upande wa mmoja na hatuwezi tukawa kama nchi ambayo inategemea sekta ya biashara upande mmoja tuwe wanunuzi, upande uwe unazalisha, haiwezekani. Hili ili liende vizuri unapozungumzia biashara hasa ya viwanda maana yake unazungumzia tatizo kubwa sana la ajira, na huwezi ukatatua tatizo la ajira bila ya kujenga viwanda na ukijenga viwanda maana yake unahitaji wafanyakazi na wafanyakazi wanahitaji maandalizi mazuri ikiwa ni hili ambalo amelieleza Mhe. Rais suala zima la *vocational training*.

Kwa maana hiyo, imani yangu kwamba tukiyatizama haya *as a package* tunaweza tukapata jambo zuri lenye manufaa kwa kujenga uwazi kwamba suala la viwanda lisichukuliwe kwamba kiwanda kinapoanzishwa Zanzibar kama kwamba hakistahiki, jitihada zote ambazo anachukua Mhe. Rais, jitihada ambazo serikali inahangaika nazo katika kutafuta watu wa kuja kuekeza akitokea mtu akihoji nikiekeza Zanzibar soko la upande wa Bara likoje tunashindwa kuwa na majibu.

Kutokana na hali hiyo, majibu lazima yatengenezwe na yawepo majibu sahihi kwamba kiwanda utakapokiwekeza Kahama sifa hizo hizo ni kiwanda ambacho utaweza kukiwekeza Micheweni. Lakini haiwezekani nadhani kuna kipindi hapa tulikuwa tunanunua chaki zinatoka Simiyu lakini nilikwua naona hapa kuna kipindi maziwa yanayozalishwa Fumba kwenda upande wa pili

ilikuwa mgogoro. Sasa hatuwezi kwenda hivyo kama utaratibu uko wazi kwenye Katiba tuaminishane na tukubaliane kiwanda kitakachoanzishwa ng'ambo yoyote ya Muungano kiwe ni sawa sawa katika kupata fursa ya masoko.

Mhe. Mwenyekiti...

**Mhe. Mwenyekiti:** Malizia mheshimiwa.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba nimalizie kwa maneno kama matano tu hivi.

Jengine ambalo nataka kuishauri serikali Mhe. Mwenyekiti ni suala zima la maandalizi mazuri hasa ya viwanda vidogo vidogo kwa maana ya kwamba viwanda vya usarifu wa mwani, bidhaa za mali ghafi na nadhani umefika wakati sasa tuache kusafirisha karafuu kwenda nje. Kwa hiyo, kama serikali lazima tushauriane tutafute mikakati maalum ya kuona kwamba na sisi sasa tunatoa *product* ya karafuu tunaipeleka nje kuingia kwenye soko baada ya kuiongezea thamani. Haiwezekani sisi tuwe tunanunua sigara badala ya kununua tumbaku lakini sisi tunatoa karafuu zinakwenda nje zinatengenezwa sigara halafu sigara ile inarudi kwetu tunanunua kwa thamani kubwa, hapana. Nadhani umefika wakati sasa kujenga uwezo kwa taasisi zetu ili ziwe zina nguvu ya kuweza kuzalisha na kuongezea thamani mazao ambayo tunazalisha.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho niombe tu na niwasihi wajumbe wenzangu kama ilivyo desturi kwamba tuna haja ya kufanya kazi kwa pamoja sote kwa ujumla wetu tuiunge mkono serikali yetu, tumuunge mkono Mhe. Rais, tuwaunge mkono viongozi wetu ili yale ambayo tunatarajia kufikia kwa wananchi wetu tuweze kuyafikia na imani yangu kwamba tukifika pazuri tunaweza tukafanya vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kwa kumalizia naomba niseme kwamba nakubaliana na naiunga mkono kwa dhati kabisa hotuba hii na matumaini yangu kwamba lile ambalo amelisema Mhe. Rais wakati wa kampeni kuwa “Yajayo ni Neema Tupu” ni kweli. Ukitizama dira hii matendo yake na mafanikio ambayo ameyapata katiak siku mia moja bila shaka yanayo ni neema tupu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru sana Mhe. Issa Haji Ussi kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Hamad Omar wa Jimbo la Kojani atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidha na Mhe. Sulubu Kidongo Amour wa Jimbo la Mkwajuni ajiandae.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kunipa fursa hii kuweza kuchangia Hotuba ya Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* aliyetujaalia siku ya leo kuwa na afya njema na hizi ni neema zake Mwenyezi Mungu kwa waja wake hatuna budi kumshukuru kwa kusema *Alhamdulillah*.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa ni dhamira njema, kusema ni kusema maneno na kutenda ni jambo jengine, sisi tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu azma yake hii afanikishe. Hii pia inasababishwa na washauri wazuri ambao amewateuwa akisema Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais Mwenyezi Mungu awajaalie wampe ushauri mwema ili kuelekea huko tunakokusudia. Mheshimiwa ukiangalia katika hotuba ya Rais kwenye salamu tu basi inajitosheleza, ni salamu ya kiungwana na ya kiimani tunashukuru *Alhamdulillah* na tumeipokea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tukienda katika dhamira yake kubwa Mhe. Rais kasema atawaunganisha Wazanzibari bila ya kubagua kwa rangi, jinsia, ukabila na mambo mengine yanayohusiana na hayo na hili tunaliona. Imani yangu kama halipo hilo basi sisi wengine tungekuwa hatumo ndani ya Baraza hili, lakini tunashukuru mwelekeo ni mzuri, nchi *Alhamdulillah* ina utulivu wa kutosha. Sasa hivi kama si hivyo wengine tungekuwa katika ukimbizi tunashukuru nchi inaendelae vizuri, sasa tuliobakia sote tuwe kama wenzetu wa Kenya tufuate nyayo tu za viongozi wetu na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu kwa sababu tumeelewana atatupa mambo mema na tena yenye neema kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tu katika uchumi huu wa buluu umeelekeza sana kwenye viwanda na ni kweli kama alivyosema Mhe. Rais kama bahari hatujaitumia ipasavyo na tukiitumia hii watu wengi watapata ajira na samaki bado Zanzibar hii wapo wengi hawajavuliwa, *In Shaa Allah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu katika kuelekea huko watu wetu wengi watapata ajira. Lakini nisema tu hofu yangu mimi katika mambo ya uchumi wa buluu imesahau wavuvi wadogo wadogo kuwapangia mazingira yaliyo mazuri. Kwa sababu wavuvi wadogo wadogo ni wavuvi asilia lakini ukiangalia wavuvi asilia hawa sheria inawakandamiza sana.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria Nam.7 ya Mwaka 2010 inawakandamiza wavuvi wadogo wadogo na mimi namuomba Mhe. Rais pamoja na waziri kama yupo achukue sheria ile iletwe Barazani tuifanyie marekebisho, inawakandamiza sana na ukiangalia nchi yetu ni ya kisiwa na kama nchi ya kisiwa kila mwakilishi anayesimama hapa anao wavuvi, sio wengi waliokuwa hawana wavuvi na hii inatusaidia sisi hata kwenye serikali, kwa sababu wavuvi hao wanaajiri watu binafsi wengi tu. Ukiangalia watu wanaowaajiri mvuvi mwenyewe katika vyombo vyetu sisi tunavyotumia kuna vyombo vinabeba watu 50 vyengine 60 mpaka 70 wanakwenda baharini, *Alhamdulillah* wanapata riziki zao na siku nyengine kama hali ni ngumu ndio hivyo ndio uvuvi.

Lakini ukiangalia hawa wanakandamizwa sana hawapewi maelekezo ya kutosha kutokana na ile sheria imewabana, leo mvuvi anakwenda baharini atavulia kama hana nyavu, mvuvi anakwenda baharini kwenda kumvua pweza kama hana uchokoo atamvua vipi, samaki utamvua vipi, lakini ukiangalia mimi nasema hawa wavuvi wote wanakwenda kwa wizi tu kutokana na sheria inavyowabana, hivi sasa wanakwenda baharini kama wizi kutokana na sheria na kama haijafanyiwa marekebisho hii basi hali itakuwa sio nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, wavuvi hawa wanaleta tija kwa Zanzibar, ukiangalia wanawake jinsi walivyopata ajira kutokana na wavuvi hawa wadogo wadogo wanajipanga pale Mikunguni, Mwanakwerekwe wanawake wanauza biashara ya samaki leo wavuvi hawa ukiwaondoa na uvuvi wa uchumi wa buluu ambao utakuwa ni wa meli basi hawapati samaki kama hawa, hawataweza kununua samaki wa mbawasi au nduaro, papa au jodari. Haya ni mambo ya kihoteli

sasa tuangalie hii sheria na naomba neno hili lichukuliwe la Sheria Nam. 7 ya Mwaka 2010 iletwe Barazani tuifanyie marekebisho ili kuwapa haiba wavuvi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Rais kazungumza mazuri ya kujitosheleza na *In Shaa Allah* pamoja na ustawi wa jamii uliopo wa afya na mambo mengine, lakini pia aangalie sana na mambo ya chakula. Hawa wananchi wetu watatupenda kwa kupungua bei za vyakula mapembe kila siku yanapanda bei.

Kwa hivyo, na hili Mhe. Rais aliangalie hatuoni kushuka hata mara moja yanapanda tu sijui mambo haya mpaka lini, tunaomba lichukuliwe hili lifanyiwe kazi watafurahi zaidi wananchi wetu ikiwa bei za mapembe zitapungua, tusiangalie hali zetu zilizomo humu ndani ya Baraza tukafikiri na wananchi wetu wako hivyo. Wananchi wetu wana hali duni ya kutosha lazima tuwaangalie, kuna wengine shilingi mia tu hawaimiliki Wallahi Billah, mia hawaimiliki. Sasa wale tuwaangalie na tuwape kipaumbele hawa wafanyabiashara wapunguziwe ushuru na waweze kushusha bei ya vyakula ni jambo zuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, sitakuwa na mengi ya kuzungumza lakini nasisitiza katika sheria hii basi iletwe ije Barazani ili tuifanyie marekebisho. Ahsante sana nashukuru naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante nakushukuru sana Mhe. Hassan Hamad Omar kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidha, atafuatiwa na Mhe. Sulubu Kidongo Amour na Mhe. Bihindi Hamad Khamis ajiandae.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii ya kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji katika hii *golden speech* ya Mhe. Rais aliyoitoa siku aliyokuja kulihutubia Baraza la Kumi la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kwa sote kukutana hapa. Mheshimiwa ni kweli Mhe. Rais alitoa *golden speech* kwa sababu ilikuwa imekusanya mahitaji yote inayohitaji Zanzibar ili Zanzibar ibadilike jina iitwe Zanzibar iliyoendelea au iwe ni miongoni mwa nchi za dunia zilizoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza, kuna msemo naupenda sana kuutumia msemo ambao aliusema Mhe. Hayati Baba Madibou Mandela alisema: *"Poverty is not an accident, the man made".* Hatuwezi kuutoa umasikini kwa kutumia *charity the only way* kuondosha umasikini ni *human action*.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi tunamshukuru kwa kuwa yeye ndiye *Human Action* amekuja kufanya kazi hii kwa vitendo kuutoa umasikini. Tukiangalia *angle* zote katika *angle* ya kisiasa kwa mfano, tumeona aliahidi Mhe. Rais kwamba nitaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kaunda, kamteuwa Maalim Seif Sharif Hamad kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais leo *Alhamdulillah* Maalim Seif Sharif Hamad anafanya kazi vizuri katika kuhakikisha tunaendesha nchi kwa pamoja. Nasikia anaumwa Mwenyezi Mungu ampe shufaa ya uzima, lakini pia tumeona leo tunae hapa Mhe. Nassor Ahmed Mazurui tulikuwanae kule jimboni kwa Mhe. Miyaho Juma Suleiman anamtia kishindo kidogo tukamsaidia. Lakini leo Mhe. Rais kwa upande wa kisiasa ameona Mhe. Nassor Ahmed yumo humu amependeza

amekuwa *very young boy* hata ndevu amechonga vizuri, amependeza. Hii yote ni kuonesha *demonstration* ya kisiasa ya Mhe. Rais kwamba *He is committed* katika kuhakikisha Zanzibar inaendelea kwa mashirikiano. *(Makofi)*

Vile vile tunae ndugu yetu Mhe. Omar Said Shaaban tulikuwa tunamuona katika mitandao ni kijana mwenye kutaka kujua siasa, lakini Mhe. Rais amesema kwa vile ni kijana unataka kujua siasa nenda Baraza la Wawakilishi CCM wakakufundishe siasa. Tunamshukuru amekuja humu sisi CCM tumo tutamfundisha siasa ndugu yetu tunajua ni mwana harakati mzuri wa kutaka kusaidia Zanzibar iendelee. Tunamshukuru Mhe. Rais kwa kuona ni kijana anayefaa kuja kujifunza siasa kupitia Chama cha Mapinduzi tutamfundisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika tumeona jinsi gani Mhe. Rais *commitment* yake ya kutaka kuiona Zanzibar inakwenda mbele kimaendeleo kuitoa hapa ilipo. *Speech* ya Mhe. Rais ukurasa wa nne imezungumzia neno Diaspora tumeliona, Nitataja ushahidi wan chi kama Ghana, India, Ethiopia na nchi nyengine nyingi zimeendelea kwa kuwachukua wale ma-Diaspora wao wananchi wao wanaoishi nje ya nchi kuwaita na kuwashirikisha katika maendeleo ya kwao.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina hazina kubwa nje ya nchi na wataalamu wengi Zanzibar tunawakosa lakini Mhe. Rais kila hotuba yake nilikuwa naisikiliza ameahidi kuwashirikisha na amesema Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wote wanaoishi ndani ya nchi, wanaoishi nje ya nchi na popote walipo na namuahidi Mhe. Rais Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi mimi ndiye *Diaspora in chief* wa Zanzibar namuahidi wako tayari kushirikiana na Zanzibar na Rais kuhakikisha Zanzibar inatoka hapa ilipo inapiga hatua ya kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema jambo moja, ilikuwa ni aibu kwa Zanzibar ati ndio nchi ya Kiswahili kimezaliwa hapa, kimeundwa hapa, lakini elimu ya mwisho tunayoitoa kwa Kiswahili ni elimu ya *Diploma*, ukitaka *Master, Degree, PhD* ukaipate Kenya haya Kenya na Kiswahili wapi na wapi, lakini ndio hivyo. Lakini sisi Idara ya Ushirika wa Kimataifa na Diaspora tukaliona hilo tuna walimu wengi wanasomesha nje ya nchi Marekani, Canada, Swiss, Uingereza tukawaita leo namjua wazi Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aliyestaafu, Mhe. Riziki Pembe Juma anafanya *PhD* ya Kiswahili, wale walimu wote ni walimu wa Diaspora wanaosomesha nje ya nchi na wote ni Wazanzibari leo wamekuja kuifanya Zanzibar kuionesha kwamba kweli ndio chimbuko la Kiswahili, tujue huo ndio umuhimu wa Diaspora.

Mhe. Mwenyekiti, Uchumi wa Buluu. Mheshimiwa ni aibu kwa Zanzibar lakini hotuba ya Mhe. Rais ilimaliza kila kitu. Uchumi wa Buluu hivyo Zanzibar imezungukwa na bahari ukienda Kaskazini, ukienda Kusini, Mashariki, ukienda kote bahari lakini ati samaki tunaokula wa peduu; ukitoka nje hapo Baraza la Wawakilishi wanauza samaki wa peduu *imported fish* si aibu hiyo? Ni aibu ya mwaka, lakini Mhe. Rais ameliona hilo na ameanzisha wizara kabisa ya uchumi wa buluu.

Mhe. Waziri tunakutegemea hatutaki kuona samaki wa peduu, sio uwafungie aa! Isipokuwa washindwe ku-*compete* hiyo ndio *business principle* washindwe ku-*compete* kwa sababu watakuwa samaki wapo hapa *fresh,* wengi wanavuliwa. Mhe. Rais tunamwambia tunataka kuona hivyo wavuvi wetu hawajui hawana utaalamu, wavuvi wetu hawana pesa.

Jana Mhe. Waziri alisema anataka kuwahusisha wavuvi wetu na taasisi za kibenki. Nataka nimwambie asije akaiuwa ile *idea* ya Mhe. Rais, taasisi za kibenki zote duniani jukumu lake ni kuhakikisha kumuibia mwananchi ili wao wawe matajiri, asije akamuhusisha mwananchi mnyonge na taasisi ya kibenki itamuibia, itamtia *stress* mwisho itamuuwa. Kwa sababu itamvizia imchukulie nyumba yake kama mkpo halafu imuue kwa *pressure*.

Mhe. Mwenyekiti, tunakuomba sana muunde utaratibu mzuri ambao tutawasaidia wanyonge waweze kuendelea. Zanzibar ni nchi pekee duniani yenye mwani mzuri, mwingi na mwani huu wote uko baharini. Mheshimiwa tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa kuanzisha Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi naamini Zanzibar baada ya muda mchache ujao itakuwa ni nchi iliyoendelea miongoni mwa nchi zilizoendelea za Kaifrika.

Ukiacha hapo Mheshimiwa nije katika ajira. Mhe. Rais ameahidi ajira laki tatu, mimi nasema kuliko laki tatu zitapatikana kwenye hiyo bahari tu basi kuna uchumi karibu wa laki tatu bado nyengine, huo uchumi wa buluu Mhe. Rais ameliona hilo na lipo na linawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika ujenzi wa bandari. Mhe. Mwenyekiti, kweli Zanzibar tukitumia bandari zetu kama zilivyotiwa saini juzi ajira laki tatu mara mbili zitapatikana na kweli kila mtu ataleta meli hapa kuja kufanya hivi na vile, kwa sababu Zanzibar yenyewe yuko *Author* mmoja wa Afrika ya Kusini alitembelea Zanzibar na alisema hivi: *"The Paradise of Africa and motherland of East Africa is Zanzibar". I do agree with him.*

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa barabara. Ukurasa wa 19 katika hotuba ya Mhe. Rais unazungumzia ujenzi wa barabara. Ni kweli Mheshimiwa tusiseme uongo Mkoa wa Magharibi kuna watu wengi asilimia karibu 75 ya Wazanzibari wanaoishi Mkoa wa Magharibi hakuna barabara, lakini Mhe. Rais masikini kaliona na akaahidi kwamba barabara ya Makufuli - Munduli ataijenga na leo Mhe. Waziri kasema ataijenga bajeti hii. Mhe. Waziri nataka nimwambie tu *hansard* nimeshakwenda kuichukua kwa sababu wananchi wangu wa Welezo wanasikia nasubiri. Namshukuru kwa kuwa muungwana amesema wazi wazi kwamba bajeti hii ataijenga tutashirikiana na Mhe. Waziri kuijenga ile barabara ili wanacnhi wa kule waweze kuishi vizuri kwa sababu najua ni Mwana Mapinduzi na yuko tayari kuendeleza mbele Mapinduzi haya Matukufu kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika nikitoka hapo kuna mipango miji. Mahatma Ghandi alisema: "Nchi yoyote haiwezi kuendelea bila ya kuwa na *better uses of land*", lakini Mhe. Rais ameiona na ameizungumza katika *speech* yake kwamba umefika wakati.

Juzi nilisema Kwahani iliojengwa na Ukoloni nzuri kuliko Mwera ya Mhe. Mihayo Juma Suleiman iliyojengwa juzi na inaendelea kujengwa, watu wamejenga vibaya hakuna njia ya kupita *fire*, hakuna njia ya kupita *ambulance*, hakuna njia haya ya kupita vespa. Halafu chengine kibaya Mwera, Welezo, Fuoni ni *fertile land* bado tunaitumia kwa ujenzi majenzi yenyewe holela. Lakini Mhe. Rais kwenye *golden speech* yake ameliona na amesema ataweka mipango miji imara.

Mhe. Riziki Juma Pembe yeye ndie anayesimamia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi nimwambie bwana nchi yoyote duniani ili iendelee lazima iwe na mipango mizuri ya ardhi, leo

Zanzibar mtu anaamka asubuhi kapata pencheni anajenga, unajenga nchi yako hii walioipindua wenyewe hawajengi namna hiyo, unajenga tu wewe umepata pesa hizo pesa kakujaalia Mungu hujatafuta kibali kwa sheha, hujatafuta kibali wilayani, unakwenda kujenga tu mheshimiwa haiwezekani jambo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, hii nchi itakwisha pa kuzikiwa tutakuwa hatuna lazima tuwe na mipango mizuri ya kujenga matumizi ya ardhi Zanzibar tutashindwa kuzikwa ma kwetu tukatiwe baharini mheshimiwa, jukumu hilo unalo wewe.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Afya. Nchi yoyote duniani isiyo na *better health service* ni hatari kwa sababu binadamu ukiumwa tu unaona ehee kaburi hiloo na hakuna mtu anayetaka kufa mapema. Mheshimiwa tunahitaji *better health of service*. Lakini Mhe. Rais kwenye hotuba yake kasema wazi wasi kwamba Zanzibar haina *diagnosis centre* sijui kwa Kiswahili zinaitwaje zile, kweli. Pale Mnazi Mmoja Rais wa Serikali ya Awamu ya Saba kajitahidi sana lakini palikuwa bado mimi nilisema sana mpaka nikadata mdomo, lakini nasema tena leo namshukuru sana Mhe. Rais leo hii pale Mnazi Mmoja unakwenda unapewa damu yako katika *gloves* vile vidole vya *gloves* unaambiwa ukapime Kilimani, ukifika Kilimani unaambiwa hiki kipimo shilingi laki tatu hivyo mimi mtu wa shamba kwetu Mchangani shilingi laki tatu nazipata wapi, hata nikauze dume la ng'ombe si nishakufa?

Chengine zile za kupimia za kuangalia mionzi *ultra-sound* zinafunguliwa saa tatu ya asubuhi tu kama kwamba umesema usiku Mungu hayupo kakwambia nani. Lakini Mhe. Rais kaliona hilo na kalizungumza. Tumeweza kuona Hospitali ya Mnazi Mmoja imeanza kubadilika lakini usafi pia tumeanza kuona kumebadilika Mnazi Mmoja, namuombea sana dua Mhe. Rais aendelee na uzi huu huu Zanzibar sasa itakuwa kweli ni *Paradise of Africa* na *Motherland of East Africa*.

Kwenye kilimo Mhe. Rais amezungumza vizuri sana suala la kilimo na kaka yangu wa kilimo kule amesema sasa tutalima kwa kutumia zana bora, zana za kileo ili Zanzibar yetu sasa kuna baadhi ya vitu tuache kuagiza tuzalishe wenyewe. Hivyo leo ndizi ikatoke Bara inahusu nini wakati ardhi tunayo.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwa kasi hii aliyoanza nayo huku Mhe. Rais ya kutaka maendeleo, mashirikiano tumeona hata ndugu zetu, na naamini ndugu zetu hawa wa chama cha upinzani wamekuja humu kuhakikisha kuja kushirikiana katika kumsaidia Mhe. Rais na sio kuleta upinzani usio na maana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nakushukuru sana, namshukuru sana Mhe. Rais, nawashukuru Wazanzibari lakini mwisho na mwanzo naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua mimi Hassan Khamis Hafidh (*Diaspora*) kuwa mwakilishi wao. Tulikuwa 19 lakini nilishinda mimi nawashukuru sana, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Mheshimiwa nakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, nakushukuru Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Sulubu Kidongo Amour atafuatiwa na Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Shaib Hassan Kaduara ajiandae.

**Mhe. Sulubu Kidongo Amour:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii lakini pia naishukuru sana hotuba ya Mhe. Rais. Hotuba hii iko na kila kitu, imefanikisha kila kitu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuzungumza mambo mengi, lakini nataka kuingia katika mwelekeo wa usimamizi wa mawizara yetu ya serikali. Hotuba hii imezungumza zaidi wizara hii, na wizara ziko hapa tunazo ndani ya Baraza la Wawakilishi, na maana ya kuwa ndani ya majimbo yetu hakuna umasikini kuna ufukara.

Kwa hiyo, Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo anatakiwa aende chini akafatilie kilimo ili tuondoe ule ufukara tulionao. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi aende pale *custom* akaangalie kuna tatizo gani. Pale *custom* ukinunua gari ikilala siku moja tu kunaibiwa kila kitu, hii ni kazi ya waziri akasafishe pale.

Wizara ya Maji na Nishati kidogo nashukuru Mhe. Waziri anafatilia kule ndani ya jimbo langu amekuja kunisafishia wadi moja bado wadi moja. Lakini hiyo wadi moja nashukuru kwa sababu wadi ya Kidombo maji yalikuwa hayapatikani na kulikuwa na Waziri Mstaafu kule, muda wowote zaidi ya miaka 10 hakuna maji lile tangi la maji lilitolewa, lakini kaja katengeneza sasa hivi watu wanapata maji. Sasa waziri ndio iliokizungumza hichi kitabu Mhe. Rais kazungumza kitabu hichi kuwaambia mawaziri waje kwenye ufukara.

Mhe. Waziri wa Afya haidhuru kuna mmoja kasifu sana sasa hivi, mahospitali dawa zipo, na madaktari wanafanya kazi vizuri lakini ikifika tarehe 15 kwa sababu bado kuna maduka ya madawa kwa hiyo, ikifika tarehe 15 hizo dawa hazipo. Waziri unatakiwa ufatilie kule na ndio maana ya hichi kitabu, Mhe. Rais kazungumza humu vitu vingi sana, lakini vitu hivi vyote vinatakiwa vifatiliwe tusikae maofisini hatutokifanyia kazi hichi kitabu. Tukae asubuhi lakini ikifika saa 6 ahakikishe anakwenda kwenye *site* hapo ndipo tutakuwa tunakifanyia kazi hichi kitabu.

Samahani kidogo maana kuna kila kitu humu ndani ya kitabu chetu. Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Waziri, mimi nimebahatika ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC* nimetembea baadhi ya Majimbo nimeona vile pesa ambazo zimehujumiwa baadhi yao, lakini nyengine zimekwenda vizuri, na nina hakikisha kama ingekuwa waziri anafatilia moja kwa moja basi pesa zile zingekwenda vizuri hususan kule Pemba, pesa tunakwenda tunambiwa kumejengwa choo, hicho choo chenyewe tunakwenda pale hakuna. Kwa sababu hakuna usimamizi mzuri.

Sasa mimi naomba Mhe. Waziri aliposimama hapa akahutubia hotuba yake hii, kazungumza kitu kizuri na kamaliza kila kitu bado sisi, kazi yetu sisi sasa hivi ni kufanya kazi chini ili kuifanyia kazi hii hotuba. Mhe. Rais ni mzuri kwa kauli yake na moyo wake ndani na ndio maana kafanya yote sasa hivi hapa, siku mia moja tunakwenda vizuri sana. Lakini hatutofanya kazi vizuri Kama hatukusimamia hichi kitabu vizuri kwa kina hatujamfanyia haki.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri tunakuombeni njooni chini kule ndio kwenye ufukara, mvuvi anaweza akaenda siku tatu hajapata samaki hata siku moja lakini mnatwambia kutakuja uvuvi ambao sasa hivi samaki yaani utakao kuwa unakuja na samaki wengi zaidi. Mimi nasema bado

sio kweli kwanza njooni chini muangalie watu mafukara wanavua vipi, halafu tufanye hiyo kazi nyengine.

Hakuna kitu kule mimi mtu wa pwani, mtu anakwenda baharini siku tatu hana kitu, kuna ufukara tu nafasi hizi ambazo tunazo sisi kama wawakilishi mtu ndio angalau anakuja “Oh! Bwana mimi leo ya tatu kwangu hakuna, kitu” sasa naomba sana ili tuifanyie kazi hotuba hii mawaziri mje chini kwa kunako mafukara. Mje kwa wananchi huyu ananishughulisha, njooni kwa wananchi msije chini. Mawaziri njooni kwa wananchi. (*Makofi/Vicheko*)

Lakini pia la mwisho, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mimi binafsi Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni nakulika kwenye jimbo langu uje uzunguzme na Vyama vya Ushirika vya akinamama nimeona kuna hali sio ya kuzunguza Barazani. Lakini nakuomba kwa hisani yako nakuomba, nakuomba, nakuomba, utapanga wewe mwenyewe nikusanye vikundi vyangu uje uvione halafu hapo ndio nitasema maneno ambayo yako pale. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Naunga mkono hoja kwa nguvu zote. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, uliyekaa naye anakushughulisha mpaka unasahau kuunga mkono hoja. Nakushukuru Mhe. Mwakilishi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Bihindi Hamad Khamis atafuatiwa na Mhe. Shaib Hassan Kaduara na Mhe. Yahya Rashid Abdulla ajiandae kama muda utaturuhusu.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake hii ambayo ina mwelekeo wa Zanzibar pamoja na wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais kwa uteuzi wake, pia niwapongeze wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunipigia kura na nikaingia kwenye Baraza la Wawakilishi ili niwatetee wananchi wale wanawake ili kuleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hotuba hii ina nyanja nyingi sana na imeeleza vya kutosha na waheshimiwa wengi wameshaifafanua, kwa upande wangu naomba nielekee kwenye kilimo. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba Ilani ya Uchaguzi imeelekeza kwenye kilimo na tunajua kuwa kipindi kilichopita ilielekeza mabonde mengi ambayo yanataka kufanyiwa *irrigation*.

Naomba niende kwenye bonde la Makwararani, kweli kwenye Ilani ya Uchaguzi awamu zote bonde hili limo naiomba serikali. Kwa sababu bonde hili lilifanyiwa *irrigation* tangu mwaka 1979, mioundombinu yake ipo. Naiomba serikali pamoja na wizara ili iweze kusimamia bonde hili ili ile *irrigation* iendelee vizuri na wananchi ambao wanaishi kwenye Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea mbele niende kwenye utalii kwa wote. Tunajua utalii kwa wote ndio dira muhimu ya serikali yetu kujipatia mapato, kama tunavyojua kuna utitiri wa makumbusho na mambo ya kale kwenye utalii. Naiomba serikali ifanye utafiti wa kutosha ili kuyajua makumbusho yake na maeneo ambayo ni ya utalii kwa wote. Kuna maeneo mengi sana kwenye Wilaya ya Micheweni hayajafanyiwa utafiti, naiomba serikali pamoja na wizara iweze

kufanya utafiti wa kutosha, ili kuongeza kipato cha utalii kwa wote kwenye mambo ya makumbusho pamoja na historia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele hapo hapo tunajua kwamba historia yetu ya Zanzibar ni makumbusho ambayo yapo hai na yale ambayo yamefariki kwa kubomoka. Kwa kweli tumetumia fedha nyingi sana kwenye serikali kuyaendeleza makumbusho haya lakini hatukupiga hatua ndio pale niliposema kama serikali ifanye utafiti wa kutosha ili kuyaendeleza yale ambayo yameathirika kwa kuanguka na yake ambayo yanaendelea. Kwa mfano, kama tunavyojua kuna Msikiti wa Chooko tuna makaburi ambayo ya kihistoria yapo Tumbe, tuna na misikiti yetu ya kihistoria, kuna zana mbali mbali ambazo zimo mule zimeibiwa. Tunakumbuka kwamba awamu iliyopita kuna msikiti wa Shumba ya Mjini kuna vitu ambavyo ni thamani sana vimechukuliwa. Lakini tulifika pahali hatukufikia muafaka kujua vitu vile vimekwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, tuna makumbusho yetu yaliyoko Kusini Pemba nayo pia yanatakiwa yaendelezwe na yafanyiwe utafiti, kama nilivyosema Micheweni Maziwa Ng'ombe, kuna mapango ambayo ya historia, nayo pia hayajafanyiwa utafiti lakini pia kwa kushirikiana na jamii waweze kukaa wizara, ili waweze kuyatambua makumbusho hayo na maeneo ya historia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye Uchumi wa Buluu, kama tunavyojua Micheweni tuna Bahari ya Hindi ambayo ni kubwa sana. Ile bahari inatakiwa kwanza, kuwe na ulinzi wa kutosha kwa sababu kunaingia vyombo ambavyo vinavuwa kiharamu na kwa kweli Mhe. Waziri, pamoja na serikali isimamie kwa kina ili kuweka ulinzi wa kutosha ili bahari yetu na zana zetu ambazo zimo kwenye bahari kama samaki na mambo mengine yasipotee.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuendelea mbele niende kwenye Sekta ya Maji, kama tunavyojua Sekta ya Maji imeboreshwa zaidi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu iliyopita, na awamu hii ni kuendeleza tu tunamuomba Mhe. Rais kwa kusimamia majukumu yake pamoja na viongozi wa wizara wakiwa ni mawaziri waweze kuficha mianya ambazo zinaharibu mazingira ya maji kwa sababu kama hatukusimamia hatutofika pahala popote.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea mbele kwenye uwezeshaji, kwa kweli hapa tuna wanawake wengi ambao ni wawezeshaji wanatakiwa kusimamia na serikali hii kama alivyosema Mhe. Rais atawasimamia wanawake, ili na wao kuwapa kipaumbele ili kuondokana na umasikini ambao umewakabili.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali pamoja na viongozi ambao wameteuliwa pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu Makamu anatusimamia, kwa sababu na yeye ni Makamu wetu na kwa kweli nafuatilia mambo mbali mbali ambayo yameigusa serikali hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hotuba hii imechangiwa na waheshimiwa wengi hatuna haja ya kupoteza muda mrefu, lakini ilikuwa ipo haja na mimi kuweza kuichangia hotuba hii ya Mhe. Rais. Mimi naunnga mkono asilimia mia moja, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, na mimi nakushukuru Mhe. Bihindi Hamad Khamis kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Shaib Hassan Kaduara atafuatiwa na Mhe. Yahya Rashid Abdulla.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kujaalia nchi yetu ya Zanzibar kuwa ina amani, utulivu na upendo. Tunaomba Mwenyezi Mungu atuzidishie kwenye hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niunge mkono hotuba hii ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, ni *very fantastic speech.*

Mhe. Mwenyekiti, miongoni wa wajumbe wengi waliochangia walikuwa wakigusia masuala ya maji kupitia kwenye hotuba hii. Ni kweli, hata Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema *Wajaalna kulla shayin hayyi minalmaai. (Makofi*)

Kwa hiyo, waziri mwenye dhamana ya maji ndugu yetu inabidi akaze mkanda kwa sababu matatizo bado tunayo sambamba na juhudi kubwa iliyochukuliwa na serikali ya awamu ya saba lakini bado tuna matatizo na lazima afanye *task force* kwenye Mamlaka ya Maji *ZAWA*. Kwa kweli, mimi binafsi siko mbali na kituo kinachotoa maji kwa Pemba pale Machomanne ndani ya Jimbo langu la Chakechake kwenye mita mia tano tu maji sipati. Kwa hiyo, bado kuna tatizo ndugu zetu hawa waeleze tatizo ni nini na waziri asimamie masuala haya ya maji, watu wasilalamikie tena suala la maji.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wa Zanzibar sasa wanataka kuona mapinduzi kwa vitendo na Matunda ya Mapinduzi kwa kuyaona kwa vitendo sio tena kwa hadithi na hili Mhe. Rais alilizungumza sisi sote tulikuwemo humu asilimia 99.9 mapinduzi ni ya kuhadithiwa. Lakini Matunda ya Mapinduzi tumeanza kuyatumia sisi baada ya juhudi za wazazi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ili Zanzibar kuing'arisha na kuipa sifa kama Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mhe. Ali Hassan Mwinyi alipofungua mlango wa Zanzibar kwa kauli yake aliposema "Zanzibar ni njema atakaye na aje". Jamani Wazanzibari, Zanzibar yetu ni njema kweli lakini kuna mahali tulikosea wana-*philosophy* wanasema "*a person who never made a mistake never tried anything new". (Makofi)*

Tulikosea tujirekebishe, na mtu anaporekebishwa asiwe mkali Wazanzibari, Zanzibar inaumwa sasa tuitieni dawa na dawa ni kumsaidia Mhe. Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi ili nchi yetu sasa ikwamuke pale ilipokwama, kwangu mimi kuna baadhi ya mambo nimeyaona na humu katika hotuba ya Mhe. Rais na yeye kayaona pia. Mimi namuomba Waziri wa Nchi, Fedha na Mipango aende sasa makusanyo bado hatujakusanya vizuri kuna baadhi ya maduka hayalipi vizuri, kuna baadhi ya *super market* hazilipi vizuri wanaotukodisha nyumba zao vile vile hawalipi kodi. Mhe. Waziri katukusanyie hizi fedha zetu kwa sababu sisi tunawapa wao na wao kuna *share* ya serikali wailete.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la ufisadi lazima tuseme tulikuwa mafisadi, tukaifisidi nchi na sasa matokeo yake tumeyaona sisi wengine tulianza kuyazungumza mapema na wakatuona wabaya tukasumbuka sana lakini Mwenyezi Mungu kwa rehema zake katuleta hapa kwa mdomo huu

unatumika kwa Wazanzibari kusema kama wenzetu walituumiza. Leo Wakaazi wa Zanzibar waliokuwepo Pemba hawana raha ya kusafiri kwa sababu wamekosa usafiri wa uhakika, safari zao zinakuwa za kubahatisha ndugu zanguni. Hii nchi ioneani imani. Tumekwenda kununuliwa meli ambayo watu hawakufanya *survey* kama sisi tunahitaji kitu gani, meli ya aina gani, leo ipo pale inatutia hasara. Halafu leo mtu akiambiwa anakuwa mkali. Tulisema, watu wakawa wakali hapa na tulisema kwa ajili ya maslahi mapana ya nchi yetu na hatukuogapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru Dkt. Ali Mohamed Shein Rais Mstaafu. Kuna siku mimi katika uwanja wa *tenis* kule Pemba, nilimwambia mzee bado tunaibiwa na watu wako hawakusaidii. Suala hili likawa ni kaa la moto kwangu, lakini leo kila Mzanzibari anaona. Mimi nilisema miaka ile 2012 leo hapa 2021 kila Mzanzibari anaona. Hivi ndivyo ilivyokuwa Zanzibar yetu. Zanzibar hii sasa inataka msaada kutoka humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, msaada wa Mawaziri, msaada wa Wazanzibari wenyewe tuikwamue Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sehemu ya utumishi wa umma. Watumishi wa Umma wanalalamika kuhusu asilimia 40 ya *ZSSF*. Tunamuomba sana Mhe. Rais akatizame kilio kile. Je kuna nini. Akatizame kilio kile kwa nini wananchi walalamike, pale akatizame kuna nini. Wafanya ibada ya hija wahawaendi tena hija. Tunamuomba Mhe. Rais akapachunguze vizuri pale. Kulitengenezwa miradi tukapigwa. Lazima tuseme tulipigwa kwenye miradi ya *ZSSF* na hili hatuoni aibu kusema kwa sababu hata ripoti zinasema kama tulipigwa.

Kwa hivyo, Wazanzibari sasa basi kupigwa. Tunasema Wazanzibar sasa kila unapoona pana pigwa sema, huu ndio uwazi wa serikali yetu ya awamu ya nane, kwamba mwenyewe Mhe. Rais amekubali kama tuseme na tunasema.

Mhe. Mwenyekiti tukija kwenye masuala ya Shirika la meli. Sisi Wazanzibari haturidhiki na linavyokwenda Shirika la meli. Kuna meli ya Maendeleo kwa taarifa zisizokuwa na shaka meli hii ya Maendeleo huko iliko inatutia hasara. Kwa nini leo meli hii isirudi, kama ni kuikata *scraper* au kuiuza kwa thamani duni, lakini isiendelee kututia hasara maana haiwi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bandari. Bandarini bado hapajakaa sawa. Tulishaona ripoti na mwenyewe Mhe. Rais ametuambia kwamba pale palikuwa zikikushanwa na kutumiwa vipaya. Tumeona na tuna taarifa zilizokuwa hazina shaka vile vile kwamba pamenunuliwa sijui vitagi kwa bilioni sita. Bilioni 6 ya fedha za Wazanzibari imekwenda kununuliwa kitu hata kuonekana thamani yake ni ndogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, hivi jamani watu walikuwa hawana imani na nchi yao. Ikitokezea mtu ana imani na nchi na inamuuma. Tulikuwa basi tumuachie angalau na yeye apate kukosoa mule na hili ndilo jambo jema na chama chetu sisi kinasema ili uwe kiongozi bora lazima ukubali kukosoa na kukosolewa. Watu walikuwa wamekataa kukosolewa katika awamu ya saba. Wengi wao walikataa kukosolewa wakawa hawamshauri vizuri mzee wetu Dkt. Shein na muda mwengine wakamdanganya. Ikitokezea kumwambia ukweli wakawa bado wanatuzunguka nyuma.

Ndugu zetu lazima watuombe radhi. Lazima watuombe radhi Wazanzibari maana wameshatuumiza sana...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa. Nimekuona Mhe. Issa Haji Ussi.

**MWONGOZO**

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na nimesimama kwa kanuni ya 67 pamoja na kanuni 70. Nimuombe tu Mhe. Mjumbe ajielekeze kwenye hoja iliyokuwepo mezani. Maana maneno anayoyasema mengine yatampa tabu kuyathibitisha, kusema kwamba viongozi walikuwa walikimdanganya Mhe. Rais, itampa shida kuthibitisha na inaweza ikamuondolea heshima yake.

Mhe. Mwenyekiti, mjadala uliopo mezani sote tunajadili, sote tunakubaliana nao, sote tunaupenda. Tuna Hotuba ya Mhe. Rais, Dira ya Serikali yetu ya Awamu ya Nane, tuna miaka mitano ya kutekeleza. Mhe. Rais ameziona, miongozo ya serikali imetolewa, maelekezo ya serikali yametolewa, hatua zitachukuliwa. Chombo hiki kisimamie yale ambayo yana maslahi mapana na wananchi.

Tukimtaka Mhe. Mjumbe athibitishe kiongozi ambae amekwenda kumdanganya Mhe. Rais atashindwa. Akishindwa atachukuliwa hatua, akichukuliwa hatua tutakuwa tumemvunjia heshima yake. Nimuombe tu Mhe. Mjumbe ajikite kwenye mjadala uliopo kwenye meza nao si mwengine, ni hotuba ya Mhe. Rais. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. lssa Haji Ussi kwa kusimamia kanuni hiyo. Naomba Mhe. Shaib Hassan Kaduara uendelee kwa dakika zako zilizobaki lakini ufate miongozo ya kanuni kuhusiana na Hotuba iliyokuwepo mbele yetu tunayoijadili. Ahsante, nakushukuru Mheshimiwa, endelelea.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti, japo mengine yanakuwa yanachoma lakini inabidi tuvumulie hivyo, hivyo, maana mambo mengine...

**UTARATIBU**

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe, Mwenyekiti, nimesimama kwa nia njema na lengo langu...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Issa haji Ussi nimekufahamu na yale uliyoyazungumza hata mimi kama ulikuwa unaniona kabla ya kusema, nilikuwa natamani niweze kumuelewesha Mheshimiwa. Lakini wewe umesema ni haki yako pia na wajumbe tutumie hizi kanuni, si lazima kiti kiseme lakini hata nyinyi mnayo fursa ya kuona jambo ambalo linakwenda kinyume na taratibu zetu tuliseme.

Sasa Mhe. Shaib Hassan Kaduara, Mheshimiwa ametoa hoja pale na mimi nimekupa maelekezo. Sasa nadhani Mheshimiwa alitaka aseme, nimemuachia asiseme kuhusiana na kauli uliyozungumza “japo kuwa yanachoma” nadhani ndio hilo kidogo alitala akiseme. Hayachomi ila ufate tu taratibu Mhe. Shaib Hassan Kaduara, halafu mambo yaendelee.

Kwa hivyo, ukubali na ukuri kwamba ulikwenda kidogo nje halafu tuendelee na ile hoja yako ambayo unaisimamia. Hiyo, kauli ya kuwa mambo mengine yanachoma, Mheshimiwa nadhani itoe tu kwamba umeelekezwa ili tuende sawa katika kuendesha mambo yetu hapa.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi natengua kauli ya kuchoma. Hayachomi, ni mjadala wetu halali ndani ya kuchangia Hotuba ya Mhe. Rais wetu. Changamoto haziachi ndio ugeni jamani, vumilieni mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunapokwenda kwenye suala la biashara. Kwenye suala la biashara naomba nichangie kwenye hotuba ya Mhe. Rais, kuna wenzetu wa *TFDA* wajitahidi sana, kuna watu wanaumia sana. Kwa mfano, kuna watu wanafika pahali kwamba tayari wameshapewa vibali lakini ushindani wa kibiashara upo, unawasokota, wanaozuiwa. Wameshatoa mzigo bandarini unazuiwa. Hili jambo walisimamie wasiwaumize ndugu zao. Watu wanapoteza mitaji, serikali inakuwa haipati *income*. Namuomba Mhe. Waziri mwenye dhamana ya chakula na madawa alipitie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo ambayo niyapongeze basi ni masuala ya miundombinu ambayo serikali ya awamu ya 7 ilijitahidi na hili. Lazima hili suala tulipongeze sana lakini ndani ya Chakechake mji Mkuu wa Pemba wenye Jimbo la Chake chake bado kuna shida, sambamba na mitaro miziru iliyojengwa hapa kwetu katika Mkoa wa Mjini Magharibi bado na sisi Chakechake tuna tatizo kubwa, tuna kilio kikubwa na usumbufu mkubwa na muda mwengine siku za mvua unasababisha ajali ya watoto wetu kwenda madrasa na skuli, pale Mtoni Chakechake. Na sisi tunaomba mtaro ule tukasaidiwe, upo ndani ya mji, kati kati ya mji. Tunamuomba waziri mwenye dhamana hii, atusaidie kwenye hili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tuna suala la michezo. Nimshukuru na nimpongeze ndugu yangu Mhe. Tabia Maulid Mwita kuwa waziri anayehusika. Kuna kiwanja ambacho ni cha zamani, kikongwe, kinalingana na Mao-Tse-Tung kiko Tibirinzi Chakechake. Namuomba akakione kiwanja hiki, akipitie na akijue, kipo Chakechake ndani ya Mji wa Chake na hapo zamani ndio kiwanja kilichokuwa kikitumika kwa *primer* ligi. Namuomba sana Mhe. Waziri akipitie kiwanja kile alau akitupie macho. Vya kufanya atajua yeye baada ya kukiona. (*Makofi)*

Mhe. Mweyekiti, miongoni mwa mambo mazuri ambayo Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyaahidi katika hotuba yake hii, basi ni ustawi wa Wazanzibari. Mimi ningewaomba sana Wazanzibari tuendelee kushirikiana, ningeomba sana Wazanzibari tuendelee kumuamini Mhe. Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, alioyapanga yana neema tupu na yanafurahisha kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi sasa niunge mkono hoja hii lakini vile vile niendelee kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Chakechake kwa kuniamini, kwa kunipa muda ili niweze kusimamia mambo yao na tunaona kusimamia mambo ya wananchi yana changamoto zake na wao wenyewe wanaanza kuyaona, lakini nawaahidi kwamba sitowaangusha. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Shaib Hassan Kaduara. Waheshimiwa Wajumbe nilimtaja Mhe. Yahya Rashid Abdulla awe mchangiaji wa mwisho lakini nahisi kutokana na muda dakika zilizobaki inawezekana zisimtoshe katika kuchangia kwake.

Kwa hivyo, Waheshimiwa kabla ya kuakhirisha naomba nimtangaze yeye Mhe. Yahya Rashid Abdulla atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza jioni tukijaaliwa, atafuatiwa na Mhe. Shaaban pamoja na Mhe. Shadya Mohamed Suleiman ajiandae. Hiyo, nimewataja hao watatu ndio watakuwa wa mwanzo ili waweze kuwahi kufika. Waweze kuendelea kuchangia na mjadala wetu huu uendelee.

Lakini kabla ya kuakhirisha kikao hichi, naomba Waheshimiwa Wajumbe niwajuulishe kwamba wale wafanyakazi wa bima ya afya wapo hapo juu kwenye *gallery* ya mapumziko kwenye makochi kwa ajili ya kujazishwa fomu za bima ya afya. Kwa hivyo, tukitoka hapa waheshimiwa nadhani tuelekee huko ili kujaza hizo fomu.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwashukuru wachangiaji wote, na Waheshimiwa Mawaziri ambao walianza asubuhi kwa kujibu maswali. Niwashukuru sana kwa utulivu wenu na naomba niakhirishe mpaka saa 11:00 jioni. Ahsanteni.

(*Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Yahya Rashid Abdulla:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kupata nafasi hii kwa kuchangia hotuba ya Mhe. Rais aliyoitoa wakati wa uzinduzi w Baraza letu siku ya tarehe 11 Novemba, 2020.

Awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kukutana jioni hii katika majadiliano yetu ya kujadili hotuba ya Mhe. Rais. Lakini pia sina budi kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi na wananchi wa Jimbo la Kwahani kwa kuniamini na kunichagua niwe mtumishi wao katika Baraza hili tukufu Mhe. Spika.

Sina budi pia kuwapongeza wale wote ambao Mhe. Rais ameweza kuwateuwa katika nafasi tafauti kwa ajili ya kuongoza serikali ambayo anaiongoza yeye. Serikali ambayo ataiongoza kwa kipindi cha miaka mitano katika kumsaidia yeye katika majukumu ya kazi zinazomkabili Mhe. Rais katika serikali yake.

Lakini nimpongeze pia Mhe. Rais namna hotuba yake ambayo tunavyoijadili inayoonesha namna gani dira na muelekeo ya serikali anayoiongoza itakavyoendesha shughuli zake ndani ya miaka mitano kama inavyoainisha katika ilani ambayo aliinadi kwa wananchi ambayo waliiamini na kukichangua Chama cha Mapinduzi kwa asilimia 76.2% kwa kura za Uraisi. Lakini pia kwa asilimia 92 kwa kura za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na asilimia 93.6 kwa Madiwani ambao ni ushindi mkubwa na wa kihistoria katika suala zima la vyama vingi vya siasa.

Lakini pongezi nyengine za uteuzi alizowachagua viongozi ambao wanamsaidia yeye katika majukumu yake ya kazi za kila siku, aidha mwendo wa kasi na wa muda mfupi ambao tayari Mhe. Rais ameshaunza katika utekelezaji wake wa ahadi alizoainisha miradi ya Bandari

Mangapwani, Mkoani pamoja na Mpigaduri. Hii ni ishara na dhamira ya dhati ambayo aliyonayo Rais wetu katika uendeshaji wa majukumu ambayo tayari wananchi amewaahidi.

Mhe. Spika, niende katika hoja yangu katika ukurasa wa 25 wa kitabu cha Mheshimiwa alichokitoa yeye kuzindua, kuna suala la huduma za jamii. Mimi hoja yangu itakuja katika suala zima la Elimu, niweze kumkariri Mhe. Rais aliyozungumza katika *speech* yake alizungumzia suala la Elimu ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya jamii serikali yake itachukuwa hatua za kuimairisha ubora wa elimu ambayo ni haki ya msingi kwa kila mwananchi na katika kukabiliana na changamoto hizo zinazoikabili Sekta ya Elimu hivi sasa serikali itaekeleza juhudi zake katika kuimarisha miundombinu ikiwemo skuli za kisasa na kuzikarabati skuli za zamani. Kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kusomea pamoja na madawati kupitia upya mitaala ya elimu na kupunguza tatizo la walimu hasa wa Sayansi.

Mhe. Spika, nimpongeze Rais kwa hilo kwanza katika kuonesha dhamira ya dhati aliyonayo katika suala zima la elimu. Nimpongeze kwanza kwa kukutana na wadau wa elimu na kusikiliza changamoto zao, alionesha njia ya kukabiliana na changamoto lakini pia serikali anayoiongoza na kuahidi kuendelea kushirikiana nao na kila aina katika kutafuta njia ya kuondosha changamoto zakutatua elimu na kuweza kusogeza elimu mbele. Katika suala la ujenzi wa skuli za kisasa ndani ya kipindi kifupi tumekuwa tukiona skuli nyingi sana zinajengwa na za kileo ambazo zinalingana na hadhi ya kutaka kuendeleza elimu yetu na maeneo hayo ya ujenzi yanazidi kuzingatia mahitaji ya viwanja vya michezo mbali mbali.

Mhe. Spika, nilikuwa nina maana ya kwamba zinajengwa skuli za kileo lakini, skuli zinazotengenezwa sasa hivi hazizingatii maeneo ya michezo, kwa sababu ndani ya maskuli ndio vinapoanza kuonekana vipaji mbali mbali, vipaji ambavyo vingekuwa ni misingi mizuri ya kuanzishwa katika maskuli kuanzia skuli za msingi hadi sekondari. Tukirudi nyuma huko nyuma kuna viongozi wengi sana na vipaji vingi sana vilipatikana skuli akiwemo Mheshimiwa wetu Rais mstaafu wa awamu wa saba, kipaji chake kilianza kuonekana skuli. Nikiwa na maana katika mahitaji ya skuli zetu tunazozitengeneza sasa hivi, Mhe. Spika, ipo haja ya miundo mbinu ya skuli zinazotengenezwa kuwekwa maeneo maalum ya shughuli za michezo ili iwe ni sehemu ya kutafutwa vile vipaji ambavyo vitahitajika.

Bado mimi naamini nchi kama Zanzibar vinazaliwa vipaji hadi leo lakini vinashindikana kuonekana katika mfumo ambayo tuliokuwa nao sasa hivi. Kama tutakumbuka huko nyuma skuli zetu hata na hizi za Mjimkongwe ambazo sasa hivi zinahitajika kukarabatiwa zilikuwa bado zina maeneo maalumu ya michezo, tunatengeneza skuli sasa hivi tunahitaji zaidi maeneo hayo kwa ajili ya kufufua na kuvipata vipaji vyetu vya vijana wetu kwa sababu sasa hivi michezo ni ajira.

Suala la pili kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kusomea pamoja na madawati huo ndio muelekeo wa serikali. Pamoja na kujengwa skuli nyingi bado kuna kuzingatia miundombinu ya watu wenye mahitaji maalum, bado kuna uhaba mkubwa Mhe. Spika, kwa vifaa vya kufundishia na kusomea watu wenye mahitaji maalum katika maskuli yetu. Hayo yanatokana na ukubwa wa gharama za vifaa hivyo. Hata hivyo, nashauri serikali itowe vipaumbele na kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu katika kuwatafutia vifaa vyao.

Mhe. Spika, nije katika sehemu ya Utawala Bora, serikali yetu sasa hivi ina mwendo wake wa kasi mkubwa sana na bado Mhe. Rais amekuwa akizungumzia masuala ya tuondokane na mazoea. Lakini bado katika suala zima la uwajibikaji hasa katika maeneo ya huduma. Mhe. Spika, maeneo haya bado wananchi katika maeneo yetu hasa mahospitali bado kuna matatizo makubwa zile huduma wanazozipata wananachi hazikidhi vigezo maana sio bora. Kwa hiyo, lazima tukubaliane na kasi ambayo anataka kwenda Mhe. Rais ili tuondokane na matatizo yanayotukabili katika serikali yetu. Wananchi wana matarajio makubwa na serikali yao na watendaji wetu wakubaliane na mabadiliko yaliyokuwepo katika masuala mazima ya utendaji.

Mhe. Spika, dhamira ya Rais wetu ya kukutana na wadau tafauti hii yote kuonesha jinsi gani wananchi waweze kuiamini serikali yao waliyoiamini na kuichagua kwa ushindi mkubwa waweze kuiamini serikali yao na waweze kwenda na matumaini ambayo wanayatarajia katika masuala mazima ya huduma...

**Mhe. Spika:** Naomba umalizie Mheshimiwa.

**Mhe. Yahya Rashid Abdulla:** *Inshaallah* Mhe. Spika.

Mwisho niishauri tu nipende kusema naunga mkono hoja kwa asilimia zote. Ahsante sana.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nitangulie kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu muumba mbinu na ardhi kutujaalia jioni ya leo kuwa pamoja katika Baraza lako hili tukufu. Lakini nikupongeze wewe pamoja kwa kunipa nafasi na kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Baraza la kumi Wawakilishi la Zanzibar.

Mhe. Spika, kipekee kabisa nimpongeze kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Hussein Ali Hassan Mwinyi Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalum Seif Sharif Hamad, Makamu wa Pili na mwisho kwenye pongezi si kwa umuhimu sana nimpongeze kaka yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuteuliwa kwake kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijaelekea kwenye hoja nianze kwa kuipongeza sana hotuba ya Mhe. Rais watangulizi waliongumza wameisifia sana nami naungana nao kwa sababu hotuba inastahili sifa zaidi ya zilizotolewa.

Mhe. Spika, ukiangalia kwa undani zaidi utagundua ni hotuba ambayo inekidhi mahitaji na matarajio ya Zanzibar kwa miaka zaidi ya 20 mbele. Lakini hotuba iliyochambua dira ya muelekeo ya serikali ya awamu ya nane kwa miaka mitano ijayo.

Mhe. Spika, kwa kuokoa muda nijielekeze moja kwa moja kwa kuanza na ukurasa wa 17 uniwie radhi sitakwenda kwa mtiririko lakini nitajaribu kugusia na kwa pale ambapo nimeona inafaa kuchangia katika suala la elimu.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais ameelezea kwa kina azma yake ya kuboresha sekta ya elimu katika hotuba hii sina haja ya kuchambua neno moja moja lakini kwa ukubwa wa maudhui

yake amegusia zaidi suala la kuboresha ufaulu wa wanafunzi wetu hasa wale wa kidato cha nne na kidato cha sita.

Mhe. Spika, wakati Mhe. Dr. Saada Salum Mkuya akieleza alijaribu kugusia mambo mengi yanayohusu sera na sheria katika kuboresha Sekta ya Elimu. Lakini mimi nataka niwe tafauti kidogo na kwa kujaribu kutoa mifano bado kuna vitu ambavyo vipo nje ya sera na sheria zetu ambavyo vinakwaza maendeleo ya ufaulu wa wanafunzi wetu hasa wa kidato cha nne na cha sita. Nitatolea mfano kwa kwa ku-*declare interest* katika Skuli yangu ya Sekondari ya Mpendae. Mhe. Spika, matokeo yaliyopita hayakuwa mazuri sana kwa skuli hiyo lakini wakati kama Wawakilishi tunafatilia kubaini nini kiini cha sababu hizo moja kati ya sababu ambayo ilielezwa ni kwamba pamoja na kuwepo kwa Skuli ya Sekondari ya Mpendae na Skuli ya Sekondari ya Migombani wanafunzi wanaofaulu ambao ni wazawa wa Mpendae kwa kiwango bora cha *division I* na *II* malalamiko ya walimu ni kwamba wanafunzi hawa wanatolewa na kupelekwa katika Skuli ya Dr. John Pombe Magufuli na wanaosalia kwa *division III* za mwisho na *IV* ndio wanapelekwa katika Skuli ya Sekondari ya Mpendae.

Sasa ukilitizama Mhe. Spika, hili ni tatizo la kimfumo wa ndani ile ni Skuli ya Sayansi tunawapeleka wananfuzi ambao ufaulu wao ni wa mwisho wale ambao wana uwezo wa matokeo ya kuleta *division I* na *II* tunawapembua tunawapeleka skuli nyengine sasa wakati tunajaribu kuuliza, hoja kubwa iliyokuwepo skuli ile ni ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imebeba jina lake. Kwa hiyo, ghofu iliyotanda watu pengine walikuwa wanahofia ingefanya vibaya watu wangetumbuliwa.

Lakini Mhe. Spika, nilitaka niliweke sawa hili hata sasa Wawakilishi wa Wananchi tunaogopa kutumbuliwa na wananchi kwa skuli zetu zinavyofanya vibaya na zinapoleta matokeo mabaya. Sasa ushauri wangu katika hili pamoja na kupongeza jitihada nzuri za serikali katika kuboresha huduma hii ijaribu sasa kuwachanganya wanafunzi hawa wale wenye vipawa vikubwa na wenye uwezo mdogo ili wigo ule wa ufaulu uwe mkubwa katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, nikielekea katika ukurasa wa 13 katika Sekta ya Mafuta na Gesi nishukuru sana jitihada za serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane katika kulipa nguvu na umuhimu mkubwa suala la Uchumi wa Buluu ambalo lina mnasaba na *Oil and Gas,* hapa kidogo Mhe. Spika, nilikuwa nataka nizungumze kidogo na Waziri mwenye dhamana tumewahi kukutana nae katika kamati lakini na hapa nitalisema ili Wazanzibari nao wapate uwelewa wa hili.

Tume-*experience* nchi nyingi duniani zimejikita katika uchumi huu wa mafuta na gesi hata ndugu zetu wa Tanzania Bara. Mhe. Spika, tunapoelekea kwenye uchumi kubwa wa namna hii suala la usalama wa nchi ni suala la msingi na linapaswa kipaumbele nchi za wenzetu zimepitia katika migororo mingi ambayo inasababishwa na wafanyabiashara wakubwa wennye maslahi na sekta hii. Watu hawa wamekuwa wakiwarubuni wazawa wakiwahujumu ili kufanya saboteji kwenye serikali yao. Matokeo yake kuibuka kwa migororo na tumeiona wakati wenzetu Watanzania Bara wanachimba gesi kule Mtwara migogoro ilikuwa mingi kati ya wananchi na serikali yao.

Sasa ombi langu na indhari yangu wakati tunaelekea kwenye uchumi mkubwa wa namna hii suala hili la usalama hasa wa watifa letu kuepuka migororo lizingatiwe na lipewe kipaumbele zaidi. Sambamba na hilo kuwepo kwa ma-*experts* ambao wana uwezo mkubwa wa majadiliano ya kibiashara limezungumzwa na kakaangu Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) hili na mimi nalisisitiza kwa sababu tunaenda katika ubia na mashirika makubwa wafanyabishara wenye uwezo. Kwa hivyo, lazima na sisi tuimarishe nguvu zetu za ndani katika kushindana ama kukidhi vigezo vya ushindani.

Sambamba na hilo nimpongeze tena Mhe. Rais kwa kumteuwa Dr. Mwinyi Talib Haji Mwanasheria Mahiri makini ambaye atatusaidia sana. Nina imani kubwa atatusaidia kwa kuimarisha kitengo chake cha sheria ambacho ndicho kitahusika katika kuingia mikataba mikubwa yenye maslahi na taifa letu. Kwa hiyo, rai yangu kwenye upande huu napo yeye pamoja na timu yake nzima wajiweke uzuri katika uwezo wa kuweza kuhakikisha serikali yetu haiingii katika mitego mikubwa ya kibiashara ambayo baadaye inaweza ikalisababishia taifa hasara kubwa.

Mhe. Spika, nigusie kidogo ukurasa wa 10 ambapo suala la Uchumi wa Buluu limezungumzwa kwa upana wake. Nimpongeze tena Mhe. Rais kwa kuunda wizara maalum ambayo inahusiana na uchumi wa buluu na uvuvi. Lakini katika hili wakati Mhe. Rais anatoa *speech* yake aliwaeleza Wazanzibari juu ya suala la ufinyu wa ardhi na muelekeo wetu katika bahari.
Mhe. Spika, mimi nataka niseme kidogo, Mhe. Spika uwekezaji wowote ambao unahusu bahari *base line* yake ni ardhi ya nchi kavu. Kwa hivyo, tutawaita wawekezaji wakubwa na tumeona *sign* zimefanyika kubwa lakini hawendi kujenga viwanda baharini wanakwenda kujenga viwanda vyao katika ardhi. Zanzibar sasa hivi tunakabiliwa na uhaba mkubwa wa eneo la uwekezaji nchi kavu, ukienda *ZIPA* Mhe. Spika ni balaa, ile ni mamlaka ambayo imepewa uwezo na dhamana ya kukuza na kuendeleza uwekezaji lakini suala la *Land Bank* kwa hivyo, hapa rai yangu ni nini tujaribu kwa kila uwezo tutakaojaaliwa na ninaamini hili chini uongozi wa Mhe. Rais na Makamu wa Pili wa Rais linawezekana tujaribu ku-*review* mikataba ya wawekezaji ambao tayari wanamiliki maeneo makubwa ya ardhi bila ya kuyaendeleza.

Haya ikiwezekana sheria zipo zisimamiwe vizuri ardhi hizi zirudi serikalini ili wale wawekezaji tunaowalenga wakija wasisumbuke kupata maeneo ya uwekezaji. Mhe. Spika, mengi yameshazungumzwa nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja asilimia mia moja na nimshkuru tena Mhe. Rais na uongozi wake kwa umakini na uweledi mkubwa katika kuliongoza taifa letu kwa siku mia moja zilizopita na tuna matumaini makubwa kwa kipindi kilichosalia.

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi na mimi yakuweza kuchangia hutuba ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa katika Baraza la kumi la Wawakilishi tarehe 11 Novemba, 2020.

Mhe. Spika, naomba kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambae anaendelea kunipa pumzi zake na nikaweza kusimama hapa nikiwa ni mwenye afya. Lakini Mhe. Spika, naanza kwa kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushindi mkubwa alioupata katika kuongoza nchi yetu, tunamuahidi Mhe. Rais kwamba tutampa mashirikiano na tunamuombea Mwenyezi Mungu amzidishie hekma busara na

ampe afya njema ili aendelee kutuongoza Zanzibari na kutufanyia yale mazuri ambayo ameyakusudia.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuniamini na kuniwezesha tena kuweza kuingia katika Baraza lako tukufu niseme niko pamoja nao sambamba lakini niendelee kuwambia kuwa sina cha kuwalipa isipokuwa Mwenyezi Mungu ndie atake walipa. Mhe. Spika, hutuba ya Mhe. Rais kwa kweli ni hotuba nzito ambayo imepangika na imezungumzia kila sekta lakini Mhe. Spika, mimi nitachangia kwenye baadhi ya sekta kwa haraka haraka ili kwa ajili ya kuokoa muda.

Mhe. Spika, nianze na kwenye uvuvi, Zanzibar tumezungukwa na bahari tunamshukuru Mwenyezi Mungu, na bado suala la uvuvi kusema la ukweli Mhe. Spika, hatujalifanyia vizuri. Kisiwa cha Pemba Mhe. Spika, kimejaliwa samaki wengi kila siku samaki hawa wanazaliwa. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia hotuba ya Mhe. Rais kujipanga kutafuta vyombo vya kisasa kutumia neema hii ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Ili kuinua salama na  uvuvi nchi hii Mhe. Spika, kuna mambo katika sekta hii ya uvuvi tunaomba serikali ili iweze kupatikana. Kwa mfano, vyombo vya kisasa vya kuvulia, pili taaluma kwa watumiaji wa vyombo hivyo na tatu utafutaji wa soko au maeneo ya kufanyia biashara.

Nikiondoka kwenye uvuvi Mhe. Spika, naomba kidogo nigusie suala zima la utalii, Mhe. Spika, kama tunavyoelewa serikali zote duniani ili ziimarishe huduma za jamii, maji safi na salama, elimu ya afya na kadhalika lazima zikusanywe kodi. Hivyo, kupitia utalii makusanyo hayo hayako vizuri katika maeneo ya nyumba za wageni, naiomba serikali na wizara husika kulifanyia kazi eneo hili ili makusanyo yasiwe ya kusuasua. Maeneo muhimu Mhe. Spika, ambayo yanapaswa kufikiriwa ni bandari na viwanja vya ndege nyumba za kulalia wageni. Mhe. Spika, kwa sasa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anatilia manaani suala zima la ukusanyaji wa kodi ili serikali iweze kutekeleza mambo mbali mbali aliyoahidi wakati wa kampeni alipokuwa akizifanya. Kwa hivyo, naomba suala hili wizara husika pamoja na serikali waweze kulifanyia kazi hususan katika maeneo ambayo niliyoyazungumzia.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba kidogo nigusie elimu, sekta ya elimu imekumbwa na kasoro mbali mbali hapa nchini pamoja na lengo zuri la serikali ya awamu ya nane mambo muhimu yanahitajika kuangalia kwa makini suala hili la elimu mfano, uwepo wa walimu wenye uwezo wa kitaaluma motisha kwa walimu ili kuondoa ile hamahama ya walimu kutoka sekta ya umma na kukumbilia kwenye sekta binafsi. Ujenzi wa nyumba za walimu wanaosomesha vijijini lakini pia upatikanaji na uwepo usafiri wa walimu hawa wanaokwenda masafa marefu.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, naomba kidogo nizungumzie biashara na viwanda Mhe. Spika, vijana wetu wengi hawana ajira za uhakika sio sekta ya serikalini wala sekta binafsi. Hivyo Mhe.Spika, katika eneo hili naunga mkono hutuba ya Mhe. Rais, aliposema kuwa katika uongozi wake atahakikisha kuwa sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika mpango wa mkakati wa ujenzi wa viwanda vidogo vidogo na na vyakati vikubwa vyenye kuzalisha bidhaa bora. Mhe. Spika, iwapo serikali itasimamia kikamilifu uwepo wa viwanda hapa nchini basi mrundikano wa vijana katika vijiwe utapungua na vijana wengi kupata ajira katika maeneo ya viwanda.

Mhe. Spika, naingia tena bandari kidogo Mhe. Spika, hizi ni pongezi napenda kumshkuru Mhe. Rais kwa kufanya ziara makusudi kwa kutembelea Bandari ya Malindi ili kuonana na wafanyabiashara na kuweza kuona changamoto za wafanyabiashara wale ambao zinawakabili nampongeza sana Mhe. Rais kwa kulifanya hili.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nizungumzie na kumalizia suala zima la udhalilishaji. Maomba nichukue fursa hii tena kwa kumpongeza Mhe. Rais, kwa kutilia mkazo suala zima hili la udhalilishaji sote Mhe. Spika, tunajua kwamba udhalilisha katika nchi yetu sasa hivi umekuwa ni mtihani. Kwa hivyo, tumuhakikishie Mhe Rais kwamba tutaungana nae na tutampa *support* zetu zote katika suala hili.

Lakini pia kwa kuanzisha mahakama pekee ya kesi hizi za udhalilishaji niombe tu Mhe. Spika, kwa sababu watakao fanya kazi katika mahkama ni binadamu ninaamini tukishirikiana sote kwa nguvu zetu na nia yetu ikawa safi, basi ninaamini kwamba udhalilishaji Zanzibar itakuwa ni historia. Kwa hivyo niwaombe wananchi na sisi viongozi wao tutashirikiana katika suala zima la kuondosha udhalilishaji katika nchi yetu kwani udhalilishaji Mhe. Spika, sasa hivi unatutia dosari katika nchi yetu ya Zanzibar.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba niseme tu naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Mussa Fuom Mussa: A**hsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona jioni hii na mimi kunipa ruhusa ya kuchangia kidogo hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Mhe. Spika, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Rais kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kwa kura nyingi sana. Pili vile vile nimpongeze Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad kwa kukubali na kuiendeleza Katiba yetu ya Zanzibar vile inavyokubali au inavyotuelekeza kwa sababu inatuelekeza tuwe na serikali ya pamoja. Kwa hivyo, na yeye kwa vile kakubali pamoja na chama chake ni vyema tukampongeza kuwa nae pamoja. Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuwa na yeye yuko pamoja katika nyanja kubwa ya kumsaidia Mhe. Rais katika kuendeleza nchi yetu ya Zanzibar.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi niseme kwamba hutuba ya Mhe. Rais ina muelekeo mzima wa nchi yetu ya Zanzibar pindipo haya yote yaliyomo humu yatatekelezwa kama vile alivyoelezea katika kitabu chake hichi.

Mhe. Spika, mimi nataka kidogo nijikite katika Mapinduzi ya Uchumi Zanzibar. Mhe. Rais hapa amelezea mambo mengi katika Mapinduzi ya Uchumi Zanzibar kaelezea uchumi wa Buluu huu nao una mambo mengi lakini sana unajikita kwenye bahari. Lakini katika ukurasa huu wa 10 Mhe. Rais hapa katika hotuba yake amelezea ahuweni tuliyonayo ni kuwa na eneo kubwa la bahari hivyo sisi wazanzibari hatuna budi tuigeuze bahari hii kuwa ni eneo la shamba letu.

Huko ndiko fursa za ajira za Zanzibari mpya zilipo huu ndio msingi wa dhana nzima wa uchumi wa bluu. Mhe. Spika hii dhana hii ni dhana nzuri kwa sababu nchi yetu ni kisiwa na tumezungukwa na bahari na ukweli tulionao ni kwamba bahari yetu bado iko bikra bado haijavuliwa, naona waheshimiwa mumefurahi sana kwa kusema neno hilo. Bado bahari yetu ina samaki wengi na bado hawajavuliwa meli nyingi za nje huja zikaiba samaki sasa na wavuvi wetu bado wengi wa wavuvi wa nchi hii wanatumia ule ule uvuvi wa kizamani wa mshipi kwa kuvua

samaki mmoja mmoja. Sasa nadhani Mhe. Rais alipoelezea hii dhana hii ni kwamba itakapotekelezwa basi asilimia kubwa ya Wanzanzibari watafaidika na dhana hii ya uvuvi wa bahari kuu.(*Makofi*)

Kwa hivyo, vile vile niseme kwamba hata Mhe. Rais alipokuwa anagombea urais wa Zanzibar alifika katika jimbo letu na alikuja katika shehia ya Muambe na akaonana na wavuvi, na wavuvi walimueleza kwamba bado hawana zile zana za kufikia bahari kuu. Sasa nadhani Mhe. Waziri, hapa anaehusiana na uchumi wa bluu namuomba tu apate mda atakapokuja katika jimbo langu aje awatembelee wavuvi kwa sababu tuna wavuvi wengi, tuna wavuvi wa Mtangani tuna wavuvi wa Kiwani lakini pia tuna wavuvi wa Shamiani pia na Muambe. Lakini hawa bado wanavua katika uvuvi ule ule wa kizamani wa kuvua samaki mmoja mmoja kwenye mshipi.

Mhe. Spika, baada ya hapo vile vile nielezee suala la utalii Mhe. Rais kaelezea hapa na napenda ninukuu kidogo ukurasa wa 12.

'Nimeahidi na nitaetekeza ahadi ya kuongeza utalii katika kisiwa cha Pemba nina azma ya kukifanya kisiwa cha Pemba eneo maalum la uwekezaji kwa kutoa vivutio mahasusi kwa wawekazaji ili maendeleo ya Unguja yaendane sambamba na maendeleo ya Pemba'.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais kwa azma yake hii kwa sababu anakusudia kwamba atoe kipa umbele atoe unafuu wa kisiwa cha Pemba kwa sababu bado suala la utalii Pemba liko nyuma kidogo ukilinganisha na kisiwa cha Unguja. Kwa hivyo, azma hii Mhe. Rais akiitekeleza basi na kisiwa cha Pemba kitapata nafuu kwa ajili ya utalii hasa utalii huu wa fukwe.

Mhe. Spika, niende haraka haraka katika suala la bandari, Mhe. Rais hapa kasema kwamba pia katika kujenga vile vile tumedhamiria kuimarisha bandari ya Wete na Shumba Mjini kadhalika tutaimarisha bandari ya Mkoani, ili iweze kuhudumia meli kubwa kutoka njie moja kwa moja kwa lengo la kunyanyua uchumi na biashara kwa kisiwa cha Pemba. Mhe. Spika, tumpongeze Mhe. Rais kwa sababu bandari yetu ya Mkoani bado haijakuwa na uwezo wa kutoka meli moja kwa moja kutoka nje zikafika Mkoani. Sasa likifanyika hili basi wafanyabiashara wengi watapata unafuu na wananchi wanoishi Pemba watapata unafuu wa bei za vyakula na mambo mengine mengine.(*Makofi*)

Mhe. Spika, baada yapo vile vile niende kuchangia katika suala la elimu, Mhe. Rais hapa katika ukurasa 25 kaelezea kwamba katika mambo atakayoyafanya moja wapo ni kuimarisha elimu hasa katika kupunguza tatizo la walimu. Mhe. Spika, hili tatizo ni kweli kwa sababu hivi sasa tuna skuli nyingi zina upungufu wa walimu sana tu lakini, katika skuli zote zenye upungufu wa walimu lakini skuli yetu ya Muambe katika Shehia ya Muambe imezidi, upungufu umekuwa mkubwa tena sana. Kwa sababu hivi sasa ninavyozungumza na suala hili kila mara nilipokuwa nikipata fursa nilikuwa ninalizungumza Mhe. Spika, hivi sasa skuli ya Muambe Msingi ina upungufu zaidi ya walimu 50.

Nadhani kipindi kilichopita kamati nani wote walikuwa wanaenda kuangalia pale lakini katika jitihada yote iliyofanya serikali ya kuajiari walimu bado tatizo la walimu lipo kubwa. Hivi sasa matokeo ya mara hii darasa la nne tumetokea wa mwisho. Hii sababu kubwa ni sababu ya walimu, Sasa namuomba Mhe. Waziri anayehusika na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa basi apate

muda aje tuende skuli hasa na yeye akathibitishe, kwamba hili tatizo lipo kweli au la ili lile tatizo lipatiwe ufumbuzi kwa sababu tunamshukuru Mwenyezi Mungu serikali imetujengea skuli za ghorofa pale lakini pia imekuwa ndogo, sasa nadhani kidogo haijambo tunafanya kazi.

Pale kuna mpango hivi sasa kujenga skuli nyengine ya msingi katika shehia ya Jombwe kwa hivyo nadhani Mhe. Spika, hili nalo tunaiomba serikali ili elimu iende sambamba na wakati wetu huu tulionao basi suala la walimu lipatiwe ufumbuzi.

Mwisho nasema nachangia katika sekta ya barabara Mhe. Spika, suala la barabara Mhe. Rais kazizungumza barabara za ndani na sisi tunazo na ni mbovu kwa mfano mimi katika jimbo langu ninanyo barabara kutoka Mtambile, Muambe barabara hii hivi sasa haipitiki hali mbaya. Lakini pia tunayo barabara kutoka Ukutini Mtangani imejengwa na *MIVAD* lakini hivi sasa hali yake sio nzuri.

Kwa hivyo baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naiunga mkono hotuba hii asilimia mia juu ya mia.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na uhai jioni hii tukaweza kukusanyika hapa kwa ajili ya kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba na hasa hii hoja iliyokuwepo mbele yetu ya kuchangia hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar aliyoitoa tarehe 11 mwezi wa Novemba, 2020 wakati anafungua Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi jioni hii ya kuchangia. Pia nikishukuru chama changu na kukipongeza sana Chama cha ACT Wazalendo, kwa maamuzi ya busara yenye kuzingatia maslahi mapana ya nchi hii ya kuamua kuingia katika Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nielekee moja kwa moja kwenye kuchangia hoja iliyokuwepo mbele yetu. Mhe. Spika, wakati Rais analihutubia Baraza hili kwenye hotuba yake ukurasa wa tisa alisema maneno yafuatayo na naomba kuyanukuu.

3) “Kote nilikopita wakati wa kuomba ridhaa ya wananchi wa Zanzibar nimekutana na ari, shauku na utayari wa hali ya juu ya wake kwa waume, vijana na wazee, wakulima kwa wavuvi, wafanyabiashara kwa wafanyakazi na makundi yote na kuyapokea mapinduzi mapya ya kiuchumi na kujenga Zanzibar. Wananchi wetu wamechoshwa na siasa za uhasama, kuhubiri chuki na visasi ambavyo havibadilishi hali ya maisha yao kuwa bora zaidi, wanataka matunda ya Mapinduzi na sio simulizi za Mapinduzi na Muungano, wanachotaka ni kustawi na kufaidika na matunda ya mapinduzi kwa usawa bila ya upendeleo wala ubaguzi. Mimi nakubaliana nao na nasimama nao na mimi nimewahi”. Akamalizia, ‘yajayo ni neema tupu”.

Mhe. Spika, kwa nini nimenukuu maneno hayo, na *interest* yangu kubwa ni haya maneno yaliyokozeshwa, na nina amini kulikuwa kuna sababu ya kuyakozesha maneno haya na yalikuwa haya yanatosha kuyatafsiri sasa kwenye michango yetu nini Rais anakusudia, nina amini kwenye uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane, Mhe. Rais atayatafsiri maneno haya kwa mabadiliko ya

kisera na ya kisheria, ili tuweze kufikia kwenye malengo haya ya kufaidika na matunda ya Mapinduzi.

Matunda ya Mapinduzi Mhe. Spika, maana yake ni wananchi kupata maji safi na salama, afya bora, elimu bora, huduma za nishati, ajira, uhakika wa usalama wa mali zao na kadhalika. Kwa hivyo Mhe. Spika, haya yaliyosemwa na Mhe. Rais ndio ambayo naamini kabisa ndio sisi wawakilishi kwa umoja wetu, Waheshimiwa Mawaziri kwa umoja wao na watendaji wengine wa serikali watajikita katika kutafsiri falsafa hii ya Mhe. Rais katika kumsaidia ili kuleta ustawi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya kumaliza kuchangia hiyo napenda pia nijikite kwenye eneo jengine ambalo Mhe. Rais amelizungumza katika hotuba yake, nalo ni suala zima la utalii. Kwenye ukurasa wa 12 wa hotuba ya Mhe. Rais amezungumzia dhana ambayo ipo ya utalii kwa wote. Mhe. Spika, ni muhimu sasa dhana hii ikatafsiriwa kwa kufungamanisha sekta zote za kiuchumi na sekta za kijamii zinazoingiliana na utalii, ili kuona wananchi wananufaika na utalii uliokuwepo.

Mhe. Spika, hivi karibuni kumekuwa na mikakati mbali mbali ya kuhakikisha kwamba utalii wetu unawavutia wawekezaji wakubwa. Wawekezaji watakaowekeza katika mahoteli makubwa na huduma za viwango vya juu sana. Mimi sipingani na mikakati hiyo wala dhana hiyo ni muhimu. Lakini vile vile tutambuwe kwamba hawa wawekezaji wakubwa wanao utamaduni wa kutokushiriki katika ujenzi wa uchumi wa watu, badala yake wao wanashiriki zaidi katika kulipa kodi. Sasa sote ni mashahidi na wale ambao wanatoka kwenye maeneo ya utalii, utakuta mahoteli makubwa *supplies* zao hawazipati kutoka ndani, Kuna mahoteli mpaka maji ya kunywa yale wanaagiza kutoka Afrika ya Kusini. Kuna mahoteli kila kitu *supplies* zao zinaagizwa kutoka. Sasa namna gani kama tunataka kwenda na hizi dhana mbili, dhana za utalii wa hali ya juu na dhani na dhana ya utalii kwa wote. Ni lazima sasa serikali itafsiri vipi dhana hizi mbili zinaweza zikaingiliana kufungamanisha sekta za kiuchumi ili kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na uwepo wa miradi mikubwa au uwekezaji mkubwa kwenye Sekta hiyo ya Utalii.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nakusudia namna ambavyo wanaweza kuwa-*outsource* mahitaji yao kutoka ndani na badala ya mahitaji kutoka nje. Hili haliwezi kwenda peke yake bila ya kuwajengea uwezo watu wetu.

Mhe. Spika, katika jambo jengine ambalo Mhe. Rais amekuwa akilizungumza sana, sio kwenye hotuba hii tu, lakini hata kwenye hotuba zilizofuata kila anapokutana na wadau. Wengine tumekuwa tukifuatilia sana hotuba zake anapokutana na wadau. Mhe. Rais ameonesha *concern* kubwa ya kutokuwepo utamaduni wa kuhudumia watu katika sekta ya umma, amekuwa kwa maneno yake mwenyewe Mhe. Rais amesema anatamani ku-*instil* kile alichoita *cooperate culture* kwenye Taasisi za Umma.

Mhe. Spika, ni jambo la kuunga mkono sana, ili kuhakikisha kwamba Taasisi zetu za Umma zinatoa huduma katika dhana hiyo ya *cooperate*, katika mtindo wa *cooperate culture*. Sasa *cooperate culture* inahitajika kushushwa chini, isiwe tu katika ngazi ya wizara ishushwe chini wilayani, mikoani na ishushwe kila sehemu kwenye taasisi za huduma.

Mhe. Spika, moja kati ya tatizo kubwa tulilokuwa nalo katika taasisi zetu za huduma hasa za umma ni kukosekana kwa hii *cooperate culture* na hii inajengwaje, inajengwa kwa wafanyakazi na watendaji kwenye hizo taasisi. Kwanza kuwa na *shared values and beliefs*, kila mmoja ajuwe madhumuni ya kuanzishwa kwa taasisi hiyo anayofanya kazi. Malengo na matarajio ya hiyo taasisi anayofanyakazi. Unaweza kwenda kwenye taasisi za umma ukakuta anachokijua mfanyakazi huyu kuhusu taasisi ile, ni tofauti na anachokijua mfanyakazi mwengine kuhusu taasisi hiyo hiyo anayoifanyia kazi. Hapo tunasema hakuwezi kuwa na *cooperate culture*, kwa sababu hakuna *shared values and beliefs*. Sasa ni muhimu sana, kwa sababu Rais ameonesha dira ya kwamba anatamani mtindo wa utoaji huduma kwenye sekta ya umma uwe wa ile *culture* ya *cooperate*, kama wanavyofanya kwenye *private sector* basi hili tumsaidie kwa kulitafsiri. Hili pamoja na kwamba linakosekana sana kwenye taasisi zetu, jambo la kufurahisha ni kwamba ukisoma kwa mfano, kanuni za utumishi wa umma za serikali hasa kanuni ya 37, inasisitiza kuwepo kwa mkataba wa huduma kwa wateja, yaani *customer charter*.

**Mhe. Spika:** Anza kuhitimisha Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Spika, nahitimisha. *Customer Charter*. Mkataba wa huduma kwa wateja. Leo unakwenda kwenye taasisi za umma unataka huduma hujui *time line* ya lini utaipata na ya lini utaikosa. Sasa muhimu sana wakati sasa umefika wa serikali ku-*insist* sana juu ya kila taasisi inayotoa huduma kuweka hizi wanaita *Customer Charter*, yaani mkataba wa huduma kwa wateja.
La mwisho kabisa Mhe. Spika, ambalo nataka nilichangie bila kulikosa, ni suala ambalo wenzangu Waheshimiwa Wajumbe wameanza kulizungumza la sekta ya *Oil and Gas*. Katika hili Mhe. Spika, hasa kwenye kujenga uwezo. Nimesoma hotuba ya Mhe. Rais ukurasa wa 13 mpaka wa 14 anazungumzia kujenga uwezo kwenye taasisi zetu mbili za *ZPDC* na *ZPRA*. Mimi napenda pia kusisitiza na kuna mjumbe pia amezungumza hapa, lazima pia tujenge uwezo kwenye taasisi yetu ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoja na Mamlaka ya Ukusanyaji Kodi. Hizi ni muhimu sana zikajengewe uwezo ili ziweze kushiriki ipasavyo katika sekta hii ya uchumi wa mafuta na gesi. Pia …..

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha, nakushukuru sana Mhe. Omar Said Shaaban.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante. Naomba nimwite Mhe. Ali Abdulgulam Hussein, atafuatiwa na Mhe. Mariam Thani Juma na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma ajiandae.

**Mhe. Ali Abdulgulam Hussein:** Mhe. Spika, awali ya yote na mimi naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* kwa kutujaalia jioni ya leo kuweza kukutana tena katika kikao hiki cha Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba na kuunga mkono hotuba, kwa kuwa leo siku yangu ya kwanza ningeomba kuanza kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuweza kuniteuwa mimi kuwa mwakilishi wa kuwawakilisha wananchi wa Jang'ombe, niwashukuru pia wananchi wa Jang'ombe kwa kunichagua kwa kura nyingi na za kishindo katika uchaguzi mkuu

wa mwaka 2020. Imani yangu kwao kuwa kura zile walizonipa, ninawaahidi kazi kwa vitendo katika kuitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kipekee kabisa nachukua nafasi hii kumshukuru mke wangu mpenzi bibi Asha Sheni kwa mchango wake katika safari yangu hii kubwa kwenye maisha yangu. Namshukuru sana na ninampenda sana. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Spika, kwa kuendelea na hotuba hii na mimi binafsi nitapenda nigusie katika mambo mawili au matatu, hasa katika masuala ya utawala bora. Mhe. Spika, katika nchi yetu masuala ya utawala bora ni muhimu sana. Tumeona jitihada zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Saba kwa kuanzisha taasisi zinazosimamia masuala ya utawala bora, ikiwemo rushwa na maadili ya viongozi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika hotuba ya Mhe. Rais ameeleza na imefafanuliwa wazi kuwa ni Rais ambaye kuwa anachukizwa sana na rushwa na anahakikisha atapambana na vitendo vya rushwa na kusimamia utawala bora.

Mhe. Spika, sisi wananchi wa Jimbo la Jang'ombe tutaendelea kumuunga mkono kwa kupambana na masuala ya rushwa. Mhe. Spika, katika ziara zangu katika kutoa shukrani kwa wananchi wa Jimbo la Jang'ombe, waliniagiza nipeleke salamu kwa Mhe. Rais kuwa wanaungana naye bega kwa bega katika kuhakikisha mapambano dhidi ya masuala ya rushwa.

Mhe. Spika, vile vile napenda kuzungumzia suala la michezo. Suala la michezo bado Zanzibar hatufanyi vizuri na tunaona waziwazi timu yetu ya Jang'ombe Boys inahujumiwa na Mhe. Waziri hilo analifahamu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba kwenye hili suala la michezo, uhakikishe unakaa na wadau wa michezo ama tunamuomba Mhe. Rais akutane na wadau wa michezo tumuelezee changamoto zetu ambazo zinatukumba katika hii sekta ya michezo.

Mhe. Spika, Mhe. Rais ameanza kukutana na wadau mbali mbali, lakini bado mpaka sasa hivi hajakutana na wadau wa michezo, na ukizingatia michezo ni sehemu ambayo inatoa ajira nyingi kwa vijana wetu. Kwa hivyo, wananchi wa Jimbo la Jang'ombe wana mapenzi makubwa sana na timu yao ya Jang'ombe Boys, lakini inaendelea kuhujumiwa ambapo sasa hivi sasa tunatengeneza jambo letu ili kuhakikisha kwamba tunataka turudi *firsting*, lakini tunapata hujuma katika Chama cha Michezo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba sana umshauri Mhe. Rais akutane na wadau wa michezo, ili tutowe mawazo yetu na tuoneshe dira katika kuisaidia nchi yetu kwenye suala la michezo.

Vile vile ningependa nigusie suala la utumishi wa umma. Katika hotuba ya Mhe. Rais amehimiza masuala ya nidhamu, uwajibikaji na uwazi katika masuala ya utumishi wa umma. Haya wananchi wetu awamu zote zilizopita wanayatekeleza kwa vitendo. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Rais katika awamu yake awaangalie sana watumishi wa umma kama awali zilizopita, kwa hivyo ni imani yetu atawaangalia watumishi wa umma hasa katika haya mashirika mbali mbali.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni Shirika la Umma ambalo linaendelea kufanya vizuri kama unavyoona ndege nyingi zinaendelea kuja na wafanyakazi wake wanafanya vizuri. Mhe. Spika, kwa taarifa tu pale Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wafanyakazi wengi wanaathirika na masuala ya kelele wanakuwa viziwi, wanaumia na mionzi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aende pale airuhusu bodi iweze kuwapatia japo posho wale wafanyakazi, ili waweze kuondokana na masuala ya mionzi na kuwa viziwi baada ya kustaafu kazi. Hii itawasaidia kwenda kufanya *medical checking* na masuala mengine. Tunaona kuwa sasa hivi wizara ya utumishi wa umma ime-*control* haya mabodi kuweza kubadilisha au kuwajaalia posho wafanyakazi wake.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwenye hilo tunaungana na Mhe. Rais katika hotuba yake ya kuendelea kuimarisha utumishi wa umma na utawala bora. Ni imani yangu kuwa miongozo ambayo itatolewa wafanyakazi wetu wataifuata vizuri.

Mhe. Spika, kwenye suala la maji safi na salama, katika hotuba yake Mhe. Rais alikuwa na dhamira njema ya kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapatiwa maji safi na salama. Kwa hivyo, nimtake tu Mhe. Waziri wa Maji na Nishati Mhe. Suleiman Masoud Makame, aanze kufanya ziara katika Jimbo la Jang’ombe, kwani mabomba sasa hivi yanamwaga maji mengi inaonekana maji yameshafika lakini katika majumba bado hayajaingia. Ukipita mitaani kwenye mitaro maji yanamwagika kila leo.

Mhe. Spika, siku moja usiku saa mbili nilimkuta fundi wa maji maeneo ya Jang’ombe gengeni pamoja na mafundi wake. Hii inaonekana *resource* ya maji imeshafika, lakini ZAWA mpaka leo bado hawajawaungia wananchi katika maeneo yao.

Pia nimtake Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Mhe. Rahma Kassim Ali, aiangalie vizuri njia yetu ya kutoka Kwa Mchina mpaka Skuli ya Jang’ombe, ile ni njia kubwa na tayari nyumba nyingi zimevunjwa na watu wameshapewa fidia kwa kupitisha ule mradi wa *ZUSP*, lakini mpaka leo njia haijatanuliwa na inapelekea wananchi kurudi tena na itapelekea kulipa fidia mara mbili serikali. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Spika, napenda pia nigusie katika suala la idara maalum. Nimpongeze kwanza Mhe. Masoud kwa jitihada zake nzuri ambazo amezianza katika idara hii maalum kwenye wizara hii, hongera sana.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais amezungumza vizuri katika hotuba zake kwamba anataka kuviimarisha hivi vikosi vya SMZ, ili viweze kwenda na kasi ya uchumi ambao tunautegemea. Lakini ushauri wangu kwenye hili, hivi vikosi vyetu ukizingatia hasa hiki cha JKU na hivi vingine ambavyo vimejengwa maalum kwa ajili ya kukuza uchumi wetu, lakini bado havizalishi au havileti yale matokeo ambayo tunategemea.

Kwa hivyo, ushauri wangu ni kuwa tuwahamasishe katika kuweza kujiendesha wenyewe na kuweza kujiendeleza ili ipate yale matokeo ambayo inategemea.

Vile vile ningemuomba sana Mhe. Rais wakati anatengeneza maslahi ya watumishi wa umma, basi awaangalie sana hawa vijana wa vikosi vya SMZ wanafanyakazi nzuri ya kutuliza amani ya nchi yetu na kuweka usalama kwa raia wetu.

Mwisho kabisa, Mhe. Spika, napenda nichukuwe nafasi hii kuwashukuru tena wananchi wa Jang'ombe tena na tena, muda huu wa miaka mitano kila nikisimama hapa nitakuwa naendelea kuwashukuru wananchi wa Jang'ombe kwa kura zile nyingi walizonipigia.

Mwisho kwa kumalizia na mimi napenda niunge mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Ali Abdulgulam Hussein na ahsante kwa namna ulivyoweza ku-*manage* wakati. Naomba nimwite sasa Mhe. Maryam Thani Juma, atafuatiwa na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Said Saleh Salim ajiandae.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kurudi tena kwenye Baraza hili tukufu tukiwa wazima wa afya.

Mhe. Spika, kutokana na Uchaguzi Mkuu wa uliopita wa mwaka huu lazima tumshukuru Mwenyezi Mungu tukiwa tumerudi tena ndani ya Chombo hiki Kitukufu.

Mhe. Spika, sina budi kuwapongeza sana na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Gando kwa kuweza kunirudisha tena kunichagua kwa kura nyingi sana kuweza kuwa Mwakilishi wa Jimbo hili la Gando. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimpongezea sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hotuba yake nzuri mwanana ambayo ameitoa ndani ya Baraza hili Tukufu. Mhe. Spika, nikianza na Mchango wangu nianze na kwenye Sekta hii ya Utalii kama walivyoanza wachangiaji waliyopita.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais wetu kwa kuzungumzia suala la utalii kwa wote kama alivyozungumzia kwenye kitabu hiki kwenye ukurasa wa 12. Mhe. Spika naomba ninukuu Mhe. Rais amesema:

"Nimeahidi na nitaitekeleza ahadi ya kuongeza utalii katika kisiwa cha Pemba".

Mhe. Spika, tunaizungumzia hii kwa sababu ni jambo zuri sana ambalo amelizungumzia Mhe. Rais kwa sababu tumeona kwamba Kisiwa cha Pemba bado kipo nyuma kwa masuala haya ya utalii na ushahidi wa Mhe. Spika, tuna vivutio vingi vya utalii Pemba vikiwemo chumba kile cha chini ya bahari, Msitu wetu wa Ngezi na mambo mengi Pemba.

Lakini tukiangalia kwenye vyombo vya habari ambavyo vinatangaza masuala ya utalii Zanzibar kile chumba si mara nyingi kuona kwamba wanakitangaza kwenye vyombo vya habari. Chumba kile tukiangalia kinaingiza fedha nyingi katika serikali yetu hii ya Zanzibar kinaingiza mapato mengi Mhe. Spika, lakini bado haujatangazwa utalii Pemba.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumzia suala la Msitu wetu wetu wa Ngezi, Msitu ule ulikuwa na vivutio vingi ulikuwa na wanyama, ulikuwa na vitu vingi vya kihistoria. Lakini msitu umeachwa tunaona choyo Mhe. Spika, kuona kwamba Jozani iko hali nzuri, inaeleweka na inatambulika

ndani ya mataifa mbali mbali na ndio maana watalii wanakuja. Lakini tukiangalia msitu wa Ngezi umeachwa umetupwa wanyama hawamo kwa sababu hawakuenziwa lakini wangeenziwa wanyama wale naamini Pemba nako utalii ungekuwa vizuri sana. Lakini kwa maelezo ya Mhe. Rais, Mhe. Spika, tuna imani kubwa sana kwa Mhe. Rais wetu huyu kwamba atasimamia haya kuonekana kwamba utalii Pemba unaimarika.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kuzungumzia suala zima la uekezaji katika Kisiwa cha Pemba. Mhe. Spika, tuna maeneo mengi na Mhe. Rais pia na yeye yapo maeneo yawawekezaji kuja kuwekeza katika Kisiwa cha Pemba na naamini maeneo yapo mengi atakapofanya hivyo, na nawaomba sana wawekezaji wajitokeze katika kum-*support* Mhe. Rais kwa hilo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niendelee kwenye suala zima la Bandari nanukuu Mhe. Spika, Mhe. Rais amesema:

“Vile vile tumedhamiria kuimarisha Bandari ya wete na Shumba Mjini”.

Hili limetupa faraja wananchi wa Wilaya ile ya Wete kwa sababu tumeona kwamba Bandari hii ya Wete wafanyabiashara wapo wengi sana kulikoni hata hiyo Bandari ya Mkoani. Wafanyabiashara wengi wanatoka katika Mkoa wa Kaskazini Pemba lakini tukiangalia bandari hadi leo iko katika hali ile hairidhishi. Lakini kwa maneno haya mazuri ya Mhe. Rais ya kuimarisha hizi bandari zetu naamini yataleta manufaa kwa wananchi wetu na kutoa ajira kwa wingi kwa vijana wetu ambao wako nje wamekaa bila ya ajira. Kwa hiyo nampongeza sana kwa hili kadhalika Mhe. Rais amesema tutaimarisha bandari ya Mkoani ili iweze kuhudumia meli kubwa kutoka nje moja kwa moja kwa lengo la kunyanyua uchumi na biashara kwa Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, ni jambo la kufurahisha sana, kitu kama hiki kikija kwenye Kisiwa chetu kwa kweli wananchi watafarajika sana watakuwa na imani kubwa ya Mhe. Rais wao kwa ajili ya mambo mazuri na maendeleo ambayo watayafanya katika kisiwa hiki. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Rais ahadi hizi ambazo amezielezea kwenye masuala yake mbali mbali azitekeleze kama alivyokusudia.

Mhe. Spika, nikiendelea niendelee kwenye masuala ya barabara, Mheshimiwa amesema kwamba ujenzi wa barabara bora za kisasa ni muhimu kufikia mapinduzi ya uchumi mkubwa wa kisasa. Pia nimpongeze kwa sababu amezielezea kwamba atajenga barabara za kisasa Unguja na Pemba na katika kuelezea kwake pia barabara ya Chake – Wete na Mkoani kupitia Chanjaani na barabra ya Finya- Kicha.

Mhe. Spika, barabara hii ya Finya–Kicha tokea awamu iliyopita ilikuwa ikielezewa sana kwenye Ilani zote zilizopita barabara ya Finya – Kicha imo, barabara ya Chake - Wete imo lakini bado hizi hazijatengenezwa lakini kwa Mhe. Rais alivyoelezea tuna matumaini makubwa kama alivyosema Mhe. Waziri juzi kwenye swali kwamba muda mfupi hii barabra ya Wete – Chake itatengenezwa. Lakini barabara ya Finya – Kicha muda mkubwa sana inazungumziwa lakini mpaka leo hatujajua khatima yake kwa hiyo, kwa vile Mhe. Rais ameielezea humu tunaomba sana hizi barabara zitengenezwe kwa sababu wananchi wanapata shida sana.

Mhe. Spika, niendelee katika matengenezo hayo ya barabara hizo pindipo itakapofikia hatua ya utengenezaji wa barabara mara huwa nazungumzia kwenye Baraza hili Tukufu na na Mhe. Spika, wewe ni shahidi. Muda wa utengenezaji wa barabara watu wanakuwa wanalipwa fidia kwa vipando vyao wanalipwa kwa ajili ya Nyumba zao, lakini mwisho wa siku inatokezea wengine kutopewa zile haki zao na hadi sasa ikiwemo barabara yangu ya Gando napenda sana kusema kwa sababu hii changamoto inaumiza sana namuomba sana Mhe. Rais kwenye uongozi wake aanze kulifanyiakazi suala hili la wale ambao wanadai fidia zao kwenye barabara ya Gando mpaka leo wananchi hawajalipwa.

Kwa hiyo, namuomba sana katika utengenezaji wa barabara hizi ambazo wamezitaja kwenye kitabu hiki azingatie sana wale ambao watapitiwa zile nyumba zao kulipwa kabla ya utengenezaji wa barabara kuondosha haya yaliyotokea kwenye barabara ya Gando - Wete na Wete - Konde.

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye sehemu ya ufugaji katika kitabu hiki Mhe. Rais ameelezea kuhusiana na pembejeo za mifugo dawa za chanjo na kutoa elimu juu ya matumizi ya mbegu bora za mifugo. Mhe. Spika, pia mimi naelezea na dawa za kuulia wadudu ambazo wananchi ambao wanajishughulisha na kilimo, vilimo vyao mara nyingi huwa vinakuwa vinaingiliwa na wadudu fulani lakini wakienda kilimo kutafuta wataalam siku nyengine wataalam wanakuja lakini hawawapi maelekezo zidi ya vilimo vyao vilivyovamiwa na wadudu. Kwa hiyo, naomba sana na hili Mhe. Rais kwa hotuba hii aliyoielezea na hili litashughulikiwa kwa haraka.

**Mhe. Spika:** Anza kuhitimisha Mheshimiwa.

**Mhe.Maryam Thani Juma:** Ahsante, Mhe. Spika, pia amesema serikali itabuni na kutekeleza mikakati madhubuti ya kukomesha wizi wa mifugo na mazao. Mhe. Spika, hili suala ni gumu sana na ni zito kwa sababu hasa Jimbo la Gando, kuna wizi mkubwa wa mifugo. Lakini wizi huu wa mifugo mwisho wa siku wale ambao wanaiba hawashughulikiwi, ingawa Mhe. Hassan juzi alielezea kwamba wizi wadogo wanafungwa lakini wizi ambao wanaiibiwa serikali, fedha za serikali hawafungwi mimi nashauri kwamba hawa wizi wa serikali Mhe. Spika, wataifishwe mali zao ili walipe lakini hawa wizi wa mifugo watiwe adabu wawekwe ndani kukomesha hili ambalo wanalifanya.

Mhe. Spika, kwa vile umeshaniwashia taa naomba sana kwa maelezo haya na Ripoti hii ya Mhe. Rais naunga mkono Hotuba hii asilimia mia moja ahsante.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwanaasha Khamis Juma atafuatiwa na Mhe. Said Saleh Salim na Mhe. Haji Shaaban Waziri ajiandae.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma :** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi tarehe 11/11/2020.

Mhe. Spika, na mimi nitangulize kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo tena kwa mara nyengine ndani ya Baraza hili na kuweza kupata nafasi ya kuwawakilisha wananchi ambao wametuchagua.

Mhe. Spika, mimi nije katika hii hotuba ya Mhe. Rais katika ukurasa wa 19 Mhe. Rais alipozungumzia suala la Ujenzi wa Barabara tofauti tofauti zilizokuwepo katika Visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba. Mhe. Spika, niipongeze sana serikali katika hili na moja katika barabara ambazo zimetajwa katika maeneo haya ni Fumba na Kisauni – Fumba.

Mhe. Spika, suala hili la utengenezaji wa barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ni eneo kubwa hilo la Fumba ni la uwekezaji kwani eneo hili lina umuhimu katika kupatia serikali mapato kwa vile ni la uwekezaji. Kwa hiyo, Mhe. Spika, nilikuwa naomba sana barabara hii itengenezwe ili wazidi kushawishiwa au kuwashawishi wawekezaji katika maeneo hayo. Lakini Mhe. Spika, niombe sana serikali katika upembuzi wao yakinifu walioufanya kuna baadhi ya maeneo hayo wananchi wataathirika kwa kuvunjiwa nyumba zao hivyo, niiombe serikali iangalie kwa makini ili wananchi waweze au waje kulipwa stahiki zao watakapopitisha ujenzi wa barabara hiyo.

Lakini pili, Mhe. Spika, tuje katika kitabu hiki hiki cha Mhe. Rais aliyoitoa hotuba yake kuna maeneo wamezungumzia suala la mazingira na tabia ya nchi, sina mashaka na mipango ya serikali katika mazingira ila naomba serikali kuna maeneo tayari yameshakuwa na uharibifu wa kimazingira baada ya kuchimwa na vifusi hivyo, naomba wizara husika wayapitie maeneo yote yaliyochimbwa vifusi na mawe kwa sasa hayatumiki tena kwa uchimbaji wa fusi na mawe ili kuona athari zilizojitokeza katika maeneo hayo na hasa yakiwemo maeneo hayo Kisauni kuelekea Shakani na kuwatoa wasiwasi wananchi wa maeneo yale kwani inaonekena kutakuwa na athari kubwa kwa yale mashimo yaliyokuwepo pale kuwa hayafanyiwi kitu chochote.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 25 Mhe. Rais amezungumzia suala zima la elimu nimpongeze sana Mhe. Rais kuona changamoto ambazo zinakabili suala zima la upatikanaji wa elimu na ameahidi kutatua changamoto hizo zinazokabili Sekta ya Elimu ikiwemo kuimarisha miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa skuli.

Mhe. Spika, niombe sana serikali katika ukarabati wa skuli za zamani ambazo Mhe. Rais katika hotuba yake amesema moja ni kukarabati hizo skuli za zamani, niiombe basi serikali pia ziangalie na kufanyiwa tathmini zile skuli kumi na tisa zinazovuja. Kwa kweli skuli hizi zinavuja na walimu wanapata shida sana wakati wa kufundisha hivyo katika mipango yao basi na skuli hizi amabazo zina kasoro hizo ziangaliwe ili wanafunzi wapate salama katika kujifunza kwao. Kwa nini nasema hili moja katika skuli hizo ipo Skuli ya Kombeni ya Sekondari iliyopo katika Jimbo la Dimani nayo pia imekumbwa na kadhia hiyo na wananchi na wanafunzi katika eneo lile wanapata shida sana.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 27 maji safi na salama. Mheshimiwa nimpongeze sana Mhe. Rais lakini pia nimpongeze kwa kutuchagulia Waziri ambaye mfatiliaji sana katika wizara hii na kwa kuona kwamba suala la maji suala mtambuka, Mheshimiwa suala la maji limekuwa kilio cha siku zote na bahati nzuri likija suala kama hilo basi Waheshimiwa wengi huwa wanataka kupata nafasi ili waulize kuhusiana na suala zima la upatikana wa maji.

Lakini nimshukuru Mhe. Waziri tulipofanya ziara katika Jimbo la Dimani na akaona katika vile vyanzo vikubwa vya maji ambavyo vinapatikana katika jimbo lile na akasema kwa kuthibitisha eneo lile lina maji ya kutosha lakini wananchi wa Dimani, Fumba, Bweleo pamoja na meneo jirani wanakosa maji yale lakini nimshukuru kwa hatua za awali ambazo amewapa matumaini wananchi wa eneo hilo wataweza kupata maji salama katika kipindi kifupi kijacho. Lakini ushauri wangu Mheshimiwa inaonekana kwamba maji yapo lakini tatizo kubwa ni miundombinu imekuwa chakavu na nina imani katika maeneo yote au mengi yana tatizo hilo. Niwaombe au niiombe serikali izidi kufanya ufatiliaji katika maeneo mbali mbali yanayohusiana na kadhia hiyo ili tuondokane na suala hilo zima la ukosefu wa maji au kutokupatikana kwa maji katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na hayo katika hotuba hii na nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kuyaona yote haya na katika hotuba yake hii kama alivyosema Mhe. Saada ni hotuba ya dhahabu ni dhahabu ya kweli kweli na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafanikisha.

Mwisho, kabisa Mhe. Spika, niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Dimani kwa kunichagua niwe Mwakilishi wao lakini pia niwashukuru Wajumbe wako wote wa Baraza la Wawakilishi jana kunipa imani ya kunieka tena kiti kukusaidia kazi na kuonesha matumaini kwangu nawashukuru sana na naunga mkono hoja hii asilimia mia. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, naomba nimwite sasa hivi Mhe. Saidi Saleh Salim, atafuatiwa na Mhe. Haji Shaaban Waziri na Mhe. Ali Suleiman Ameir atafuatia karibu Mheshimiwa.

**Mhe. Saidi Saleh Salim:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru sana kawa kunipatia na mimi fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako hili Tukufu kuwawakilisha wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe. Awali ya yote na mimi niungane na wezangu walionitangulia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya na kutujaalia kuwa na amani ya nchi.

Pili, nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kunipa imani ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Tumbe na pia niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Tumbe kwa kuniamini naahidi kushirikiano bega kwa bega mpaka mwisho wa awamu hii *Inshaallah.*

Lakini, Mhe. Spika, pia naomba uniruhusu niishukuru sana familia yangu inaoongozwa na mkongwe ndani ya CCM babu yangu Mzee Salum Khamis yeye pia aliniwezesha na kunipa moyo leo niweze kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu.*(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba uniruhusu na mimi nichangie katika hotuba hii ya Mhe. Rais, hotuba ambayo imesheheni mambo mengi mazuri na ya maana. Kiukweli Mhe. Spika, hotuba imemaliza kila kitu na hakuna mtu nadhani humu ambaye hataiunga mkono iko kamili. Mhe. Spika, mimi nataka nianze pale pale kwenye suala la miundombinu ya barabara.

Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Tumbe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mambo mengi mazuri na katika mambo hayo baadhi yake ni kutujengea nyumba za maafa katika Shehia ya Tumbe Mashariki nyumba ni nzuri, ni nyingi, na ni kijiji cha kisasa. Naomba uniruhusu

niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyo chini ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi. *(makofi)*

Mhe. Spika, sambamba na hili kijiji ni kizuri lakini bado kina changamoto ya miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri anayehusika na masuala ya barabara aiangaliye sana barabara ya Finya–Kicha kwa maana haipitiki tena hasa na sio kama ni mbovu lakini haipitiki kwa sasa. Lakini aiangalie barabara ya Mapofu Shumbaviamboni mpaka Tumbe ambayo imepita kwenye kijiji hichi.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye suala la barabara, naomba uniruhusu niongelee suala la maji. Katika Jimbo la Tumbe, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepeleka maji katika vijiji vingi lakini bado kuna changamoto katika vijiji vya Bule, Gombe na Kinoe. Hivi vijiji bado vina changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri, hili nalo aliangalie kwa ukaribu sana.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu niangalie kidogo katika Ustawi wa Jamii. Mhe. Rais Mstaafu Dkt. Ali Mohamed Shein, alianzisha utaratibu wa kutoa pensheni kwa wazee. Naomba Mhe. Spika, uniruhusu nimpongeze sana Mhe. Rais Mstaafu kwa hatua hii aliyofikia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hili naomba nichangie katika hotuba hii kwa kumuomba Mhe. Rais aliyekuwepo hili jambo aliendeleze na wale wazee awaongeze kidogo kadri ya uwezo utakavyowezekana.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nieleke katika elimu. Katika Jimbo la Tumbe suala la elimu halipo vibaya. Mimi niseme tupo vizuri kwa maana ya kwamba Mitihani ya Elimu ya Msingi kwa Jimbo la Tumbe kwa Pemba tumechukua nafasi ya kwanza. Lakini kuna changamoto ya elimu katika vituo vyetu vya *nursery* maarufu tunaita tutu. Vile vituo vina changamoto sana, asilimia kubwa hatuna madarasa, watoto wadogo wanasomeshwa chini ya mishelisheli na miembe. Kwa hiyo wanakuwa wanasoma kwa msimu, kukianza manyunyu wao wapige mbio, kikitoka kiangazi wakakae kwenye mavumbi.

Sambamba na hilo katika vituo vyangu vingi vilivyo katika Jimbo langu la Tumbe vya vituo vya afya, vituo vya elimu yaani maskuli havina walinzi. Hivyo miundombinu inaharibiwa sana kwa namna moja au nyengine. Kwa hiyo, niiombe wizara ya elimu nayo iangalie suala la kutupatia walinzi katika vituo hivyo.

Mhe. Spika, katika Jimbo la Tumbe Wizara ya Afya nayo haipo vizuri sana. Katika Kituo cha Afya cha Chimba hata mlango wa chumba cha daktari sasa hivi upo pembeni, kwa hiyo unapita bila ya kuwa na mlango, hii nayo ni changamoto. Kituo hakina mlinzi, madirisha yake kufungua hadi utumie rimoti yaani ni shida tupu. Katika kituo cha Shumbaviamboni ni hivyo hivyo.

Mhe. Spika, katika suala la umeme tupo vizuri, naomba kutumia fursa hii kuipongeza wizara ya nishati isipokuwa kuna changamoto ndogo ndogo za kawaida. Katika vijiji vyote vilivyomo ndani ya Jimbo la Tumbe vimeshafikiwa na umeme isipokuwa bado mitaa na tushafanya maombi na tunamuomba Mhe. Waziri anipe nguvu katika hili ile mitaa nayo imalizike. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba uniruhusu nimalizie kwa kuyangalia masuala ya uwekezaji hasa katika sekta ya Utalii. Mhe. Spika, Pemba tuna sehemu nyingi sana zenye sifa ya kuekeza katika Sekta ya Utalii. Lakini bado kama walivyotangulia wenzangu Pemba tupo nyuma kidogo kwenye jambo hili. Tuna visiwa vingi kwa mfano tuna kisiwa cha Fundo, Uvinje, tuna magofu ya Msikiti Chooko. Hivi vyote ni vivutio ambavyo hatujawekeza vizuri. Sisi tunafahamu kwamba serikali haiendeshwi kwa pesa zinazoanguka na mvua ni kuwekeza na Pemba tuwekeze ili mapato ya serikali yaongezeke.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naahidi kushirikiana na Mhe. Rais bega kwa bega. *Inshaallah (Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Saidi Saleh Salim, naomba sasa nimuite Mhe. Haji Shaaban Waziri atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ameir na Mhe. Juma Ali Khatib ajiandae.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na siha nzuri. Pili nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana. Pia nakushuru Mhe. Spika, nawashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Uzini kwa kunichagua kwa kura nyingi sana, kwa Zanzibar hii mimi ndie nilieongoza kwa kura. Lakini kulinganisha na nafasi ya Mhe. Rais, ambayo mpaka muda huu tumefikia basi kama tungelikuwa tunacheza karata hapa tumeramba dume. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunapokikamata kitabu hiki cha hotuba ya Mhe. Rais kimemaliza kila kitu. Kilichosalia ni sisi kutekeleza kwa vitendo. Maneno yamemalizika ili kuona sasa yale yaliyozungumzwa yanatekelezwa, katika hilo nilikuwa ninataka kutoa mawazo yangu na nilikuwa ninataka kuanzia kwenye Uk.11-12 kwenye sehemu ya utalii.

Mhe. Spika, Mhe. Rais kwenye kitabu hiki ameuzungumzia utalii kama ni muhimili mkuu wa uchumi katika nchi yetu. Katika suala hilo maana yake nini  tunahitaji kufanya mambo mengi ili utalii uweze kukuza na iwe kivutio kwa watalii waweze kuja wengi. Hivyo basi ningeomba sasa mabalozi wetu wa nchi za nje waliopo nje huko waanzishe matamasha tofauti tofauti ili kuitangaza nchi yetu na watalii waweze kuja kwa wingi zaidi. Ukiangalia hivi sasa watalii ambao wanakuja wengi ni kutoka Urusi, sasa tunatakiwa tuongeze nchi nyengine ili zikweze kuja ili watalii waweze kuwa wengi zaidi. Hilo moja.

Pili, hata wana michezo wetu sasa na waweze kuvaa jezi ambazo zitakuwa zinatangaza Tanzania kuwa ni nchi yetu ya utalii na pia tuwashawishi wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo kujenga kwenye visiwa ambavyo havijajengwa ili navyo viweze kuwa vivutio, kuwe na majengo ya watu wengine kwenda kukaa kule, nina mani kuna watalii wao wakija wanapenda kwenda kukaa kule visiwani.

Nikiondoka hapo, niende kwenye Uk. 27 ambao unazungumzia masuala ya maji. Kama tunavyofahamu kuwa maji ni jambo muhimu sana. Lakini kwenye sekta hii nilikuwa naomba nitoe ushauri, hivi sasa kisima cha maji kama *pump* itakua imeharibika maana yake ni kwamba

watu hawapati huduma mpaka iagizwe mashine nyengine. Mimi ushauri wangu ni kwamba, ziwekwe mashine za akiba na nalisema hilo nina ushahidi Jimboni kwangu hivi sasa kuna mashine mbili zimeungua inafika miezi miwili, watu wanakosa huduma ya maji tatizo mashine hakuna. Kwa hiyo, ningeomba ziwe zinanunuliwa na ziwekwe za akiba kwa kuwa tunajua kwamba ni kitu ambacho kinaharibika.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye elimu. Elimu kama tunavyofahamu kwamba ndio msingi mkuu wa maendeleo na kila mmoja anazungumzia elimu kwa namna yake anayofahamu mwenyewe lakini jambo hili ni kubwa na tunahitaji sasa tufunge vibwebwe ili kuona wanafunzi wetu wanafaulu vizuri.

Ushauri wangu, tuanzishe Kitengo Maalum au Kamati Maalum ya wasomi ukiacha wale wafanyakazi wa wizara ya elimu kwa ajili ya kushauri mambo ya elimu ili kusonga mbele. Wao wawe wanaishaushauri, yaani tuunde tume maalum ambayo itakuwa inaishauri wizara juu ya kukuza elimu yetu hapa Zanzibar. Hilo la kwanza.

Pili, tuunde tume tofauti tofauti kwenye shehia ambazo ziwe zinasaidia kuhamasisha watu juu ya kusoma. Kila shehia kuwe na tume ambayo itakua ipo pale kwa ajili ya kushirikisha watu katika kuhamasisha wanafunzi wawe wanafaulu vizuri zaidi.

Jengine, mara nyengine ni kwamba baadhi ya wakuu wa vitengo vya elimu, huwaambia walimu wakuu kwamba mara hii upasishe, lakini hawawapi hamasa namna gani wafanye ili wapasishe. Kitendo hiki wakati mwengine husababisha hata walimu wakuu kuwaibia wanafunzi mitihani ili tu na yeye aweze kupasisha. Kwa hiyo, tunafikia mahali wanapasi watoto sio tu ile kwa kutumia akili yao bali kwa kusukumwa. Hii inatusaidia elimu yetu iweze kushuka. Kwa hiyo, ningeomba tuwe tunawashauri na kuwapa mipango namna ya kupasisha wanafunzi katika hali ambayo mwanafunzi mwenyewe atakua amejitegemea.

Mhe. Spika, jengine nilikua nataka kushauri kwamba wale wanafunzi ambao wanafanya vizuri basi tungetenga zawadi maalum za kuwapa kama ni motisha ili na wengine waweze kuona kwamba na yeye akifanya vizuri atakuwa amepata motisha wa kile ambacho amekiona kwa mwenzie.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Haji Shaaban Waziri, naomba sasa nimuite Mhe. Ali Suleiman Ameir atafuatiwa na Mhe. Juma Ali Khatib na Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed ajiandae.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Nashukuru Mhe. Spika. Awali ya yote niendelee kumshukuru muumba wa mbingu na ardhi kwa kunijaalia na mimi niweze kusimama katika siku hii ya leo. Lakini nikishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuweza kuniteua na kusimamia kuwa Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Pangawe na hatimae kushinda kwa ushindi wa kishindo.

Mhe. Spika, niendelee pia kwa kukushuru wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako kwa kuweza kutuongoza vizuri katika hili Baraza la Kumi na kuweza kutekeleza yale yote ambayo tumeweza kuyapanga.

Mhe. spika, niendelee na pongezi kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa ushindi mkubwa ambao ameupata unaotokana na Wananchi wa Zanzibar kwa asilimia 76.2. Hii inaonesha wazi kuwa muono wake, shauku yake, ari zake, wananchi wamezikubali na wapo tayari kuongozwa na yeye.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa uteuzi wake na nimpongeze ili aweze kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar na pongezi za pekee ziende kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kaka yangu Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa uteuzi huu ambao ameupata tumwambie na sisi tutashirikiana nae kwa lengo la kuipeleka Zanzibar kule ambapo tunataka ifike.

Mhe. Spika, nianze na mimi kuchangia katika mjadala huu, lakini kabla ya kuanza kuchangia naomba nisome maneno machache ambayo yanatokana na kitabu hichi cha hotuba ya Mhe. Rais, ambayo yanapatika katika Uk.7 paragraph ya mwisho, naomba kunukuu.

"Lengo langu ni tuweze kufahamiana juu ya tulipo, tunapotaka kwenda na namna ambayo sisi katika serikali tumejipanga kutafsiri na kutekeleza Ilani ya CCM 2020-2025 ambayo Chama cha Mapinduzi kinachounda serikali kimetuelekeza tuitekeleze, nafanya hivyo ili wenzetu katika Baraza mtufahamu na kuona namna bora ya kutusaidia kufanikisha azma hiyo."

Mhe. Spika, basi na mimi wacha nisaidie kufanikisha azma hiyo. Nianze katika sekta ya Biashara na Viwanda ambayo maelezo yake yanapatikana katika Uk.16. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Nane kwa kuwa na dhamira njema ya kukuza Sekta ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda hapa Zanzibar. Kuendeleza mashirikiano baina ya serikali na Sekta binafsi hii itapelekea tuweze kuifanya Sekta ya Biashara na Viwanda ili iweze kuendelea.

Pili, Mafanikio yote yana gharama. Naiomba serikali wajielekeze katika mambo yafuatayo ili Sekta ya Biashara na Viwanda iweze kuendelea.

Mosi, niiombe serikali na watendaji, tuhakikishe uwepo wa mitaji ya kutosha ya uzalishaji na uongozi bora ili Sekta ya Biashara na Viwanda iweze kuendelea.

Pili, uwepo maeneo ya viwanda na maeneo ya huduma pamoja na maeneo ya uzalishaji malighafi.

Tatu, tujiekeze katika rasilimali watu ambao wataweza kufanya kazi kwa lengo la kuleta tija na kuukuza uchumi wa taifa hili. Niiombe serikali na watendaji waendelee kuboresha mazingira mazuri ya kodi, ada, soko na tozo mbali mbali mbali zinazowawezesha wafanyabiashara na wawekezaji kuendelea kutuunga mkono katika uwekezaji wao.

Niiombe serikali na watendaji kwamba tunapokata maendeleo lazima tujikite katika kuwekeza. Sekta ya Biashara na sekta ya Viwanda kwa Mwaka 2018-2019 imesaidia pato la taifa kwa asilimia 18.3 ni mategemeo yangu kwa 2020-2021, itasaidia kwa zaidi ya asilimia 25 kwa sababu nia ya dhati na shauku inaonekana.

Katika maendeleo ya viwanda, niiombe serikali kuendelea kushajihisha na kuelekeza katika uwekezaji wa viwanda vya ndani hususan viwanda vya kuchakatia malighafi yaani *Processing Industries*. Tukijikita kwenye *Processing Industries* tutaweza kufanikiwa. Hili tumeliona wakati wa *Corona* viwanda vya ndani viliweza kutusaidia, kwa vile Zanzibar viwanda inawezekana basi viwanda vya kusarifu mazao ya bahari, kilimo na malighafi nyengine ndio muarubaini wetu wa maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, tuna viwanda ambavyo vimeweza kutusaidia nani zaidi ya viwanda vitatu. Kiwanda cha *Basra Textile* niishukuru serikali kwa kuweza kuwekeza katika kiwanda hichi. Kiwanda hichi kimeekezwa na waekezaji jumla Bil.118 kimetusaidia. Kiwanda hichi kitatoa ajira zaidi ya elfu moja na mia sita (1600). Kiwanda hiki kitazalisha kwa siku zaidi ya mita laki mbili na hamsini (250,000) niiombe serikali mwekezaji huyu alindwe, lakini niombe wananchi na wafanya biashara wamtetee mwekezaji huyu kwa kununua bidhaa inayozalishwa hapa nchini.

Tuwekeze katika kiwanda cha *Zanzibar Sugar* ili kiweze kutusaidia uwezo wa Zanzibar *sugar* ni tani elfu ishirini na tano (25,000) kwa mwaka lakini kwa sasa hivi kimezalisha tani elfu nane (8000). Niombe serikali iweze kukaa na mwekezaji huyu tuhakikishe atawezaje kufikia lengo la kuzalisha tani elfu ishirini na tano (25,000) kwa mwaka.

Kuna tatizo la kiwanda cha *Zanzibar Azam Dairy Product Limited*. Kiwanda hiki kwa kuzalisha lita milioni nane (8,000,000) lakini hii leo kiwanda hiki hakizalishi kama kilivyopangwa sababu ya msingi ni bei ya maziwa ambayo wanunuwa kutoka kwa wakulima uwezo wa kiwanda kwa siku kuzalisha tani laki moja themanini (180,000) lakini kwa sasa hivi kiwanda hiki kinazalisha tani mia moja na sabini na tano (175) ni kutokana na sababu mbali mbali.

Niombe serikali tuweze kushirikiana na mwekezaji huyu lakini tushirikiane na wakulima ili kuhakikisha wanazalisha maziwa na wanauza katika kiwanda hiki. Pia niombe serikali iendelee kuwekeza katika kiwanda cha *organic spice* katika Zanzibar.

Nitoke hapo katika viwanda na biashara niende kwenye bandari niombe serikali tuwekeze katika bandari kwani ndio uti wa mgongo wa kwetu naomba tuwekeze basi katika kuangalia suala la kuboresha miundombinu ambayo ipo pale lakini pia tuweze kuboresha rasilimali watu na tuweze kuboresha suala la mapato. Vyombo vilivyokuwepo sio rafiki kwa sasa hivi tujikite katika kuwekeza katika vyombo hivyo.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja kwenye uwezeshaji na wananchi naomba kuhitimisha naomba serikali iweze kuweza kutusaidia kwenye uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi kwa kuweza kuuboresha mfuko wa uwezeshaji lakini kuendeleza programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi lakini kuipa meno idara ya ushirika pamoja na mafunzo mbali mbali. Mwisho nimalizie kwa kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar kwa asilimia mia moja, nashkuru.

**Mhe. Spika:** ahsante sana Mhe. Haji Suleiman Ameir, naomba sasa nimuite Mhe. Juma Ali Khatib atafuatiwa na Mhe. Fatma Ramadhan Mandoba na Mhe. Nassor Ahmed Mazurui ajiandae.

**Mhe. Juma Ali Khatib:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba hi nzuri ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika siku aliyoitoa kwenye ufunguzi wa Baraza letu tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, leo ni tarehe 11/02/2021 tunajadili hotuba nzuri ya Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi lakini leo ni siku muhimu sana Mhe. Spika, nataka niweke kumbukumbu sawa kama tarehe kama ya leo 11/02/1935 ni siku ya Jumatatu ilianzishwa *club* ya Yanga Africans. Mhe. Spika, timu ya wananchi leo imetimiza miaka 86 kwa hiyo imesadifu kwamba tarehe kama na Yanga inatimiza miaka 86. Mhe. Spika, ushindi mkubwa alioupata mgombea urais wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kupata asilimia 76.2 ulitokana na mafanikio makubwa ya kupigiwa mfano juu ya utekelezaji mzuri wa ilani ya CCM ya 2015 – 2020. Ilani hiyo ilitekelezwa chini ya Mhe. Rais mstaafu Dkt. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Spika, kazi nzuri iliofanywa na mimi nilikuwa mmoja wapo kwa sababu sote ukishakuwa Waziri ukishakuwa kwenye Baraza la Wawakilishi tukizingatia hakukuwa na kambi ya upinzani kwa hiyo hata mimi nilishiriki kuweza kuifanyia ushindi huo upatikane. Mhe. Spika, Rais wetu katika kampeni zake aliahidi kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kwa kweli mimi nataka kumpongeza kuna marais wanatoa ahadi hawatekelezi lakini yeye ametekeleza. Nchi yetu Mhe. Spika, mara nyingi huwa inaingia katika vuguvugu la kisiasa mambo yanakuwa hayaendi. Mwaka 1999 nchi yetu ilipoteza pesa myingi sana na muda mrefu sana kwa kuweka muwafaka chini ya Chief Ameka Nyauku.

Mhe. Spika, muwafaka ule haukutekelezeka na muwafaka wa pili ukaja lakini na afya nzuri lakini Mhe. Rais wetu Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi muda mfupi sana kwa kupitia chama chake cha CCM pamoja na mgombea wa urais aliepita wa chama cha ACT Wazalendo Maalim Seif Sharif Hamad walikaa pamoja muda mfupi na kulimaliza tatizo hili la kujenga maridhiano na leo mafanikio humu ndani kuna vyama, kuna wagombea, kuna wawakilishi sita kutoka nje ya Chama cha Mapinduzi. Tuko wawakilishi kutoka ADA TADEA na wawakilishi watano kutoka chama cha ACT Wazalendo haya Mhe. Spika, ni mafanikio makubwa katika utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais kwa hiyo nataka kumpongeza sana mimi katika hotuba yake hii.

Mimi niligombea urais, nakumbushwa hapa ni sawa mimi kama mgomebea Urais wa chama change cha ADA TADEA tulimuona tokea awali kwamba huyu ni Rais mwenye maono ya mbali. Hasa pale Mhe. Spika, alianza kutoa kampeni za aina yake kwa kukutana na watu wa makundi mbali mbali haikupata kutokea hii. *(makofi)*

Tulizoea kufanya kampeni kwenye majukwaa ya mikutano ya hadhara lakini mgombea mwenzetu wa CCM alikua anakutana na watu wa bodaboda, mamalishe, wakulima, wavuvi, wajasiriamali, wafanyabiashara wadogo wadogo, wafanyabiashara wakubwa ametusomesha na sisi wengine Mungu akituweka uhai kama roho zitakuwepo na sisi tutafata nyayo zake tutaiga. Mhe. Spika, sio vibaya kuiga mambo mazuri.

Mhe. Spika, leo tunajadili hapa hotuba ya Mhe. Rais hotuba yake mimi nataka kusema kwamba iwe ndio dira ya kufanya kazi zetu na Mhe. Rais tumebahatika kwamba kila hotuba yake anayoitoa ina kuwa kama muelekeo mzuri katika utendaji wa kazi katika serikali yetu. Kwa hiyo mimi nataka kusema kwamba yote yaliyozungumzwa katika hotuba ile tuyafanyie kazi, kila sekta husika kuna suala la barabara, kuna suala la elimu, kuna suala la viwanda, kwa hiyo mimi bahati mbaya sina jimbo ni mteule wa Mhe. Rais lakini zipo barabara naziona Mhe. Spika, kuna barabara ya Mtambile kwenda Mjimbini mpaka Kangani nataka kumuomba waziri husika katika mipango yake aitazame hii barabara kwa sababu sasa hivi tunapokwenda katika uchumi wa buluu ambapo umo katika kitabu hiki cha hotuba basi uchumi huu wa buluu Mhe. Rais kaelekeza kule Pemba na kule Kangani Kukuu Mhe. Spika, kuna fukwe nzuri sana za bahari na kuna mkondo mkubwa sana kule wa bahari hata waziri anaehusika ni maeneo yake hayo anayafahamu.

Kwa hiyo nataka kusema kwamba sisi sote sasa tuichukuwe hotuba hii Mhe. Spika, kwamba iwe ndio dira yetu ya kufanya kazi kama wawakilishi, kama mawaziri na wale viongozi wengine na wale watendaji wengine kwa hiyo tutaweza kufanikisha yale malengo mazuri ambayo kuwa Mhe. Rais anayo. Mhe. Spika, kuna msemaji mmoja wa ACT Wazalendo hapa Mhe. Omar Said ametoa mchango mzuri sana. *(Makofi)*

Kwanza ameonyesha na sio yeye tu wote wa ACT Wazalendo waliokuja kuzungumza hapa pamoja na wa Chama cha Mapinduzi. Mhe. Spika, hii inaleta nuru kwamba sote tumeridhia uundwaji wa Serikali wa Umoja wa Kitaifa na inaonesha wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi humu ndani wanamuunga mkono Mhe. Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi katika haya yote ambayo ameyaahidi kuyatekeleza. Tokea siku ya awali tulipoona wenzetu amekuja kula kiapo hapa kulikuwa na makaribisho mazuri, kulikuwa na mazungumzo mazuri, kulikuwa na mafahamiano mazuri hakuna vijembi, hakuna kusutana, hakuna kuzomeana hii ni afya nzuri katika kuijenga Zanzibar yetu mpya ambayo chini ya kiongozi wetu Mhe. Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi kwa mapenzi makubwa sana mimi nataka kusema kwamba wawakilishi mmeonyesha kwamba sote tupo kitu kimoja akija mtu Mhe. Spika, humu ndani hawezi kujuwa nani mpinzani nani ACT labda mpaka pale mtu ajitangaze mwenyewe.

Bahati nzuri mimi nimeshiriki katika Serikali ya Awamu ya Saba. Nilipata ushirikiano katika Baraza la Mawaziri kama Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi wenzangu wapo hapa leo tupo *back bencher* lakini bado tupo pamoja kwa hiyo hili ni jambo zuri nawapongeza sana ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi kwa kutupokea sisi tulioteuliwa na Mhe. Rais kuja kufanya kazi ya pamoja humu ndani. Nataka kuwaomba kwamba hotuba hii iwe ndio dira yetu, hotuba hii iwe ndio maono yetu, naamini Mhe. Spika, tutafanikiwa mimi sina mengi naunga mkono yote taliokuwemo humu na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Juma Ali Khatib, naomba nimuite Mhe. Fatma Ramadhan atafuatiwa na Mhe. Nassor Ahmed Mazurui na Mhe. Yussuf Hassan Iddi ajiandae.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia, kutupa afya njema tukakutana hapa tukiwa wazima. Pia napenda nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kwa ushindi wa kishindo pia napenda kumpongeza Mhe. Makamu

wa Pili wa Rais kwa uteuzi wake. Mhe. Spika, naamini Mhe. Rais hatojuta kwa uteuzi wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu tumekuwa tukiziona jitihada zake kila siku.

Mhe. Spika, pia napenda kuwapongeza wanawake wa Mkoa wa Magharibi kwa kunichagua kwa kishindo nikawa mwakilishi wao wa viti maalumu. Pia Mhe. Spika, napenda kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniamini kwa kuweza kunipatia nafasi hii nikawa mwakilishi ninae wakilisha hapa. Mhe. Spika, napenda niipongeze sana hotuba ya Mhe. Rais ambayo aliitoa tarehe 11 Novemba, 2020 ndani ya Baraza lako tukufu. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kauli yake ya yajao neema tupu. Tumeona matunda yake yashaanza kupatikana pale ambapo alipofanya ziara yake ya mwanzo katika Shirika la Bandari ambayo imeanza kuzaa matunda. Mhe. Rais alipofika pale shirika lile lilikua likikusanya mapato bilioni nne kwa mwaka lakini sasa hivi tumeona shirika hili linakusanya bilioni mbili kwa mwezi ambayo ni sawa na asilimia khamsini tunampongeza sana Mhe. Rais kwa jitihada zake ambazo anazozichukuwa.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi kumpongeza Mhe. Rais pale ambapo anapowasimamisha kazi wale wabadhirifu ambao wanaharibu mali na kusababisha kuzorotesha kwa uchumi wa nchi yetu tunampongeza sana na sisi kama wanawake tupo pamoja nae na tunaona maamuzi yake ni sahihi sana.

Mhe. Spika, mimi ningependa kwenye hotuba kuzungumzia suala zima la utalii. Japo kuwa wenzangu wamegusia sana lakini na mimi kwa umuhimu wake naona nigusie kidogo katika suala zima la utalii hawa wawekezaji hasa wawekezaji wanaojenga hoteli.

Mhe. Spika, hawa wawekezaji wajenga hoteli wamekuwa wakinunua vifaa vyao kutoka nchi za nje kwa hiyo hili sio jambo zuri kwa sababu wafanya biashara wetu za Zanzibar wanaleta vifaa vya ujenzi kwa hiyo ipo haja serikali kuwekea masharti wawekezaji hawa ili waweze kununua vifaa hivi ndani ya nchi ili wafanya biashara wetu waweze kufaidika na sekta hii muhimu ya utalii.

Mhe. Spika, pia napenda kugusia suala zima la udhalilishaji wa wanawake. Mhe. Spika, katika hotuba ya Mhe. Rais aliahidi kwa nguvu zake zote kulisimamia kwa nguvu zake zote suala hili la udhalilishaji na tumeona ameanza kuchukua jitihada mbali mbali ikiwemo hii mahakama ya udhalilishaji ambayo imeshaanza kufanya kazi tunampongeza sana Mhe. Rais. Mhe. Spika, tunaiomba sana serikali aliangalie sana suala hili la wakina baba ambao wanawadhalilisha sana kinamama. *(makofi)*

Mhe. Spika, kumekuwa na talaka zisizo na msingi ambazo zinapelekea watoto wetu kuwa hawana washuhulikiaji na kuwa watoto wa mitaani. Mimi ningewaomba kinababa wawaonee huruma sana kinamama, waishi nao kwa mapenzi ili waweze kulea watoto wetu kwa sababu watoto ndio nguvu kazi ya taifa. Mhe. Spika, mimi naona mengi yameshagusiwa na mimi napenda kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Fatma Ramadhan Mandoba, naomba sasa nimuite Mhe. Nassot Ahmed Mazurui atafuatiwa na Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Mhe. Haji Omar Kheir ajiandae.

**Mhe. Nassor Ahmed Mazurui:** Mhe. Spika, kwanza kabisa nichukuwe fursa hii kumshukuru *Allah (S.W)* kwa kutujaalia siku ya leo kuwa tupo hapa katika Baraza lako tukufu tukichangia suala muhimu la hotuba ya Mhe. Rais Dkt Hussein Ali Mwinyi ya tarehe 11 Novemba 2020. Kwanza kabisa kwa dhati kabisa nachukuwa fursa hii nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar ya mawaziri wote walioteuliwa na Mhe. Rais nawatakia kila la kheri. Mhe. Spika, hotuba hii nimeisoma yote na nimeona kwamba ni hotuba ambayo kwamba ina dira ya kuweza kujenga uchumi imara kabisa wa Zanzibar na kurasa zake huku katika ukurasa wa kumi inaeleza mapinduzi ya uchumi na kweli ni mapinduzi ya uchumi.

Katika hotuba hii kuna suala la kuimarisha uvuvi, utalii, mafuta na gesi, bandari na viwanja vya ndege, biashara na viwanda, sekta binafsi, huduma za fedha, nishati ya umeme, teknolojia, kilimo na ufugaji. Naamini kabisa kwamba uchumi ukijengwa na ukajengeka vizuri kabisa serikali itapata fedha za kutosha za kuweza kuhudumia jamii, tunaweza kuhudumia jamii yetu kwa kuwapa elimu bora kabisa, afya bora, maji safi na salama na vile vile kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi kama ilivyoeleza katika hotuba hii.

Katika ukurasa wa kumi na mbili Mhe. Rais kaeleza katika hotuba hii kwamba ana azma ya kuona kwamba maendeleo ya Unguja yaende sambamba na maendeleo ya Pemba hili ni suala muhimu sana, tukiweza ku-*balance* huduma pamoja na maendeleo kuyafikisha katika miji na vijiji vya Unguja na Pemba basi tutaweza kusonga mbele na kuondosha sitofahamu ya visiwa viwili hivi.

Suala jengine ni ukurasa wa kumi na tatu masuala la mafuta na gesi, hapa Mhe. Rais vile vile amenifurahisha sana baada ya kueleza kwamba aliposema tumeshafikia makubaliano ya kindugu baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kulitoa suala la mafuta na gesi katika mambo ya muungano, hii ni *step* kubwa na muhimu sana kabisa na ni suala zuri sana katika kulifanyia kazi ili litoke katika mambo ya muungano ili Zanzibar inufaike moja kwa moja na mapato yote yatokanayo na rasilimali hizo, kama alivyosema Mhe. Rais kwamba wakati wowote suala hili la uchimbaji wa mafuta litaanza.

Mhe. Spika, suala la Bandari na Viwanja vya Ndege ili tuweze kuifungua Zanzibar kiuchumi lazima tuwe na bandari kubwa na yenye ufanisi wa kutosha lakini vile vile tuwe na viwanja vya ndege vyenye ufanisi, uchumi wa Zanzibar kama kisiwa utafunguka moja kwa moja ikiwa bandari zetu na viwanja vyetu vya ndege vitakuwa vina ufanisi na uwezo mkubwa kulingana na bandari zote za Afrika za Mashariki au viwanja vyote vya Afrika ya Mashariki.

Kwa hivyo mimi namuunga mkono kabisa Mhe. Rais kwa suala la bandari na mwenyewe ameeleza katika hotuba yake kwamba haridhiki kabisa na mwenendo wa ufanisi wa kazi inavyokwenda katika bandari zetu na viwanja vyetu vya ndege na katika hotuba hii akaahidi kwamba atafuatilia kwa karibu kabisa utendaji kazi na kuimarisha ufanisi katika bandari zetu na katika viwanja vya ndege, tumeona mashuhuda siku mia za utendaji wa kazi kama Rais wa Zanzibar namna gani anafuatilia katika bandari ya Zanzibar na namna gani mapato yameonekana kwamba ni bilioni nne kwa mwezi, ukilinganisha na bilioni kama hizo kwa mwaka mzima kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Mimi nina imani kwamba ikiwa bandari itaimarika na viwanja

vitaimarika hivi ni vichochoro kwa sasa hivi uchumi wa Zanzibar kukua kwa haraka zaidi na zaidi.

Jengine ninalotaka nimpongeze Mhe. Rais suala la biashara na viwanda linaweza likasaidia sana sana katika kukuza uchumi wa Zanzibar na vile vile kuongeza ajira kwa vijana wetu, kwa hivyo ameelezea vizuri kabisa na mimi namuunga mkono kwamba ipo haja ya kuviimarisha viwanda Zanzibar ili tuongeze ajira kwa vijana wetu na vile vile tuzalishe mali ambazo zitaweza kupatikana masoko ya Tanzania Afrika ya Mashariki na nchi za *SADC*.

Lakini vile vile kwenye hutuba hii utaona kuna suala la Diaspora wamepewa vipaumbele kwamba watapewa fursa za kuja kuwekeza kwao Zanzibar, lakini ningeongeza hapa kwamba iko umuhimu vile vile Diaspora wana kilio wanataka wapate uraia wa nchi pacha kwangu mimi sifikirii kama kuna shida, lakini suala hili vile vile tuwafikirie hawa ni Wazanzibari ingawa wako nje lakini suala la uraia pacha ni *demand* yao na nafikiri kwamba sio suala gumu ni suala la kuamua. Kwa hivyo ningeomba vile vile nao diaspora wafikiriwe na wapewe fursa za kuja kuwekeza katika nchi yao.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa kumi na nane tumeona namna gani Mhe. Rais amejikita katika kushirikiana na sekta binafsi, sekta binafsi katika uchumi wowote ndio injini ya uchumi wa nchi na vile vile kasisitiza katika hotuba yake naomba ninukuu.

"Kwamba Serikali yangu haitakuwa kikwazo kwa sekta binafsi kutakuwa wadau wezeshi".

Pia akasema kwamba hatokubali sasa hivi kurejeshwa nyuma, kwa hivyo sekta binafsi hapa imepata fursa nzuri sana na tunaomba wote ambao wamo katika sekta binafsi wajitayarishe kushirikiana na Serikali yetu katika kujenga uchumi. Kwa hivyo basi zile NGO's za sekta binafsi kama *Chamber of Commerce* na nyengine zijitayarishe ziwe tayari ili kuweza kutoa mchango wao katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Suala jengine ni suala la utawala bora hili sio muhimu sana, ni muhimu sana kuona kwamba tunampa mashirikiano Mhe. Rais, sisi Baraza la Wawakilishi pamoja na wananchi wote tumpe ushirikiano na tukimpa ushirikiano naamini kabisa kila sekta itaweza kufanya kazi zake inavyotakiwa. Naamini kwamba suala la utawala bora tukitoa ushirikiano sote tukamsaidia Mhe. Rais tukaweza ku-*pick point* yale yote ambayo yanawakwaza wananchi yataweza kusaidia sana kuleta maendeleo, wawekezaji wote duniani wanaangalia namna gani Seirikali inawajibika kwa wananchi wake na katika nchi yake.

**Mhe. Spika:** Anza kuhitimisha Mheshimiwa.

**Mhe. Nassor Ahmed Mazurui:** Ahsante kwa kumalizia nasema kwamba *legal frame work* ni suala muhimu sana katika nchi wawekezaji wanaangalia namna gani Mahakama za nchi hiyo zinafanya kazi zake na namna gani sheria za nchi hiyo zinatungwa. Sisi Wawakilishi katika Baraza hili ndio tunaotunga sheria kwa hivyo tujikite kwamba tunatunga sheria ambazo kwamba zitakidhi haja ya kujenga uchumi wetu na kutoa matumaini wawekezaji kutoka nje.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema kwamba naiunga mkono hotuba ya Mhe. Rais mia kwa mia na nawatakieni kila la kheri ahsanteni.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa naomba sasa nimuite Mhe. Yussuf Hassan Iddi atafuatiwa na Mhe. Haji Omar Kheir na kama muda utaturuhusu nitamuita mtu mwengine mmoja Mhe. Mihayo lakini simuoni *around*.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi ambayo ameiwasilisha katika Baraza hili katika mwezi wa kumi na moja.

Mhe. Spika, kwa vile ni mara ya kwanza kusimama katika Baraza hili katika awamu hii nichukue nafasi hii kukishukuru kwanza Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini kupeperusha bendera katika Jimbo la Fuoni. Vile vile niwashukuru wananchi wa jimbo la Fuoni kwa imani yao waliyonipa kuweza kuwa mwakilishi katika chombo hichi muhimu cha kutunga sheria. Nawaahidi sitowaangusha na tutakuwa pamoja bega kwa bega katika kuleta maendeleo na kutatua kero na changamoto ambazo zinalikabili jimbo letu la Fuoni na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa kweli hotuba ya Mhe. Rais ni hotuba yenye maono makubwa na mwelekeo mzuri pamoja na matumaini mema kwa wananchi wa Zanzibar, hotuba hii ya Mhe. Rais ni hotuba bora na kwa mwaka 2020 na ilivuta hisia kubwa sana kwa wananchi ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar na kwa kweli wananchi wamepata matumaini makubwa kutokana na hotuba hii na yale ambayo yamo katika hotuba ya Mhe. Rais, tuwaombe wasaidizi wa Mhe. Rais hotuba hii iandaliwe mikakati mizuri ya muda mrefu na mfupi kwa kuitafsiri kwa vitendo ili basi iweze kuleta tija na neema kama anavyozungumza mwenyewe Mhe. Rais yajayo ni neema tupu. Kwa hivyo tuombe wenzetu waitafsiri kwa vitendo hotuba hii ili basi tija na neema iliyokusudiwa iweze kupatikana.

Mhe. Spika, kumaliza kwa awamu moja ndio kuanza kwa awamu nyengine na waswahili wanasema bila ya jana leo isingekuwepo, nichukue nafasi hii nimpongeze Rais mstaafu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na Mhe. Rais kafanya mambo mengi na mengine aliahidi lakini kwa bahati mbaya hakuweza kuyakamilisha, tuombe sana wenzetu wa awamu hii ya nane yale ambayo Mhe. Rais ameyaahidi kwa nia nzuri tu lakini kwa bahati kutokana na muda hakuweza kuyatekeleza basi na yale wayachukue wayafanye kipa umbele ili wayatekeleze na hapa itakuwa tumemuenzi Rais wetu mstaafu.

Nasema haya kwa sababu sisi Jimbo la Fuoni ni wahanga mwaka 2009 tulitembelewa na Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na kwa kweli aliahidi katika jimbo langu lile la Fuoni ujenzi wa barabara kiwango cha lami kutoka Fuoni Mtundani hadi Skuli ya Kitongani, lakini kwa bahati mbaya hadi leo hii ahadi ile haijatekelezwa. Kwa hivyo nina hofu hata Rais Mstaafu Dkt. Ali Mohammed Shein pia ametoa ahadi ya barabara kutoka Fuoni Melisaba kupitia Birikani hadi Mwera kwamba barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami lakini kutokana na muda nayo haikutekelezwa, tuwaombe wenzetu hizi ahadi za Rais wetu na ziko nyingi ziratibiwe vizuri na ziweze kumalizwa ili wananchi wapate matumaini makubwa lakini tupate na kumuenzi Rais wetu mstaafu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kazi kubwa ambayo ameifanya.

Mhe. Spika, vile vile Mhe. Rais wakati anahutubia Baraza la Wawakilishi alizungumza suala la maji safi na salama na aliahidi kwamba awamu ya nane itamalizikia kazi iliyobakia ikiwemo miundombinu, kwa kweli kwenye jimbo langu la Fuoni kuna viporo vingi sana na hasa vile visima vya *Ras el Khaimah*, naona Waziri simuoni hapa lakini ujumbe utakuwa umemfika. Kwa hivyo tuombe sana wakianza kumalizia hivyo viporo basi waanze katika jimbo langu la Fuoni wananchi kwa kweli wa Jimbo la Fuoni wanapata tabu sana katika kupata huduma hii ya maji safi na salama na kama tunavyojua kwamba maji ni uhai na maji ni huduma muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Kwa hivyo tuombe wenzetu watakapoanza kutekeleza na nimuombe Waziri katika bajeti inayokuja ya 2021/2022 basi vile visima ambavyo vimo katika jimbo la Fuoni vya *Ras el Khaimah* ambavyo havijamalizika basi uwezee kuviingiza katika bajeti na kuweza kukamilika.

Mhe. Spika, Mhe. Rais aligusia maridhiano ya kisiasa na hili alikuwa analihimiza kila anapopata fursa ya kuweza kuhutubia jamii na amelitimza baada ya kumchagua Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, kwa kweli sasa nchi imetulia sana na tunashirikiana vizuri hata humu Barazani. Tulipokuwa tukiangalia Baraza la nane kipindi kile hali kwa kweli ilikuwa si shuari iko tofauti kabisa na Baraza hili la kumi, kipindi kile watu walikuwa wanatoka, wanagoma kupitisha bajeti lakini hali kidogo tumeiona kwa Baraza hili la kumi hali kidogo iko tofauti na mfano mzuri tuliuona jana kura zote zilizopigwa zilikuwa zinasema ndio na mimi nilikuwa natizama kusikiliza matokeo je kuna kura itasema hapana, lakini kwa kweli hakuna sote sisi tuko kitu kimoja na wote waliridhia wale wagombea wote waliopitishwa kwa hivyo hii ni hali ya mwanzo mzuri huu ambao upo haja ya kuendelezwa kwa maslahi ya nchi yetu ya Zanzibar.

Lakini vile vile Mhe. Rais aligusia amani na utulivu na alivinasbisha amani na utulivu pamoja na maendeleo na alisema hivi vitu haviwezi kuachana vinakwenda kwa pamoja, bila ya amani na utulivu hakuna maendeleo na bila ya maendeleo hiyo amani na utulivu vile vile itakosekana. Kwa hivyo tuombe sana wananchi wetu amani hii ambayo iliyokuwepo hivi sasa basi tuidumishe na tuiendeleze ili tupate kufaidi tunu hii ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia, nchi nyingi zimekosa hali hii ya amani na utulivu. Kwa hivyo sisi ambao tumepata neema hii kwa kweli tuendeleze kuitumia vizuri ili tupate kufaidika sisi na vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, hata uwekezaji unategemea sana kuwepo na amani na utulivu wawekezaji wengi hawawekezi palipokuwa hapana amani na utulivu, kwa hivyo tunu hii ya amani na utulivu tukiiendeleza basi ndio tunawashawishi wawekezaji wengi sana kuja kuwekeza katika nchi yetu na kama tulivyoona makampuni mbali mbali yamekuja na tayari tumeshasaini MU mbili katika kipindi kifupi cha uongozi huu wa awamu ya nane.

**Mhe. Spika:** Naomba uanze kuhitimisha Mheshimiwa.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Spika, nimalizie kuhusiana na suala zima la makusanyo ya kodi, vile vile Mhe. Rais aligusia sana kodi na alihimiza sana wafanyabiashara walipe kodi pamoja na kuanzisha mifumo ya *electronic* kwa ajili ya kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali. Tumegundua kwamba baadhi ya taasisi mapato haya yalikuwa yanavuja kutokana na kutumia mifumo iliyokuwa sio rasmi, kwa hivyo awamu ya nane imekuja inabadilisha mifumo

na kutumia mifumo ya *electronic* katika suala la kukusanya mapato pamoja na uendeshaji mzima wa Serikali kiasi ambacho itasaidia sana kuleta ufanisi wa shughuli za serikali na itasaidia sana kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naona ushaniwashia taa naunga mkono hoja hii iliyokuwepo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa naomba sasa nimuite Mhe. Haji Omar Kheir ambae atafuatiwa na Mhe. Mihayo Juma Suleiman Nunga.

**Mhe. Haji Omar Kheir:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii kuwa miongoni mwa wachangiaji kwa hoja iliyopo mbele yetu kwa mujibu wa kanuni na hoja iliyotolewa na Dkt. Saada Mkuya Salum katika kikao chetu cha mwezi wa Novemba.

Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia jioni hii ya leo na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji. Mheshimiwa nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa asilimia 76.2 ya kura katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, bila ya shaka yoyote ushindi huo ameupata kutokana na ahadi zake, mwelekeo wa sera za CCM na ilani ya uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 na mwelekeo wa sera ya mwaka 2020/2030.

Kwa hiyo niendelee kumpongeza kwa ushindi huu ambao ameupata na ni ushindi wa kujivunia wa chama chetu. Ni imani yangu ni kwamba hotuba hii ambayo hotuba hii ni jambo la kisera, hotuba hii itatafsiriwa katika mipango mbali mbali ya kiserikali ikiwemo mwelekeo ya mpango wa mwaka 2021/2022 ambao pengine wiki ijayo ndugu yangu Mhe. Jamal Kassim Ali atauwasilisha na hapo tutapata nafasi nzuri ya kuweza kutoa maoni yetu juu ya kile ambacho kitatokeza kwenye mpango huu tumuombe Mwenyezi Mungu atuwezeshe siku hiyo tuwepo tuweze kutoa maoni yetu.

Mhe. Spika, lakini niwapongeze pia wateuzi wote wa Mhe. Rais kuanzia Makamu wa kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Mwanasheria Mkuu na Mawaziri wote ambao wameteuliwa na wamo katika serikali ya awamu ya nane, bila shaka vigezo vilivyotumika kuwateuwa ni vile ambavyo alivitaja kwenye hotuba yake ya mwanzo hapa Baraza la Wawakilishi niwapongeze sana.

Mhe. Spika, lakini katika kitabu hichi ukurasa wa tatu Mhe. Rais ametoa pole kwa marehemu Abubakar Khamis Bakar tunajifunza nini. Tunajifunza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ni mtu anayeweza kusamehe na hata kuelekea kwenye maridhiano ya kisiasa inaonesha hivyo hivyo kwamba ana ukomavu na ni mtu ambaye anaweze au ni mtu ambaye anayesamehe mambo mbali mbali na hili linatokana na nini sote ni mashahidi wakati wa mikutano yetu ya kampeni vyama tofauti kama ingekuwa si mtu wa kusamehe sidhani kama angeweza kukaa na mwenzake Maalim Seif Sharif Hamad akambwambia tushirikiane katika kuendesha serikali.

Lakini tunajifunza kwamba yeye ni mtu wa kusamehe hivyo hivyo na  nasema hivi mtanisamehe kidogo kwa sababu wakati wa kampeni mheshimiwa alitukanwa sana inataka moyo mkubwa,

huko tusirudi nyuma lakini kusema historia ni wajibu kwamba huko Mwenyezi Mungu atujalie tusirudi tena na tuendee kushirikiana katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije kuanzia ukurasa wa kumi Mhe. Rais amezungumzia suala la mapinduzi ya kiuchumi na amesema yafuatayo naomba nimnukuu.

> "Katika kujenga Zanzibar mpya moja ya ahadi yangu kubwa niliyoitoa kwa Wananchi na ambayo imelekezwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni kujenga Uchumi wa kisasa wa bluu yaani *blue economy*"

Hili limeelezwa kwa ufasaha mkubwa sana ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na akasema sasa ni wakati muafaka wa kuitafsiri kwa vitendo na kuitekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi hasa katika kujenga uchumi huu wa kisasa, wenzangu waliotangulia wamesema na hasa mheshimiwa wengi waliosema hapa juu ya uchumi wa bluu na hivi punde tu alikuwepo Mhe. Nassor Ahmed Mazrui amelizungumza hili kwamba sasa ni wakati muafaka wa kutafsiri kwa vitendo ilani ya uchuguzi hasa kwenye uchumi wa bluu.

Katika uchumi wa bluu sina haja ya kurejea rejea mambo ambayo Mhe. Rais amekuwa akiyasema ni sote ni mashahidi kwamba amekuwa akielezea namna au maana ya uchumi wa bluu na haya masuala ya uchumi wa bluu, nataka niseme kwamba hata katika awamu ya saba iliyopita ambayo mimi nilikuwa mmoja kati ya wahudumu wa serikalli hiyo ya awamu ya saba, tulilianza suala hili hasa pale Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alivyoka kwenye mkutano wa kimataifa kule Nairobi tulilizungumza jambo hili na ndio maana lika-*appear* katika mwelekeo wa sera na katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Kwa hiyo mimi nimpe heko na hongera sana Dkt. Hussein Mwinyi kwa kulipa kipa umbele jambo hili na kwa nini nampa heko kwa sababu amezingatia kwamba pale, alipopewa kijiti cha *relay* na mwenzake ameanzia hapo na bila shaka jambo hili litatunufaisha sote. Uchumi wa bluu kama tulivyoona siku za karibuni tumeweka saini mikataba miwili ule wa bandari ya kisasa ya uvuvi pamoja na bandari ya mafuta na gesi asilia, bandari ya mizigo na kadhalika.

Kwa hiyo bila shaka jambo hili ni kubwa na ni pana na bila shaka sina wasiwasi na mtu aliyepewa dhamana hii ndugu yangu Abdalla Hussein Kombo kwamba atalimudu na ataweza kulifanyia kazi vizuri, yeye mwenyewe kwa sababu ni *marine captain* ambaye ataweza kulifanya kazi vizuri. Kwa nini nalisemea hili kwa nguvu kubwa ndio maana mimi nilimuuliza suala la nyongeza nilishindwa kujizuwia kwa sababu sisi watu wa visiwa uchumi wetu ni wa visiwa na hasa mimi kama nilivyosema jana mimi ni mvuvi, kwa hiyo kwa mwelekeo huu nadhani wavuvi pamoja na wananchi walio katika maeneo ya ukanda wa bahari watafaidika katika sekta hii ya uchumi wa bluu.

**Mhe. Spika:** Naomba uanze kuhitimisha mheshimiwa.

**Mhe. Haji Omar Kheir:** Mhe. Spika, kwa sababu nimesema mwelekeo wa mpango wa 2021/2022 tutaujadili hapo Mheshimiwa Spika tutakuja kukuomba utupe muda mrefu sana tuweze kujadili, mwisho nimalizie kwenye ukurusa wa 35 kwenye kipengele cha amani na utulivu.

Mhe. Spika, mimi nimshukuru sana Mhe. Rais kwa kulielezea jambo hili suala la amani na utulivu ni jambo la msingi sana na ndio muhimili mkubwa sana wa nchi hasa inayotaka kukuza uchumi wake. Amani na utulivu kama alivyosema Mhe. Rais sina haja ya kumnukuu hauhitaji kusimamiwa tu na vyombo ya ulinzi na usalama pekee, bali unatakiwa hata sisi wana siasa tuliomo humu na waliomo nje kulielewa jambo hili kwamba likitetereka hakuna uchumi ambao unaweza ukaimrika.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Rais kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana waheshimiwa naomba sasa nimwite Mhe. Mihayo Juma Suleiman Nunga.

**Mhe. Mihayo Juma Suleiman:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii azimu leo ya kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, iliyotolewa katika Baraza hili tukufu siku ya tarehe 11 Novemba, 2020.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza na mimi kwa ufupi kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pili nikishukuru sana chama changu Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kunipa imani na ridhaa ya kunisimamisha kuwa mgombea wa uwakilishi katika Jimbo la Mwera, wakati huo bahati nzuri ninapozungumza suala zima la mashirikiano maridhiano sisi Jimbo la Mwera tulianza kulifanya hili na mzee wangu Mzee Nassor Mazurui na tulikubaliana.

Bahati nzuri yeye alikuwa mshauri mzuri sana kwangu wakati ule tulikubaliana tufanye siasa za amani, tufanye siasa za kistaarabu, tusitukanane katika majukwaa na kwa bahati nzuri *alhamdullilah* namshukuru sana Mzee Mazurui. katika kipindi chote cha kampeni hakuwahi kusimama jukwaani kumsema Mihayo na mimi katika kipindi chote cha kampeni sikuwahi jukwaani kumsema mzee wangu Mazurui. Kwa hivyo ndani ya Jimbo la Mwera tulifanya siasa za kistaarabu ambazo ndio hizi na Mhe. Rais wetu Dkt. Hussein Mwinyi na yeye ameamua kuziendeleza na kuwathibitishia umma wa Watanzania na Wazanzibari kwa kuendeleza kufanya maridhiano ya kisiasa ambayo na yenyewe yameendelea kutupa amani na utulivu ndani ya taifa letu.

Mhe. Spika, lakini pia nitutumie fursa hii kuishukuru sana familia yangu hasa zaidi mke wangu kipenzi kwa kunipa mashirikiano makubwa sana, amenipa mashirikiano muda wote, wakati wote na kwa hali zote na hata katika wakati wa kipindi kigumu tulichokuwa tunakutana mitaani na Mzee Mazurui, lakini hata niliporudi mke wangu alinifariji vyema, alinipa ushauri mzuri namshuruku sana hakika amekuwa mke bora, mwema anahitaji heshima, anayehitaji kupongezwa na mwenye sifa za pekee katika kisiwa hichi namshukuru sana mke wangu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini pia kama ambavyo nimenza hapo awali kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameanza kutuongoza katika siasa za kistarabu...

**Mhe. Spika:** Samahani mheshimiwa kidogo unajua nashindwa kuelewa kwa nini mtu akipongeza mke shangwe inakuwa kubwa endelea mheshimiwa.

**Mhe. Mihayo Juma Suleiman:** Mhe. Spika, moja kati ya jambo gumu wewe unajua wengi humu wanaogopa kuwasifu wake zao, kwa hiyo sisi wachache mimi na ndugu yangu Ali Abdulgulam ambao tuna upendo wa dhati kwa wake zetu hatuna sababu ya kukaa na kuanza kwenda kuwasifu wengine, tunawashukuru sana wake zetu wanatusaidia sana katika jambo hili na unajua katika jambo la siasa na Mwenyekiti wa *UWAWAZA* anajua hapo katika jambo hili katika kila mafanikio ya mwanamume basi mwanamke anakuwa yuko pembeni lazima tuwashukuru wake zetu.

Lakini pia nitumie fursa hii kumshukuru na kuwapongeza sana wateule wote wa Mhe. Rais tukianza na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Mwenyezi Mungu aendelee kumuafu tumepata taarifa kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha *ACT* kwamba alipata maradhi Mwenyezi Mungu aendelee kumuafu, tunamini sana mchango wake katika taifa hili ni mkubwa sana, uzoefu wake katika taifa hili ni mkubwa sana, kauli yake katika taifa hili inathamani kubwa sana kuliko namna nyengine watu ambao wanaweza wakaitafsiri, yawezekana kuwepo kwake ndani leo yakawa watu wengi wanasubiri kusikia kauli yake. Tutunamini katika siku zijazo Mwenyezi Mungu andelee kumpa afya njema arudi tuje tuendelee kusonga naye na kutoa michango katika taifa hili ili kuweze kulipeleka kutoka sehemu moja kwenda katika sehemu nyengine.

Mhe. Spika, nianze katika sekta kubwa sana ya uchumi na hapa ndipo ambapo taifa letu linaweza kusonga mbele na tukizungumza uchumi wa Zanzibar kama kisiwa maana yake muelekeo wa serikali hii ya awamu ya nane, kama ambavyo tumesema kwamba 'yajayo ni neema tupu' na katika neema hizo basi tumeanza katika uchumi wa bluu na tukienda katika ile *blue economy* maana yake pale kuna *resources* nyingi ambazo lazima tutakapotumia vizuri maeneo ya bahari, tukapotumia vizuri rasilimali zetu.

Lakini uchumi ule wa buluu hauna maana ya tafsiri kwamba yote yatakwenda baharini lakini yapo ambayo yapo katika eneo la ndani ya kisiwa na yenyewe yanaweza yakatumika vizuri. Katika hili tunamini Mhe. Waziri mwenyewe pale amekuwa ni mtu makini, mweledi na mchapa kazi na ana historia kubwa sana maeneo haya ya bahari hasa kule katika eneo ambalo amebahatika kufanya kazi la *ZMA*, anajua nini maana ya uchumi wa buluu, anajua nini maana ya kanda za visiwa zinavyotaka kwenda ku-*transform* kuleta maendeleo katika maeneo ya uchumi wa buluu kipi na kipi kinahitajika tukiweka mkazo katika eneo hili tunaamini muda si mrefu uchumi wetu utaweza ukaimarika sana.

Maana katika ukurasa wa 10 mpaka 11 Mhe. Rais katika hotuba yake amelizumgumzia sana hili na maana yake tukiweka nguvu kwa wavuvi, tukiweka nguvu kwa wakulima wa mwani, tukiweka nguvu maana yake leo zao la mwani limekuwa lina faida kubwa sana. Lakini tukiweka nguvu katika kilimo cha majongoo kimekuwa na faida kubwa sana katika mwili wa binadamu lakini pia hata katika biashara ya kimataifa, ni mambo ambayo lazima sasa serikali yetu inapaswa kujipambanua vizuri zaidi.

Lakini katika sekta nzima ya utalii sisi sote tunafahamu kisiwa chetu uchumi wake asilimia kubwa tunategemea katika biashara ya utalii. Ni lazima sasa imefika Mhe. Spika, tufahamu

jitihada kubwa sana na serikali zimeendelea kuchukuliwa katika sekta hii, tukizungumza roho ya uchumi wa Zanzibar tunazungumza suala zima la utalii na sote tumekuwa mashuhuda kuanzia mwaka 2020 mwezi wa nne baada ya kutangazwa suala zima la uwepo wa virusi hivi vya *CORONA* basi namna ambayo uchumi wetu ulitetereka na kuyumba kidogo imetupa muangaza mpaka wachache wakaanza kufikiri namna ambavyo sasa ikiwezekana uchumi wetu utakapoweza kuimarika, kama kisiwa ifikiri sasa namna ya kwenda kuwekeza katika maeneo mengine hasa katika mashirika yetu haya ambayo tunayo.

Maana sasa *transform* katika kuyaimarisha yetu mara tunazungumzia Shirika la Bima, tunazungumzia *ZSSF*, tunazungumzia Mabenki haya tukiyapa uwezo na nguvu wa kutoka kwenda mbali kufanya kazi na kuwekeza basi kile ambacho kitapatikana, ile faida itakayopatikana inaweza kuja kuingizwa katika uwekezaji sasa au katika maendeleo ya kisiwa, ikiwa tunafanya biashara katika upande wa pili wa taifa letu lakini faida yake inakuja na huu mfano mdogo ambao wenzetu wa *PBZ* wameanza kuanzisha na katika hili maana yake tuendelee kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais kwa kupata leo Mkurugenzi mpya wa Benki hii ya *PBZ.*

Sasa tunaamini na yeye atakuja na mawazo mapya, mazuri yakuifungua Benki hii ya *PBZ* na tunamini itakapokwenda kufanya biashara katika maeneo mengine na tusiishie tu ndani ya Jamhuri, kwa sababu Benki ya *PBZ* ina *brand* kubwa sana katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki maana yake lazima ifungue sasa imefungua *branch* nyingi upande wa Bara lakini sasa inaweza pia kwenda katika katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, kama wenzetu wanapoja kuekeza kwetu basi na sisi tuanze kutoa fursa hizo ya za kwenda kuwekeza katika maeneo yao.

Maana tuaamini wakienda wakifunguka wakiweza kufanya biashara tunaweza tukafanya biashara nzuri na faida itakayokuwa inaweza kuendesha uchumi wa Zanzibar na tukaacha kutegemea ule uchumi wa utalii peke yake, maana yake uchumi wetu unategemea watu kuja wasipokuja kidogo tunayumba.

Mhe. Spika, lakini pia katika ukurasa wa 14 Mhe. Rais amezungumzia suala zima la bandari na hili tumeanza kuona sasa mwelekeo baada ya kusainiwa kwa baadhi ya makubaliano ya namna kuendeleza bandari ya Mangapwani na maeneo mengine, nini sasa azma yake. Azma yake kwamba lazima *entry point* hizi kisiwa zinahitaji kutumika vizuri kama ni *resources* muhimu katika hili na hapa napenda nizungumzie bandari pamoja na *airport* maana yake maana yake tukizungumza uchumi wa Zanzibar lazima maeneo haya mawili tuweze kuyagusia.

Huwezi kuwa na uchumi makini kama utakuwa *entry point* ambazo kwanza hazipo katika mikono salama ya serikali, lakini tunapozungumzia *entry point* ya bandari na *airport* maana yake ni miongoni wa mwa eneo mawili ambayo yako *very sensitive* katika uchumi wa sehemu yoyote Mwenyezi Mungu ametujaalia bandari, tukiitumia vizuri bandari yetu, tukiweza vizuri katika bandari basi neema kubwa itafika, wafanyabiashara *automatic* watakuja, biashara zitafunguka na maisha ya Mzanzibari mnyonge yatapungua na tutapata unafuu katika maisha haya sambamba na tukirekebisha maeneo ya viwanja vya ndege na tunamini kwa aina ya uwekezaji uliofanywa na serikali ya awamu ya nane, hasa katika maeneo ya bandari na uwekezaji uliofanywa katika serikali ya awamu ya saba maana yake awamu ya nane itaweza kuendeleza pazuri katika maeneo la viwanja vya ndege. Maana sasa hatua kubwa itakuwa imefanyika kwa yale ambayo ya uendeleshaji ni mambo ambayo serikali inapaswa kuweka mkazo kupunguza zile changamoto

ndogo ndogo zilizokuwepo na tunaamini kwa aina ya mawaziri tuliokuwa nao wataweza kuisaidia sana serikali na kuipelekea kupata maendeleo katika taifa letu sambamba na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, lakini pia Mhe. Rais alilizungumzia suala zima la barabara na hapa Mhe. Rais aliahidi sana alizungumza kwa kina katika Baraza hili pia alizungumza kwa kina sana alipokuwa katika mikutano ya kampeni. Nipende sana kuishauri serikali yangu na nipende sana kumshauri Mhe. Waziri katika hili la mawasiliano ni lazima sasa wakati umefika, wakati tunatizama *main road* lazima tutizame sasa na *feeder road* ambazo zinafunguka zinakwenda katika maakazi ya watu kwenda katika *main road* ambazo zinasaidia sana katika maendeleo ya taifa hili...

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa nimekuzidishia dakika moja kwa sababu ya kumsifu mkeo. *(Makofi)*

**Mhe. Mihayo Juma Suleiman:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa umuhimu wake naomba moja nimalizie.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 20 Mhe. Rais alizungumza sana na hapa maana yake lazima tukubali hatuwezi kwenda kwenye maendeleo kama hatutokuwa na nishati nzuri ya umeme.

Mhe. Spika, hakutokuwa na maendeleo, hatutokuwa na viwanda, hatutokuwa na viwanda, hatutokuwa na uchumi mzuri kama hatutokuwa na nishati nzuri ya uhakika ya umeme. Hapa tunaona jitihada kubwa ambayo serikali inaanza ku-*invest* lakini lazima tutizame aina ya umeme upi ambao mwananchi wa kawaida atakwenda kuutumia, dunia nzima ukisoma *statistic* umeme wa *hydro* ni umeme rahisi zaidi kwa matumizi ya mwananchi katika suala zima la kuleta maendeleo na sasa maana yake tutakuwa na changamoto ya umeme kidogo kama ambapo itafika miaka miwili hatuto-*invest* vya kutosha katika jambo hili niiombe sana serikali yangu, nimuombe sana Mhe. Waziri, mimuombe Mhe. Rais, nimuombe sana Mhe. Makamu wa Pili.

Lazima sasa tufanye uharaka kutizama namna ya kuwekeza vya kutosha katika sekta hii ya umeme ili kuweza kupata umeme wa uhakika

Mhe. Spika, baada ya kusema maeneo yangu hayo na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwera nauonga mkono hoja asilimia mia juu ya mia nakushukuru sana Mheshimiwa Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mihayo Waheshimiwa Wajumbe kwanza na mimi nichukuwe nafasi hii kuwasifu waheshima wawili Mhe. Ali Abdulgulam Hussein na Mhe. Mihayo Juma Suleiman kwa kukumbuka kuwasifu wenza wao lakini wamewasaidia zaidi waheshimiwa wa kiume lakini hakuna hata mmoja mheshimiwa mmoja wa kike ambaye amenyanyuka hapa akamsifu mumewe na tungetemea wangelifanya hilo lakini wamejitolea waheshimiwa wa kiume. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe nina tangazo moja ni kwamba Mhe. Mnadhimu wa Chama Cha Mapinduzi anahitaji waheshimiwa wa CCM wabaki humu kwa ajili ya kikao cha dharura cha *Caucus* mara baada ya kuahirishwa kwa hii shughuli yetu.

Waheshimiwa wajumbe wachangiaji bado wapo lakini muda hauruhusu tena maana yake umeshamalizika kwa hiyo kesho tutaendelea na sina haja ya kuwatamka hapa kwa sababu ni zaidi ya watu sita hapa wapo, watu saba mimi naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuruni sana kwa michango ilikuwa mizuri maana yake michango ikiwa mizuri hata Spika kusinzia hawezi unasikiliza mambo yako vizuri sana.

Kwa mantiki hiyo sasa naomba niakhirishe shughuli za Baraza mpaka kesho saa tatu barabara za asubuhi.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 12 Februari, 2021 saa 3:00 asubuhi)*